# UFAHAMU NA UHURU

Ulinganifu wa kina kati ya Uislamu na Ukristo



Na Dk. Daniel Shayesteh

Muasisi na mwanzilishi wa EFD

# Ufahamu Na Uhuru

**Vitabu vingine vya mwandishi**

*The House I Left Behind*

*Islam and the Son of God*

*Christ Above All*

Ujumbe uliopo kwenye kitabu hiki pia unapatikana kwa mfumo wa pantaninga (DVD) na santuri za sauti (CD). Kitabu hiki kina rejea zote za maandiko katika DVD na CD za sauti. Kwa nyongeza zaidi, pia kuna maelezo ya ziada kwa chini kama tanbihi.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vitabu vya Daniel Shayesteh.

www.exodusfromdarkness.org

7spirits@gmail.com

# Ufahamu Na Uhuru

## Ulinganifu wa Kina kati ya Uislamu na Ukristo

**Na Daniel Shayesteh**

**Exodus from Darkness, Inc.**

Hatimiliki © 2016, Exodus from Darkness, Inc.

Kitabu hiki kina hatimiliki, lakini kinaweza kuchapishwa au kusambazwa kama kilivyo au kwa sehemu endapo tu ukurasa huu wa hatimiliki wenye jina la mwandishi, Daniel Shayesteh, na mchapishaji, Exodus from Darkness, umeambatanishwa. Endapo kitabu hiki au sehemu ya maudhui yake yatatumika kama zana ya kufundishia, ni lazima mwandishi atajwe. Kwa vyo vyote vile hakipaswi kurekebishwa au kubadilishwa.

Mwandishi: Daniel Shayesteh, 1954 **Ufahamu Na Uhuru:** Ulinganifu wa Kina kati ya Uislamu na Ukristo.

Kimechapishwa na Exodus from Darkness, Inc.
York, PA, USA.

ISBN: 978-9987-859-98-6

www.exodusfromdarkness.org

usa@exodusfromdarkness.org

## Yaliyomo

Dibaji ya mwandishi (7)

Utangulizi (8)

Kwanini Tunahitaji Ufahamu Binafsi? (15)

Uhitaji wa kuboresha tamaduni zetu – Kwanini, kivipi (27)

Mifano ya Mabadiliko Binafsi Kutokana na Maisha ya Daniel (38)

Mungu – Je Mungu Yupo? (51)

Namna ya Kutofautisha Kati ya Mungu wa Kweli na wa Uongo? (64)

Tofauti Kati ya Mungu wa Uislamu na Mungu wa Ukristo (74)

Je! Mungu wa Uislamu anaweza kuwa kiongozi mzuri? (88)

Je! Una Amani na Mungu wa Uislamu? (104)

Je! Qura'ni ni Neno la Mungu wa Kweli? (116)

Je! Uislamu ni Dini Sahihi na ya Mwisho? (132)

Kati ya Yesu na Muhammad, nani anaweza kuwa kiongozi bora kwako? (146)

Uongozi Katika Uislamu ni Vurugu (157)

Kati ya Sharia ya Uislamu na Upendo wa Kristo, upi ni mfumo bora ? (170)

Ubinadamu Unahitaji Marafiki Sio Maadui (180)

Injili ya Yesu Kristo Ina Maelekezo Sahihi Kuhusu Mahusiano (190)

Qura'ni Inamtaka Mtume wa Uislamu Kuiamini Biblia (197)

Tuhuma za Uislamu Dhidi ya Imani ya Kikristo Hazina Msingi (208)

Michezo ya Kisiasa Katika Uislamu Inakinzana na Imani Yake (220)

Tumaini La Kuwa Huru Dhidi ya Vitisho, Uongo na Michezo ya Kisiasa (237)

Hakuna Wokovu Nje ya Yesu (245)

Yesu ni Njia, Kweli na Uzima (256)

Bibliography (263)

## Dibaji

Kitabu hiki kinaleta mwanga kuhusu imani kuu katika Uislamu na kuzilinganisha na Ukristo na imani zingine - taarifa ambazo waislamu wanapaswa kujua. Pia kinadhihirisha namna viongozi na walimu wa Uislamu walivyowaweka Waislamu gizani ili wasijue baadhi ya mambo nyeti kuhusu imani zao.

Kitabu hiki ni ushuhuda wa mambo ambayo mimi mwenyewe nimeyajua wakati wa safari yangu ya kutoka Uislamu kwenda kwa Kristo. Muda mwingi katika safari yangu nilishangazwa sana na jinsi nilivyokuwa nimeshikiliwa kwenye ujinga wa asili ya siasa za Kiislamu, na kuzuiwa kujua Uislamu katika muktadha wa ulimwengu, na muhimu zaidi kutokuona uzuri uliopo ndani ya Yesu Kristo.

Ninashukuru kwamba maisha yangu yamebadilishwa na Yesu Kristo, na kwamba ameniwezeshwa kuwashirikisha na wengine kuhusu dini na mitazamo ya kidunia ambayo inaweza kupotosha wengi wakiwemo Waislamu. Maombi yangu ni kwamba, ujumbe wa kitabu hiki uwe nuru kwa Waislamu na wasio Waislamu Duniani kote, na kuwasaidia kupata hifadhi ndani ya Mfalme wa Amani, Yesu, ili kwamba wafurahie maisha ya amani sasa na hata milele.

Daniel Shayesteh

## Utangulizi

Hivi punde, ninakwenda kuanza majadiliano marefu na wewe kupitia mada 21. Kabla sijaingia hatua hiyo, nataka nikufahamishe katika sehemu hii ya utangulizi kuwa nimeandaa mfululizo huu katika mfumo wa majadiliano. Hata kama sitaweza kusikia sauti yako binafsi, lakini bado nataka kuyaita majadiliano kwa sababu unaweza ukaruhusu dhamiri yako izungumze na kukufanya utathimini kila jambo ninaloliibua. Majadiliano yetu hayawezi kuwa na maana kama tukipuuza dhimiri zetu. Kwa hiyo, tuahidiane tungali mwanzoni mwa mfululizo huu kwamba hatutapuuza sauti za dhamiri zetu.

Kila mada katika mfululizo huu ina kichwa, lakini mfululizo wote unaitwa “Ufahamu na Uhuru”. Nilikutana na Yesu Kristo katika namna ya ajabu sana. Alinisaidia kuyaendea maisha kwa ufahamu, kuwa na sababu ya imani yangu, kutotii nisichokijua na kuishi kama mtu huru.

Nimezungumza na maelfu ya Waislamu, wenye elimu na wasio na elimu, watulivuS na wenye vurugu, viongozi na wafuasi, moja kwa moja na pia kupitia redio, runinga na mtandao kwa miongo iliyopita. Nimeona matokeo makubwa ya majadiliano ya kimatiki, na jinsi mitazamo ya wengi wao ilivyobadilika kwa sababu ya kufahamu umuhimu wa uhuru katika

kila jambo kwenye maisha. Uzoefu huu umenihamasisha kuandaa mada hizi ili kufungua njia kwa ajili yako na mamilioni ya Waislamu wengine, na wasio Waislamu, pia kuonesha namna Ufahamu na Uhuru vinavyohusiana.

Hatuwezi kuwa huru kiroho wala kijamii kama hatutakuwa waangalifu katika imani na tamaduni zetu na kutafuta njia sahihi ya kujinasua kutoka kwenye misingi potofu. Ndiyo maana nimechagua kichwa cha "Ufahamu na Uhuru" kwa mfululizo wote. Ufahamu na Uhuru ni mahitaji mahususi na muhimu sana katika maisha yetu. Kati ya hayo hakuna linaloweza kuwepo peke yake na likaleta maana halisi.

Imani na dini nyingi zimeshikilia waumini wake katika ujinga na kuwanyima uhuru wao. Ni dhahiri kwamba mamlaka yao yanatokana ukosefu wa Ufahamu na Uhuru wa watu wao. Dini yeyote inayowazuia watu wake kulinganisha misingi yao na ya dini zingine ili kujua iliyo bora zaidi ni kikwazo kwa uhuru wa watu wao. Uhuru maana yake hakuna chochote chenye uwezo wa kukuzuia kujua ukweli wa mambo. Watu ambao hawana sababu sahihi za imani yao hawana uhuru na wala hawajui uhuru maana yake nini.

Unapaswa kufahamu kuwa una wajibu wa kutoa sababu zenye nguvu kama unadhani imani yako ni bora na sahihi. Mara nyingi watu waliniambia uso kwa uso

kuwa imani yao ndiyo ilikuwa bora na sahihi. Baada ya kuwataka waniambie maana ya bora na sahihi, waligundua kuwa madai kuhusu imani yao yalikuwa si kweli. Ndiyo maana nimekusudia kukusaidia uwe na sababu kuhusu madai yako.

Baada ya kusikiliza mazungumzo yangu, itakuwa rahisi kwako kujua kwamba, kuwa na imani sio kushindana na wengine au kuwatawala, bali ni kuangalia kama inathamini misingi au uwezo wako wa kuchanganua na kuamua. Imani ya kweli lazima iwasaidie watu kuelewa mambo kwa undani. Hii ndiyo sababu iliyonihamasisha kuleta hizi mada 21 tofauti, ili kuonesha ulinganifu mpana kati ya Uislamu na Ukristo. Nataka nikuthibitishie kuwa ufahamu ni jambo muhimu katika kupata imani sahihi inayotoa uhuru.

Moja wapo ya vikwazo vikubwa katika nchi za kiislamu ni vizuizi vya kuuchunguza Uislamu na kuulinganisha na imani zingine. Watu hawana uhuru wa kuchunguza dini yao. Sio hivyo tu, bali pia waislamu wanalazimishwa kusifia Uislamu na kukashifu misingi ya imani zingine zisizo za kiislamu hata kama zina umuhimu na ni sahihi.

Kuzuiwa kufahamu kuhusu imani yako au imani zingine ni ufungwa. Kama una kiu ya uhuru, unapaswa kupata ufahamu wako binafsi kwanza, kutambua

vikwazo katika utamaduni na imani yako na kisha kutafuta njia sahihi ya kuvishinda. Ufahamu ndiyo ufunguo pekee wa kupata uhuru. Pasipo ufahamu, tutakuwa tunakandamiza dhamiri zetu na kuwa wafuasi vipofu katika huduma ya wale wanaokusudia kunufaika kwa ujinga wetu. Ndiyo maana, mada mbili za mwanzo katika mfululizo huu zinahusu ufahamu binafsi na maboresho ya kiutamaduni ili kuamsha dhamiri yako na kutengeneza kiu ndani yako itakayokuwezesha kuvunja minyororo na kukuweka huru.

Nataka nikukumbushe kwamba, kupata kilicho bora ni haja yako kubwa na haja ya kila mtu ulimwenguni. Vitu vizuri na vilivyo bora ni kwa manufaa yetu. Ndio maana tunaepuka kuwa na vitu vibaya na visivyo bora. Hii pia inahusika na masuala ya imani au dini. Tunapaswa kuwa na imani iliyo bora. Watu wengi wamerithi imani zao kutoka kwa wazazi au jamii bila kujua kama zina ubora au la. Watu wanapaswa kuwa na imani inayowapa ujasiri, kuheshimu uhuru wao wa kuchagua na kuwapa viwango bora vitakavyowasaidia kuwa na mafanikio katika maisha na mahusiano yenye amani katika familia zao na wengine.

Kuwa na imani nzuri kama hii kunahitaji juhudi, uwazi, jitihada binafsi za kuchunguza na kulinganisha, na kisha ujasiri wa kufanya maamuzi sahihi. Kupata

imani sahihi na bora sio manufaa kwetu pekee na familia zetu, bali pia itaangaza jamii zetu na kuboresha tamaduni zetu. Maboresho ya tamaduni yatapelekea watu wafanikiwe katika nyanja zote za maisha na kuwaongoza kugundua kanuni bora za maisha kwa ubunifu na maendeleo zaidi.

Tutadanganywa na wapotoshaji na kuwa wahanga wa mbinu zao zisizofaa kwenye Nyanja zote za maisha kama hatutatumia akili, moyo na dhimiri. Nimejaribu kuibua mambo mengi katika mazungumzo yangu ili uweze kuelewa kuwa kukosa ufahamu kunaweza kutuweka kwenye mitego katika namna nyingi. Lakini kujua ukweli kutatuweka huru.

Nimezipanga mada katika mtiririko, kiasi kwamba mwisho wa mada moja utakusaidia kuelewa vizuri mada inayofuata. Mada mbili za mwanzo zitakusaidia kuthamini ufahamu. Vile vile zitakukumbusha kwamba una uwezo wa kuthamini kila jambo na kufanya maamuzi sahihi wewe binafsi. Kufuatia mada hizo, nimetoa mifano ya maisha yangu kuonesha namna ambavyo watu walikuja wakanisaidia kutumia ubongo, moyo na dhamiri yangu na kupata uhuru niliopewa na Mungu ambao wale wapotoshaji waliukandamiza kwa sababu ya ujinga wangu. Kama wengine walivyonisaidia nami pia nataka nikusaidie upate uhuru ili uwasaidie wengine kuwa huru. Uhuru ni

mzuri kwa kila mtu. Kila mmoja wetu anapaswa kuwa mhamasishaji wa uhuru.

Katika mifano yangu, nimezungumza kuhusu Mungu kwenye mada tano katika namna ya ulinganifu ambayo huwezi kukosa lolote kuhusu Mungu. Neno Mungu ni neno la msingi katika dini yako na dini zingine zote. Unapaswa kujua umejengwa juu ya mzizi upi. Kwa kufahamu msingi wa dini yako utaweza kuamua ama kuendelea nayo au kuiacha na kutafuta bora zaidi. Tumeumbwa kupata vilivyo bora zaidi.

Nitaweka wazi kila kitu kuhusu Mungu ili ufahamu kama Mungu yupo au la. Kama yupo, je anajificha au anajidhihirisha kwako. Pia utajifunza jinsi ya kutofautisha kati ya Mungu wa kweli na wa uongo na kama Mungu wako ni kiongozi mzuri kwako au unapaswa kutafuta mwingine wa kweli.

Kwenye mada zilizosalia, nimeonyesha kifilosofia, kiitikadi na kimaadili namna ambavyo picha potofu ya Mungu inavyoweza kupotosha jamii na maisha katika namna nyingi. Ninapozungumza kuhusu tatizo natoa na ufumbuzi pia. Nimejitahidi kila niwezavyo kukusaidia uondokane na matatizo na mikanganyiko ya imani yako na uishi maisha huru.

Nakushauri, uthamini utambulisho wako wa uliopewa na Mungu, ruhusu akili, moyo na dhamiri vifanye kazi

pamoja katika kila jambo unalosikia kutoka kwangu, usiruhusu mtazamo wa upande mmoja ukuzuie kusikiliza mazungumzo yako. Nakuahidi kuwa kusikiliza kwa makini ni kwa manufaa yako binafsi na wengine wote - waislamu na wasio waislamu.

Asante sana kwa kuwa tayari kutembea nami kupitia mfululizo huu.

Daniel Shayesteh

Januari 2016

## Kwanini tunahitaji Ufahamu Binafsi?

Ufahamu binafsi kuhusu tunachoamini au wanachoamini wengine. Tunachopaswa kujua ni kwamba maisha hayawezi kwenda vizuri bila ufahamu na udadisi.

**Pasipo ufahamu tutabaki nyuma.**

Ufahamu ni kama mwanga maishani mwetu. Tunahitaji ufahamu kwa kila kitu katika maisha; kununua chakula, nguo, nyumba, magari, kutafuta mwenza, marafiki, kulea familia, kukubali au kukataa imani, misingi na vitu vingine vyote. Fikiri kama tungefumba macho wakati wa kuchagua vitu; wachumba au marafiki pasipo kujua sifa na haiba zao. Matokeo yake yangekuwaje? Kwa hiyo ni muhimu sana kuwa macho wakati wa kuchagua misingi itakayofanya mahusiano yetu kisiasa, kijamii na kiuchumi kuwa ya amani, furaha na maana.

**Kuwa na imani sahihi unahitaji ufahamu.**

Kama hatujui njia sahihi, hatuwezi kufikia hatima yetu. Kwa mantiki hiyo hiyo, kama tusipojua imani sahihi tutapotea kiroho na hatutaweza kukutana na Mungu.

**Maisha bila ufahamu ni upotevu kabisa.**

Mtu mmoja asiye na hekima alitaka kujenga nyumba, lakini hakujua kama nyumba inapaswa kujengwa kwenye msingi imara. Kwa hiyo alijenga juu ya mchanga. Mafuriko yalipokuja nyumba ilianguka. Kama angejua angejenga nyumba yake mahali ambapo ingestahimili mafuriko. Kwa hiyo kama hewa ilivyo muhimu kwa kuishi ndivyo ufahamu ulivyo muhimu kwa kupata imani bora. Maisha ya kweli yanapaswa kuwa ni mchakato wa kutafuta vilivyo bora ili kukidhi mahitaji yetu. Hatuwezi kuwa na hatima nzuri kama hatutachagua imani bora kwa maisha yetu. Utafiti ni karama ya Mungu kwa kila mtu. Utafiti unapaswa kuwa ni sehemu ya imani yetu. Hatupaswi kufuata imani zinazozuia utafiti binafsi na kukataza watu kuchagua imani wanazotaka.

**Ili kufanya maamuzi tunahitaji ufahamu.**

Tunahitaji ufahamu kufanya maamuzi sahihi binafsi na kwenye familia au jamii. Maamuzi yetu yanaathiri maisha yetu binafsi, familia na jamii kupitia mahusiano. Kwa hiyo uamuzi wenye ufahamu utakuwa mzuri na wenye tija kwa kila mmoja. Lakini uamuzi usio na ufahamu hautakuwa na tija na pengine ukaleta madhara kwa watu wote hasa ukifanywa na viongozi ama kwenye familia au biashara au taifa. Wewe ni

kiongozi tayari au utakuwa kiongozi muda mfupi ujao. Kwa hiyo unapaswa kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya mafanikio kwenye maisha binafsi na familia. Kwa hiyo ufahamu ni muhimu kwa kila kitu.

**Hatua gani tunahitaji kuchukua ili kujenga ufahamu binafsi?**

Ninakwenda kukupa hatua kumi zinazotegemeana za kupata ufahamu.

*Hatua ya kwanza ni kufumbua macho na masikio.*

Macho ni kwa ajili ya kuona na masikio ni kwa ajili ya kusikia. Wale wanaofumba macho na masikio kwa falsafa hii rahisi au wanaozuia njia ya wengine kuona na kusikia, wanajitenga wenyewe na wengine kwa Mungu na wanadamu. Macho na masikio ya Mungu wa kweli wakati wote yapo wazi; wanadamu wanapaswa kufuata kanuni hiyo hiyo kwa maisha ya kweli. Maisha yatakuwa na tija zaidi kama tukitumia macho, masikio, mioyo na akili kwa kujifunza. Yeyote anayependa ukweli lazima aangalie imani zingine, asikilize mafundisho yao, apambanue na kulinganisha na imani yake, achague iliyo bora kwa ajili yake, na kuishi sawa sawa na mafundisho yake. Mtu yeyote au imani

inayokuzuia kutafuta ukweli, haiwezi kuwa inapenda ukweli au kuhamasisha upendo.

*Hatua ya pili ni kujua vikwazo na suluhisho.*

Vipi ni vikwazo kwako kujifunza? Je imani yako ni kikwazo? Je wewe mwenyewe ni kikwazo? Je familia yako ni kikwazo? Je matatizo ya kijamii na kisiasa kwenye jamii yako ni kikwazo? Je serikali au kiongozi wako ni kikwazo?

Haijalishi ni vikwazo vya namna gani vipo dhidi yako, familia, nchi au hata dunia. Unapaswa kuvijua na kutafuta njia nzuri ya kujinasua kutoka kwenye madhara yake.

*Hatua ya tatu ni kwamba tunahitaji dhamiri zetu zifanye kazi.*

Dhamiri ni wakala mzuri sana katika kuthibitisha na kuongea ukweli. Hupaswi kukandamiza dhamiri yako wala kuinyamazisha. Mtu anakuwa amekufa kiroho kama dhamiri yake haina sauti. Dhamiri iliyo huru hukubali kukosolewa na mtu mwingine aliye sahihi hata kama humpendi. Watu wanaopuuza haki za wengine ni wale ambao wanapuuza sauti za dhamiri zao wenyewe. Wale wanaokataa ushauri mzuri na njia nzuri ya maisha ni wale wanaokataa umuhimu na maana ya dhamiri zao wenyewe. Yeyote anayepuuza

dhamiri yake mwenyewe hawezi kuheshimu haki za wengine. Dhamiri huru haiwezi kuturuhusu kudharau haki na uhuru wa wengine hata kama ni wapinzani au adui zetu. Dhamiri huru inatufundisha kuwa hakuna tofauti kati ya mfalme na omba omba, kiongozi na mfuasi, bwana na mtumwa, mume na mke; wanadamu wote wana haki ya kuwa huru. Kwa hiyo unapaswa kujitenga mbali na chochote hata imani inayozuia dhamiri yako.

*Hatua ya nne ni kwamba tunahitaji kuwa na kiu ya kutafuta kilicho bora.*

Hatuwezi kupokea maji bila kuonyesha kuwa tuna kiu. Ufahamu wa misingi bora pia hauwezi kupatikana bila kuwa na kiu na mbinu.

Je unashauku ya maisha bora na yenye tija? Kama ndiyo, basi unahitaji kutafuta hilo kwa kiu. Ni kiu ya ufahamu na uvumbuzi itakayodhihirisha ukweli kwetu na kisha kutuweka huru kutokana na imani potofu.

*Hatua ya tano ni kwamba tunapaswa kuwa na uhuru binafsi.*

Watu wameumbwa kuwa huru; vinginevyo watabaki nyuma kwenye kila eneo la maisha. Tunapaswa kuwa na uhuru binafsi na uwezo wa kutafuta ukweli. Kwa sababu tunawajibu binafsi wa kuishi na kuonyesha

ukweli kupitia maisha yetu wenyewe, kwa hiyo tunapaswa kujua ukweli kwa uwezo wetu wenyewe. Kwa maneno mengine, ukweli hautakuwa na maana bila kujitawala. Mtu hawezi kutumia uwezo wake kamili kwenye kutafuta ukweli kama hana kujitawala na uhuru. Kwa upande mwingine kama huwezi kutafuta ukweli kwa uwezo wako wote basi huwezi kuupata ukweli kamili. Kwa sababu hiyo kama kuna chochote katika jamii yako ikiwemo imani yako inazuia uhuru na uwezo uliopewa na Mungu wa kutafuta ukweli, basi unahitaji kutafuta njia bora ya kuvunja huo mnyororo na kujinasua mwenyewe. Kujitawala katika uchunguzi kunaleta ufahamu thabiti kwenye maisha na ufahamu thabiti unafungua mlango wa mafanikio kwenye maisha yako.

*Hatua ya sita ni kwamba tunahitaji kufuata imani inayoruhusu uhuru.*

Haijalishi jinsi wazazi au babu zako walivyokuwa wema, wanaweza wakakupa imani inayozuia njia yako ya mafanikio. Unapaswa kubadili imani hiyo imani na kupata imani ambayo inayofungua mlango wa mafanikio kwako na jamii yako. Haijalishi unalizimishwa kiasi gani kufuata dini yako au imani, kama ipo kinyume na uhuru na kujitawala, unatakiwa kubadilisha dini au imani hiyo au na upate nyingine bora zaidi. Maendeleo kwa watu binafsi, familia, jamii,

siasa, uchumi na maadili kwenye mataifa yaliyoendelea ni kwa sababu ya ujasiri wa wanaume na wanawake ambao wamethubutu kufuata misingi ya imani inayoruhusu uhuru. Si tu wamefanikiwa bali pia wamefungua milango kwa wengine kufanikiwa. Kwa sababu walifuata imani iliyowafundisha kuwa kufanikiwa kwa wengine kutasababisha na wao kufanikiwa. Kwa mara nyingine tena kama unaona imani yako inakufunga, iache tafuta nyingine itakayokupa uhuru.

Nataka nikwambie ukweli kwamba kama unafuata imani inayoheshimu uhuru wako na wengine pia, utaachana na mateso ya utamaduni kandamizi. Ukweli utakuweka huru.

*Hatua ya saba ni kwamba tunapaswa kuwa jasiri.*

Sisi wenyewe tunatakiwa kuchukua hatua kwa ajili ya maendeleo yetu wenyewe. Kama mimi binafsi ninataka maendeleo, natakiwa kuchukua hatua madhubuti kwa mafanikio yangu mwenyewe. Shauku binafsi inaleta nguvu inayoweza kushinda vikwazo. Watu jasiri wanaweza kupata suluhisho wenyewe au kwa wanafamilia wenzao bila kujali vikwazo vingi vinavyowazunguka. Watu jasiri wanaweza wakatoka kwenye kifungo cha imani kandamizi na kutafuta misingi bora. Uwe jasiri .

*Hatua ya nane ni kwamba tunatakiwa kulipa gharama.*

Tunapaswa kulipa gharama ili kupata ufahamu. Tunahitaji kuwekeza muda na pengine hata pesa. Kuna wakati gharama ya kupata ufahamu fulani huwa kubwa kuliko hata mategemeo yetu. tunapaswa kuwa tayari hata kwa hilo pia. Tunapaswa kuwa tayari kupata mashambulio kutoka kwa wale wenye mtazamo finyu na washirikina na madikteta ambao wanatumia ujinga wa wengine kwa manufaa yao wenyewe. Kujitoa huku kote ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe, familia zetu, jamii na dunia.

*Hatua ya tisa ni kwamba tunapaswa kufanya ushindi kuwa lengo binafsi.*

Hakuna kikwazo kisicho na suluhisho. Unapaswa kuwa mshindi kwa kila kikwazo maishani mwako ikiwemo imani yako ambayo inalenga kukuzuia usijue chochote. Njia sahihi ya kushinda vikwazo kiatika maisha ni kujua imani sahihi au njia bora ya maisha na kuifanya yako. Ndiyo! unahitaji kupata imani bora. Binadamu ameumbwa kuweza kutafuta na kupata kilicho bora kwa ajili yake, imani bora ambayo inampa ushindi dhidi ya vikwazo. Ushindi dhidi ya vikwazo vyote utakuwa wako kama ukikusudia kuupata.

*Hatua ya kumi ni kwamba tunahitaji kuamsha jamii zetu.*

Ni jitihada na ufahamu pekee ndivyo vinaweza kuamsha jamii zetu. Katika njia yeyote ile, tunatakiwa kung'ara kama mwanga wa kweli, kuruhusu wengine kujifunza kupitia uzoefu wetu na kung'ara kwa wengine. Kama upo mwenyewe, unapaswa kufanya kazi kwa bidii kuwafanya marafiki ambao pia wanatafuta ukweli na kukua katika ushirika ili na wao waamke na kuwekwa huru. Pia tunapaswa kuimarisha mahusiano yetu na wale wenye lengo moja na sisi mpaka wote tufurahie uhuru.

**Uelewa wetu unategemea maamuzi yetu wenyewe.**

Hakuna anayeweza kutulazimisha na kutufanya tujue vitu kama sisi wenyewe hatujaamua kubadilika. Majeshi yote duniani yangeungana na kutulazimisha kumka kuutafuta kweli, bado tutaendelea kulala kama hatuna shauku halisi ndani yetu. Hata kama yule tunayempanda na mwema sana angekuwa kiongozi wa serikali, bado hawezi kutuongoza kwenye ukweli mpaka tuamue kuvunja viambaza mioyoni mwetu na kutilia maanani. Kuamka na kubadilika ni juu ya kila mmoja wetu binafsi. Tunapaswa kuamua kubadilika. Hebu tuanze na sisi wenyewe tuingie kwenye kwenye

maisha ya ukweli na kufanywa upya. Kujaribu ni kuzuri.

### Hitimisho

Kama unamwanini Mungu unapaswa kujua kuwa Mungu anapenda watu wawe na ufahamu. Mungu ajuaye kila kitu anajua kipi cha kweli na kipi cha uongo na kipi kizuri na kipi kibaya. Kwa sababu hiyo Mungu anataka watu wajue tofauti kati ya ukweli na uongo na kuchagua ukweli.

Mungu mwenyewe ni huru, hivyo anataka kila mtu awe huru. Mungu ni mkamilifu na anataka sisi pia tuishi kiukamilifu. Kwa hiyo imani yeyote inazuia uhuru, ufahamu au maboresho haitoki kwa Mungu.

*Mtu wa kwanza kuwa huru ni wewe.*

Mtu wa kwanza anayetakiwa kuikimbilia imani inayoweka huru na kuwa huru ni wewe. Tafadhali usiseme “hakuna anayetamani kuwa huru kwanini mimi nitamani?” Unahitaji kufuata uhuru na kusema “kama uhuru ni bora, je kuna sababu ya mimi kuukosa?” Hapana, natakiwa kuwa huru. Natakiwa kufuata imani ambayo inathamini uhuru, inafungua mlango wa ufahamu na ukweli kwangu.

*Mabadilika huwa kichocheo cha maendeleo zaidi.*

Mlango wa mabadiliko na mafanikio utakuwa wazi kwa familia zetu na marafiki kama tumeamua kubadilika na kujirekebisha. Kupitia sisi wao pia watakuwa mikono na miguu ya ufahamu na mafanikio kwa wengine. Tukiwa chachu ya mabadiliko na mafanikio kwa watu wanaotuzunguka watatusaidia kufikia malengo yetu. Ndio maana ni muhimu kwetu kufanya kazi kwa bidii ili watu wanaotuzunguka waelewe kuwa uhuru wa kutajfiti, kuandika, kuongea na imani ni haki kwa wote, kutetea haki zao na ikiwezekana kulipa gharama kwa ajili ya haki za wengine. Kila mtoto kwenye jamii zetu anapaswa kujifunza kwanini anatakiwa kujitenga na imani zisizofaa na kufuata imani inayofundisha uhuru, wema na amani.

*Hakutakuwa na nafasi ya utawala wa kidikteta katikia jamii huru.*

Jamii ambayo imepata ufahamu na uhuru kamwe haiwezi kuwa na nafasi ya udikteta. Ndiyo maana madikteta wote huzuia watu wasiwe na ufahamu linganifu ili waendelee kutawala. Udikteta na ufahamu haviendi pamoja.

Ufahamu wa ukweli unafanya maisha na mahusiano kuwa na tija na mazuri kwenye familia na jamii.

**Wakati wa kutafakari 1**

1. Toa sababu za kwanini watu wanazuiwa kupata ufahamu wao wenyewe na imani zingine.
2. Je kuna njia ambazo tunaweza kutumia kuhimiza watu kuwa wazi na kulinganisha imani zao na za wengine ili kuchagua bora? Ni zipi hizo?
3. Je kukosa kwetu ufahamu kuhusu kweli kunamfanya Mungu asiwe na maana katika maisha yetu? kivipi?
4. Ni zipi faida za ufahamu ?
5. Kama ufahamu ni mzuri, je kuna sababu yeyote kwetu kuupuuza?

# Haja ya kuboreshwa Utamaduni wetu.

## Kwanini? Kivipi?

**Utamaduni ni nini na wapi panahitaji kuboreshwa?**

Utamaduni unajumuisha imani, maadili, lugha, mila, misemo, tabia, muziki; kwa kifupi, ndiyo utambulisho wa taifa.

Kwa hiyo unaona ni vipengere vya utamaduni vinavyoweza kufanya uwe mbaya au mzuri. Kwa sababu hiyo hata uboreshaji wa utamaduni unapaswa kufanywa kwenye vipengere ili kufanya utamaduni bora. Kuwa na utamaduni mzuri haimaanishi ni kuachana na utamaduni wako wa sasa bali ni kuuboresha au kabadilisha vipengere vyenye mapungufu. Kwa sababu hii, unatakiwa kufungua moyo wako kwenye misingi mizuri ya maisha, hata kama inatoka kwa watu usio wapenda. Kwa sababu misingi mizuri daima ni mizuri, haijalishi inatoka wapi, na ipo kwa ajili ya kila mtu. Tufurahie kubadilisha sehemu nyeusi za tamaduni zetu kwa kupokea misingi mizuri na hivyo kuufanya utamaduni wetu kuwa mzuri zaidi.

Je umetafakari kwa kina kuhusu utamaduni wako? Niruhusu nikushirikishe matatizo machache

yanayochafua vipengere vya tamaduni. Yamkini utamaduni wako umechafuka na unahitaji marekebisho.

**Utatuzi wa matatizo katika tamaduni iliyo haribika.**

Je suala la kuingilia maisha ya wengine na kupuuza uhuru sio jambo la kawaida kwenye tamaduni za kiislamu? Kutokana na asili ya ubabe kwenye Uislamu wote waliokuzidi umri wanaweza kuingilia maisha yako hata kama umekuwa mtu mzima na una familia. Serikali na wakati mwingine hata watu binafsi hawaheshimu uhuru wako. Familia yako na ndugu zako pia wanakuwa wakali kwako kama haufikiri au kuamini kama wao.

Kuingiliwa huko kusikofaa kila wakati hupelekea woga baina ya ndugu katika familia, na jamiii na huwa kizuizi cha maboresho kwa njia yeyote ile. Kwanini? Kwasababu watu huogopa kuleta mabadiliko katika maisha yao ili kuwafurahisha viongozi na ndugu zao na hivyo kuepusha migongano zaidi. Jamii hubaki bila uhuru wa kuvikubali vitu vizuri kwa sababu ya mahusiano ya kimabavu.

## Kutoheshimu upinzani.

Maisha kwenye utamaduni usio vumilia kukosolewa huwa magumu sana. Watu wengi hawaheshimu raia wenzao wenye mawazo huru kwa sababu wanawaogopa viongozi wao. Wanategemewa kukaa mbali na wakosoaji na wapinzani wao. Mwitikio unaweza kuwa mbaya zaidi kama wakosoaji ni wanawake au wasichana. Ni hatari kukosoa viongozi wa kisiasa au mtu mwenye hadhi ya juu.

Katika jamii kama hii isiyovumilia, watu wataamua kubaki kimya dhidi ya ukiukwaji wa haki na kuendelea kuangukia kwenye uonevu zaidi. Ukiukwaji wa haki pia utapelekea kuminywa kwa ubunifu, kuongezeka kwa tofauti, kutovumilia, uadui na kuziba njia ya maendeleo.

Niambie ukweli, je jamii yako inahangaika kwenye giza la namna hii? Kama ndiyo, unapaswa kutafuta nuru nje ya utamaduni wako na kutimiza wajibu wa kuuboresha utamaduni wako.

## Hofu kwa walio ndani.

Muda mwingi tumeona Waislamu wakiwaza na kufanya mambo kwa siri. Hawataki ndugu zao na Waislamu wenzao kujua uamuzi wao. Wanaamini sana watu wa nje wanaoheshimu uhuru wa kuchagua, lakini

hawawaamini watu wao wa karibu kwani hakuna heshima ya uhuru miongoni mwao.

Hofu hii ni matokeo ya kuingiliwa kusiko kwa kawaida miongoni mwa Waislamu ambako kumepelekea kutoaminiana na kutengana. Hakuna jamii inayoweza kuendelea katikati ya hofu, kutoaminiana na matengano.

Je jamii yako imetengeneza hofu kama hii? Unatakiwa kujinasua kutoka kwenye hofu hiyo na kutoruhusu mtu kukandamiza utu wako tena. Lengo la mafundisho yangu ni kukusaidia kutunza ubinadamu wako na kuwafundisha wengine kufanya hivyo pia.

**Kufunika madhaifu ya utamaduni.**

Wengine huwa wanahalalisha au kufunika mapungufu au kukana kwamba hayapo. Kwa mfano, kuna ruhusa katika dini ya Kiislamu ya wanaume kuwapiga wake zao, lakini Waislamu hukataa kuiweka wazi kwa watu wengine. Au Uislamu hutoa ruhusa ya kudanganya kwenye baadhi ya mazingira lakini Waislamu hukataa wakiulizwa na watu wasio Waislamu.

Mila hizi kandamizi zitaendelea kuwepo kwenye utamaduni na kusababisha hasara mpaka zitakapo wekwa wazi na kukosolewa. Njia nzuri ya kuboresha

utamaduni wako ni kuibua mapungufu yake ili wengine wayaone na kutoa mapendekezo bora.

**Kukuza au kupindisha ukweli.**

Je utamaduni wako hutilia mkazo kwenye kuonesha mambo yasiyo halisi, kuonesha madhaifu kama ushindi au kukuza ushindi mdogo? Je umejaribu kijitenga na giza hilo? Kama siyo, basi unatakiwa kuikubali misingi mizuri kutoka utamaduni mwingine na kufanya upya utamaduni wako katika maeneo hayo na kujitoa wewe na familia yako toka kwenye giza hilo.

Ulifundishwa tangu utotoni kuwa unatakiwa kuonesha mambo yako mazuri tu na kuficha mabaya. Mafundisho haya hayana ukweli. Ukificha giza ndani yako, maisha yako yote yataathirika na giza hilo na hautakuwa na uwezo wa kupata furaha ya kudumu bali ya kuigiza tu. Unahitajika kwa nguvu zote kutibu ulimi wako na utamaduni wako toka kwenye giza hilo.

**Upendeleo**

Watu wengine wana upendeleo kitu ambacho siyo kizuri kwa jamii. Upendeleo hufungua mlango wa kutokufuata sheria, matengano, na vurugu. Upendeleo pia unaweza kuharibu sana utamaduni, mfano mtu asiyekuwa na uzoefu kupandishwa cheo zaidi ya mtu mwenye sifa husika. Upendeleo hufungua milango kwa

watu wasiostahili kupata uongozi, na hivyo kudidimiza zaidi utamaduni.

Kama imani yako inaruhusu upendeleo, unatakiwa kufuata imani inayokataa giza hilo ili kufungua mlango wa maisha bora.

**Kuendeleza Uvivu.**

Katika imani nyingine, watu hufundishwa kutegemea utajiri wa watu wangine badala ya kufanya kazi kwa bidii ili kujitegemea. Moja ya imani hizo ni Uislamu unaofundisha wafuasi wake kupora mali za watu wengine wasio Waislamu. Ukiwa na imani hiyo isiyo heshimu wengine, hauwezi kuwa na utamaduni mzuri. Unatakiwa kuubadilisha ili kupata imani inayothamini juhudi ya kazi ya watu ikiwemo wasio wa imani yako, na kuheshimu haki za watu wote. Utamaduni au imani nzuri lazima ifundishe watu wake kuwajibika na kupinga uvivu, ili wasimame kwa miguu yao na kuwa raia wazalishaji badala ya kuchukua tu mali za watu wengine.

**Utaifa uliopitiliza.**

Mtaifa aliyepitiliza ni mtu anayesema; “Watu wetu ni bora kuliko wengine. Hatutakiwi kubadilika. Tutawakaribisha wale tu wanaofikiri kama sisi. Wageni ni wageni. Tunapaswa kuwatawala wengine”

Uzalendo huu hauna afya. Uzalendo wenye afya ni ule unaothamini na kuendeleza si tu utamaduni wake lakini pia unatafakari na kufungua kwa manufaa ya wengine. Uzalendo unaohamasisha ubaguzi unatengeneza utamaduni ulioganda.

**Mashaka ndani ya utamaduni.**

Kuna vitu vingi ambavyo havipo wazi ndani ya tamaduni nyingine. Chanzo kikubwa cha sintofaumu hiyo ni imani inayotawala ambayo huleta mashaka ya mambo yajayo badala ya uhakika. Mashaka hayo huenea kwenye kila nyanja ya maisha, ikiwemo mahusiano ya kijamii na kisiasa, na inaweza kuleta kuto kuaminiana miongoni mwa watu.

Mashaka ni upofu wa kiroho ambao hupelekea giza katika nyanja nyingine kama hautatibiwa. Katika utamaduni wenye mashaka mengi, ujasiri wa kuvunja mila potofu za mababu hupungua. Ukosolewaji hauvumiliki, na kueleza shauku ya kitu kipya inaweza kukugharimu. Kila mtu analazimishwa kuisifia imani na utawala huku akikaa kimya kuhusu matendo na maagizo yao mabaya. Kiujumla, watu wanalazimishwa kukubali kila kitu wanachoelekezwa na viongozi.

Nchi za Kiislamu ni mfano mzuri wa sintofahamu na mashaka ndani ya utamaduni, ambapo hujidhihirisha kwenye makundi, utawala, viongozi na washirika

hawaaminiani. Wakati mwingine mtu anaweza kuteswa, kufungwa au hata kuuawa na familia au kikundi kwa sababu ya dini au siasa.

Ugomvi kati ya Wasunni na Shia ulianza miaka 1400 iliyopita miongoni mwa warithi wa Mtume Muhammad. Hii ilitokea baada ya kifo chake na bado unaendelea mpaka leo.

Unaona jinsi sintofahamu katika imani inavyopelekea mahusiano ya mashaka, njia zisizoaminika na utamaduni wa kibinafsi. Kuna usemi wa watu wa Iran unaosema: 'hata mbwa huwa hamtambui bwana wake' wakimaanisha mkanganganyiko huo. Ni vigumu kuondoa ujasiri wa mbwa kwa bwana wake. Lakini kama huyo bwana haaminiki, hiyo ndio humfanya mbwa kupotea na kuanza kuzurura.

Kwenye utamaduni wenye sintofahamu kuaminiana ni kwa nadra sana na kuna masharti mengi sana. Umoja sio wa kiundani bali wa kimaigizo. Hata kama watu wanatamani kuwa na mahusiano mazuri, kuna vizuizi vingi visivyoonekana vinavyozuia umoja huo kwa sababu ya sintofahamu katika jamii. Kwasababu ya kutokuwa na umoja, haki za watu wengine sio kipaumbele na hupuuzwa kirahisi sana. Urafiki ni wa kitambo tu na unaweza kugeuka kuwa uadui kwa sababu ya kitu chochote, kiwe kidogo au kikubwa.

**Je utamaduni wako una mikanganyiko hiyo tajwa hapo juu?**

Kama Ndiyo! Basi fanya sehemu yako. Kivipi?

*Unatakiwa uanze na kwako mwenyewe*

Jitenge na vitu vinavyo haribu maisha na utamaduni wako. Kama imani au dini yako imeleta athari mbaya kwenye utamaduni wako, ifanyie kazi; jiulize kwanini na tafuta imani inayoruhusu uhuru, amani na kuheshimu watu wote, iwe marafiki au wageni. Kuchagua kuto kuchukua hatua kunaweza kuwa mwiba kwa jamii.

*Mathara ya vitu vibaya mara nyingi ni hatari.*

Hakuna hekima duniani inayosema vitu vibaya vina faida. Vitu hatari kwenye utamaduni vina madhara. Wewe unawajibu binafsi na kijamii kukaa mbali navyo. Chukua vitu vizuri toka kwenye tamaduni nyingine na vitendee kazi na kuboresha utamaduni wako. Maisha yako mapya yatakuwa nuru kwa utamaduni na jamii yako. Watu wengi watajifunza kwako, kufanya hivyo hivyo na kuleta mabadiliko chanya kwenye utamaduni.

*Kamwe, kamwe usiache wajibu wako wa kuchangia vitu vizuri katika utamaduni wako*

Ngoja nikupe mfano wa utengano ili uone jinsi inavyoweza kuwa hatari kwako na kwa watu wengine.

Mchungaji wa Kijerumani, Martin Niemöller[1], anaeleza jinsi kutojali kulivyo athiri maisha yake na ya wengine. Alisema wakati Hitler akiua Wakomunisti, alijisemea mwenyewe kuwa yeye siyo wa mlengo wa Kikomunisti na hakuwa akihitajika kuwatetea au kuwalinda. Alikuwa na kisingizio hichohicho wakati Hitler akiua Wayahudi na wengine. Baada ya Hitler kumaliza kuua watu wengine, alianza pia kuua wapinzani ndani ya Ujerumani. Kipindi hicho Martin mwenyewe akafungwa pia. Anasema hakuna watu wenye ujasiri waliokuwa wamebaki kumtetea dhidi ya Hitler. Kama mwanzoni yeye na watu wengine wangetetea maisha ya watu waliokuwa wakichinjwa, sasa kungekuwa na watu wengi kwenye jamii wa kumtetea yeye alivyokuwa gerezani.

Kutojali ni upofu wa kiutamaduni ambao hutoa nafasi kwa mabaya kustawi mpaka jamii nzima ikaathirika. Ndio maana unatakiwa kuuboresha utamaduni wako. Utamaduni sio kitu kisicho badilika bali hubadilika na kuboreshwa. Tunaweza kuboresha utamaduni wetu

[1]https://en.wikipedia.org/wiki/First_they_came_...

kwa kukubali vitu vinavyo kataa giza. Umebeba mabegani wajibu wa kuboresha utamaduni wako na wa taifa kwa ujumla.

**Wakati wa kutafakari 2**

1. Katika dunia ya imani mbali mbali na misingi inayokinzana, je njia gani bora ya kuwa na amani na umoja?
2. Kwanini uboreshwaji wa tamaduni zetu ni muhimu?
3. Ni wapi tunaanzia kwenye kuboresha utamaduni wetu?
4. Je kuna uhusiano wowote kati ya ujasiri, kuboresha utamaduni na maendeleo?
5. Je una wajibu wa kuboresha utamaduni wako?

## Mifano ya badiliko binafsi kutokana na maisha ya Daniel

Nina ushuhuda mzuri wa kukuambia. Nimeanza mfululizo wa mazungumzo yangu kwa kukwambia ufahamu ni jambo muhimu kwa ajili ya uhuru. Tunahitaji ufahamu binafsi kwenye kila kitu, ikiwemo imani yako, sio tu kujinda dhidi ya imani potofu, bali ni muhimu katika kufikia malengo ya maisha yetu kwa misingi mizuri. Nimekwambia pia mabegani mwetu tumebeba wajibu wa kuboresha utamaduni wetu kama tuna shauku ya kupata uhuru, kuwa wabunifu na kuboresha mahusiano yetu katika nyumba na jamii zetu.

Itakuwa ni unafiki na uongo kama mimi mwenyewe sijayapitia mabadiliko, lakini nawataka wengine wakubali mabadiliko. Kwa sababu hii, nimechagua kuongelea mabadiliko yangu binafsi katika maisha yangu ili uelewe kuwa mazungumzo yangu ni tafakari ya mabadiliko mazuri yaliyotokea kwenye maisha yangu. Nina ushuhuda wa kweli wa kukuambia. Nimebadilika, nimefanywa upya kwenye akili na moyo na nimebarikiwa na badiliko la maisha tele. Natamani upate uzito wa hoja zangu,  chunguza upya huo na ubarikiwe pia.

Yesu amenifundisha kuwa kama mimi mwenyewe sijabadilishwa kwanza, nisitegemee watu wengine kubadilika. Kabla sijawataka wengine kuangalia vitu vizuri, wanatakiwa kuniangalia mimi kwanza. Kama mahusiano yangu ya amani, upole na upendo hayaelezi jinsi nilivyo, kama uvumilivu na msamaha yatakuwa maneno tu kwangu bila kuwa na nafasi kwenye maisha yangu, kama haki ni nzuri tu kwa wengine kuifuata, basi ushuhuda wangu wote, hoja na ushauri wangu utakuwa ni bure na usio na mashiko.

Nililelewa katika mazingira yaliyo thamini unafiki zaidi kuliko ukweli. Watu walitarajia wengine tu kubadilika lakini sio wao. Kwa hiyo nilikuwa nafanya vitu ambavyo vingenichukiza sana kama watu wengine wangenifanyia mimi. Mitizamo hiyo ni viashiria vya maisha ya ubinafsi yasiyo thamini haki za wengine. Yesu Kristo hufundisha kuwa kama maisha ya wengine hayana thamani kwako, kama hauumii wengine wakiwa kwenye maamivu, mazungumo na mafundisho yako yatakuwa hayana maana kwao.

Kazi na uongozi wa Yesu Kristo katika maisha yangu ni kuchuja maneno na mitizamo kwa kutumia chujio la dhamiri yangu na kuhifadhi yale yanayo boresha utambulisho wangu, lakini kutupa vile vinavyonifunga kwenye upuuzi, ujinga, dharau, ubaguzi, chuki na vita.

Siku moja niliona tangazo kwenye runinga lililokuwa likikataza wananchi kutupa taka mtaani ili kuweka mji na mzingira safi. Hapo ndipo watu wangefurahia unadhifu wa jiji. Kwenye tangazo hilo kuna msichana mmoja aliyekuwa ameegesha gari lake mtaani, akaanza kumenya machenza, na kutupa maganda mtaani. Mwanaume mmoja aliyekuwa anapita akaja nyuma ya gari na kuokota maganda yote na kuyarusha ndani ya gari la yule dada. Yule dada alimkasirikia sana kwa kuchafua gari yake. Jibu la yule mwanaume ni kwamba amemfanyia kitu kile kile ambacho yule dada amewafanyia wengine na kwamba yule dada hakuwa na haki ya kuchukia kama kitendo chake cha mwanzo kilikuwa kizuri.

Tangazo lile lilikuwa ni zuri na la kuelimisha. Lilionesha jinsi ambavyo yule dada hakutumia dhamiri yake kuona tatizo kubwa la mtizamo wake, kuchafua mji wenye mamilioni ya watu, lakini alikasirika haraka alipochafuliwa gari yake. Alihitaji mtu wa kumwamsha na kumrejesha kwenye dhamiri yake na kuona tatizo kubwa la ubinafsi alilokuwa nalo na hivyo kutafuta njia sahihi ya kuwa na amani na watu wengine.

Dhamiri ni moja ya baraka kubwa tulizopewa wanadamu ndani yetu ili kutufanya tufikiri, tupime vitu vinavyotuzunguka na kusimamia kilicho bora. Ni dhahiri kuwa kama kusingekuwa na dhamiri ndani

yetu, nisingekuwa na mazungumzo haya na wewe. Kwasababu ingekuwa ni vigumu kwetu kuelewana bila dhamiri. Kwa bahati nzuri, tunayo dhamiri na kwasababu hiyo ninaongea na wewe kwa moyo wote, kukwambia ushuhuda wangu na kukushirikisha moyo na ufahamu kwa matumaini ya kuibua ufunguo wa kupata kitu kipya.

Nimejifunza toka kwenye Injili ya Yesu Kristo kuwa ninatakiwa kutegemea dhamiri yangu na kuwahimiza wengine kufanya vivyo vivyo, la sivyo tunakuwa kama vizuizi dhidi ya ukweli. Katika 2Worintho 4:2 Injili inasema: "Tumekataa njia za siri na za aibu. Hatutumii njia za udanganyifu, wala hatupotoshi neno la Mungu. Badala yake, tunaeleza neno la kweli wazi wazi na kujitambulisha kuwa wa kweli kwa dhamiri ya kila mtu mbele ya Mungu".

Injili ni thabiti. Ukweli hauhitaji udanganyifu wala ujanja ujanja. Ukweli huzungumza na akili, mioyo na dhamiri za watu na unaweza kuthibitisha ukweli wake. Ukweli hautumii udanganyifu na uongo kama daraja la kuingia kwenye maisha ya watu.

Kulingana na hekima hii kubwa ya Yesu Kristo, ninaamini kuwa dhamiri yako pia inaweza kupima vitu na kugundua kama ni vya kweli au la. Moyo na akili yako vinaweza kufuata vitu visivyo kweli lakini dhamiri

yako haiwezi. Kwa sababu hii, nataka kuleta ushuhuda wangu, uzoefu, uelewa na ufahamu kwenye dhamiri yako. Ni mategemeo na maombi yangu kuwa utaruhusu dhamiri yako kusema na kukuongoza kwenye maamuzi sahihi.

Mabadiliko katika maisha yangu yalianzia kwenye mizizi hadi matawi. Nimejifunza hekima ya ajabu sana toka kwenye injili ya Yesu Kristo. Inasema katika Warumi 11:16: "kama shina ni takatifu, matawi nayo yatakuwa takatifu". Kila kitu kwenye maisha yetu ya kimwili au kiroho hutegemea mzizi tulionao. Maisha yetu ni matokeo ya msingi au mzizi ambao yamejengwa juu yake. Kama msingi ni mzuri, basi maisha yetu yatakuwa mazuri pia. Kinyume na hapo hatutakuwa na maisha mazuri.

Kwa hiyo, ni muhimu kwetu kuchagua msingi na shina la kweli ili tujengwe na kuishi juu yake na tuishi kwa virutubisho vyake vya kweli. Ukweli ni kwamba hatuwezi kupata msingi au mzizi wa kweli mpaka tuwe na imani ya kweli. Imani ya kweli tu ndio hutoa mzizi wa kweli.

Msingi ni Mungu au kiongozi mwanzilishi wa imani yako. Ndio maana nilitakiwa kumtafuta Mungu au kiongozi wa kweli na kujijenga kwenye misingi yake. Mungu au kiongozi atakaye heshimu uhuru wangu wa kuchagua na kunifundisha kuheshimu uhuru wa

wengine, familia au watu wa nje. Kiongozi huyo ni Mungu ambae Yesu alimfunua kwangu. Sio tu ana heshimu uhuru wa watu wengine bali anatamani kuwa na mahusiano na watu ili kuwafunulia vitu vyote vizuri. Kinyume na mungu wa Uislamu, Yeye hajifichi kwa watu wenye shauku ya kumpata. Ametuumba ili tuwe na mahusiano binafsi na yeye.

Je si kitu kizuri na cha ajabu kuwa na mahusiano na Mungu, ambaye ndiye amekupa maisha na ni chanzo cha kila kitu kizuri? Kwa kweli ni jambo jema sana. Ndio maana nina ushuhuda mzuri wa kukwambia wewe na ulimwengu. Kukwambia nini kilitokea na kwanini nina mahusiano na Mungu.

Utaona natumia maneno “nini na kwanini?” nayapenda sana haya maneno “kwanini, nini na kivipi?” nimejifunza kwa Yesu kuwa maneno haya ni muhimu sana katika maisha. Maneno haya hutuweka huru na uongo, hofu na utii bila kufikiria, lakini hujenga ukweli, ujasiri na maamuzi ya hiari. Ndani ya Uislamu hauruhusiwi kutumia maneno haya “kwanini, nini na kivipi?” Katika Koran ni marufuku kuhoji maneno ya Muhammad na mungu wake. Pia ni hatari sana kumkosoa kiongozi wa kiislamu aliyeshika sana misingi ya Uislamu. Matokeo yake utakosa uhuru daima ukiendelea kuwa mwislamu.

Lakini Mungu wa biblia anatutaka tuwajibike na kupima kabla ya kutendea kazi unabii au maelekezo. Nisingemfuata Yesu kama asingetoa kibali cha kutumia maneno “kwanini, nini na kivipi” ili kuelewa kama njia yake ni kweli au la. Uhuru ni hatua ya kwanza katika kumfuata Kristo. Ndio maana Yesu huheshimu hata haki za maadui zake pia.

Kwahiyo, namfuata Mungu aliyeniumba nikiwa na uhuru wa kuchagua. Uhuru wangu ni kitu cha muhimu sana kwa Mungu. Hakuna mtu mwenye haki ya kulazimisha imani yake kwangu. Je hili sio ya nzuri? Hivyo nilimwomba Yesu kunijenga katika mzizi wake unaonihakikishia uhuru katika nyanja zote za maisha, kiroho na kidunia. Katika mzizi wake ninawezeshwa na jiandaa kuwa na mahusiano ya haki, wema, upendo na amani na watu wa kila taifa, lugha, jamii na rangi. Sina adui na mwanadamu yeyote duniani. Adui yangu ni shetani pekee ambaye yupo kinyume na uhuru wangu wa kuchagua na hutaka kuniweka kwenye giza la kupuuza na ujinga.

Je unaona jinsi Mungu wa kweli au msingi, kanuni au mizizi yake huathiri kila nyanja ya maisha yako na kukuandaa kufurahia maisha yako na kuwa nuru kwa wengine? Nuru hii ipo ndani yako na kamwe haiwezi kuruhusu wakala yeyote wa giza kujenga kiota ndani

yako ili kuchafua maisha yako au mahusiano yako na watu wengine.

Sasa ninamfuata huyu Mungu. Yesu amenijenga kwenye msingi ulionipa utambulisho mpya na moyo mpya, mtizamo mpya wenye misingi mipya ya kisiasa na kijamii ili niweze kuwajali watu wote, pamoja na maadui zangu. Yesu amenidhihirishia kuwa maamuzi mazuri huhitaji ufahamu wa kina toka kwenye mizizi wa jambo mpaka matawi. Sisi sote tunahitaji kufanya maamuzi mazuri kama tunataka kuwa na maisha mazuri. Nilimsikiliza ili kufanya maamuzi sahihi. Nilifuata mizizi ya kweli toka kwa Kristo, na baadaye kila tawi katika maisha yangu likawa la faraja na la kushangaza. Faraja ya kwanza niliyopata ni uhakika wa maisha baada ya maisha haya. Niligundua kuwa kama mtu amejengwa katika mzizi wa Mungu, atakuwa kwenye mzizi huo daima kwa kuwa mzizi huo ni wa milele. Sasa nina uhakika kuwa mimi ni mali ya Mungu asilimia mia moja na maisha yangu yote ya hapa duniani na milele nitakuwa pamoja nae. Sitakiwi kuhofu juu ya jahannamu kwani nimejengwa katika mzizi wa Mungu. Je, ujasiri huu sio wa ajabu na faraja? Ni kweli kabisa.

Kama ilivyo kwa waislamu wengine, kabla ya kukutana na Yesu nilikuwa na mashaka ya mustakabali wa maisha yangu ya baadaye. Nilitamani kushinda hofu

iliyoachwa ndani yangu na Uislamu kuhusu maisha baada ya kifo. Qur'ani inasema hakuna ajuae mustakabali wake, na Muhammad pia alisema mara nyingi kuwa hana uhakika na hatima yake. Hii ilinipa wasiswasi. Niliambiwa kufanya kila kitu kizuri kwa mungu wangu katika Uislamu, kufuata nyayo za Muhammad, lakini bila kujua hatima yangu. Lakini kwa kusoma vitabu vya Kikristo niligundua "kama Mungu ni mwenye huruma, anatakiwa kudhihirisha huruma zake katika maisha yangu hapa duniani. Na amefanya hivyo kwa kunipa uhakika kuwa mimi ni mali yake sasa na nitakuwa naye daima."

Huruma kubwa ninayotegemea kutoka kwa Mungu wangu ni kuniokoa toka kwenye mashaka. Uhakika wa kiroho ni muhimu kuliko vitu vyote alivyonipa. Nahitaji wokovu sasa. Natakiwa kushinda mashaka ya kiroho na kuwa huru. Mungu wa kweli mwenye huruma huwa hataki watu kuweka tumaini kwake kwa hatima isiyojulikana. Kiukweli, lengo kubwa la Mungu ni kuweka watu huru dhidi ya mashaka kuhusu mustakali wake na kuwapa tumaini.

Hata katika maisha yetu iko hivyo. Hatumwamini mtu mpaka amethibitisha kuwa mwaminifu.Hapa ndipo tunaona upungufu wa Qur'ani ukilinganisha na injili ya Yesu Kristo.

Injili inafundisha kuwa kama ukimfuata Yesu Kristo utaokoka sasa na milele. Lakini Kuran inafundisha kuwa kama ukimfuata Muhammad, hautaokoka sasa, na hauna uhakika kama utaokoka baada ya kifo au la. Kwa hiyo kwa kumfuata Yesu, niliweza kupata huruma za Mungu kwenye maisha hapa duniani, na kuokoka na kuwa na uhakika wa uzima wa milele.

Kitu cha pili cha kushangaza nilichokipata kwenye msingi wa Yesu Kristo ni kwamba mimi ni mwana wa nuru, upendo, fadhili, haki, utakatifu, na amani. Huu ni utambulisho wangu na wote wanaomfuata Kristo. Kama Mungu ni nuru, upendo, haki, mtakatifu na mpenda amani, mimi pia nimevibeba hivyo vyote kwani nimejengwa kwenye msingi wake. Sasa ninazijua hizi nyenzo na ninajua namna ya kuchukuliana na marafiki, wapinzani na maadui. Mimi ni nuru na ninatakiwa kuwa nuru kwa marafiki, wapinzani na maadui, mwenye fadhili na kepuka kuwanyima haki wengine kwa kisingizio chochote kile. Natakiwa kuutoa moyo wangu kwao kwa upendo na kuwahimiza kwa pamoja kutafuta njia sahihi ili kuwa na mahusiano ya kudumu.

Je sio jambo zuri kuamini kuwa hata adui yako mkubwa anaweza kuwa rafiki wa karibu kama ukiwaendea kwa hekima yenye upendo na kukubaliana kutafuta njia sahihi ya kujenga mahusiano ya kudumu?

Ni ajabu sana. Mimi mwenyewe nimepitia vitu hivi katika mahusiano yangu na baadhi ya watu ambao hawakuipenda imani yangu ndani ya Kristo. Ngoja nikupe mifano kadhaa.

Siku moja mtu mmoja alinambia hataki kusikia kitu chochote toka kwa wakristo kwani ni upuuzi kwake. Nilimuuliza kama kweli anaamini kuwa Ukristo ni upuuzi, akasema ndio. Nikamwambia, "nahitaji msaada wako, nimeubeba moyoni mwangu na kiukweli sitaki kubeba uchafu na upuuzi kwenye moyo wangu. Je unaweza" akaniuliza "wapi unataka nikusaidie?". Nikamwambia Yesu anasema "mpende jirani yako kama unavyojipenda, wapende adui zako na uwabariki, na mpende mwenza wake kama mwili wako", anatuambia kuwa nyenzo nzuri za kujenga urafiki wa kudumu ni upendo na upole. "Kati ya hivi kipi ni upuuzi" akasema hivi ni vizuri kabisa. Nikamwambia tena, Yesu anasema "mkubwa kwenu lazima awe mtumishi wa wote" Yesu anajaribu kusema kuwa ni viongozi wanyenyekevu ndio wanaweza kuwaongoza watu katika haki na amani. Madikteta hawawezi kuleta amani na haki. Je kuna upuuzi gani kwenye hili? Akasema hajawahi kujua kuwa vitu hivyo vipo kwenye Injili. Akaniomba msamaha na kukubali kusoma Injili.

Wakati mwingine imamu wa msikiti alianza kunishambulia kuwa nilikuwa nafunua baadhi ya

vifungu vya Qur'ani kwa watu. Nikamwambia. "ndugu, hauamini kuwa dini yako ni ya mwisho na ni kamilifu? Kwanini wafuasi wa dini hutumia nguvu kama ni ya kamilifu na ya mwisho kwa hiyo ina hekima sahihi kwa majadiliano ya amani na watu wengine? Unauita Ukristo kuwa haujakamilika, kama ni hivyo, natakiwa kutumia nguvu kama dini yangu haijakamilika, lakini cha kushangaza wewe ndo unatumia nguvu na mimi natumia upole tu."

Dhamiri yake iliguswa na akagundua kuwa nilikuwa sahihi kumtaka tuongee kwa amani. Mazungumzo yangu mafupi yenye amani yalikuwa utangulizi mzuri wa miezi 6 ya mazungumzo ya kirafiki. Mwisho wa siku alitoa maisha yake kwa Yesu. Imam wa msikiti akaacha Uislamu na kuwa mfuasi wa Yesu.

Je jambo jema kuwa sijibu vurugu kwa vurugu? Nimetokea kwenye utamaduni wa vurugu. Nilikuwa kiongozi wa Kiislamu mwenye msimamo, mwanasiasa na msomi. Nilijifunza kuwa vurugu ilikuwa ndiyo jibu pekee kwa mtu anayesema "hapana" kwa Uislamu. Lakini sasa hivi chini ya uongozi wa Kristo ninakabiliana na wapinzani wangu kwa upendo, fadhila na hoja, ili kugusa dhamiri zao ili wapate fursa ya kutafakari kwa kina na kutafuta kweli na kuwa marafiki zangu. Safari yangu toka kwenye Uislamu

hadi Ukristo imekuwa baraka kwa wote, pamoja na wapinzani wangu.

Huu ni ushuhuda wa maisha yangu. Nimeguswa na Yesu Kristo, nimefanywa upya na kupata tumaini la milele. Mimi ni kiumbe kipya sasa, nipo huru kutumia akili, moyo na dhamiri yangu ili kuwaleta watu kwenye uhuru wa kweli. Asante sana kwa kusikiliza ushuhuda wangu.

## Wakati wa kutafakari ya 3

1. Je ni sawa nisipojifunza vitu vizuri na kutegemea wengine wawe wazuri?
2. Je ni kwanini tunahitaji akili, mioyo na dhamiri zetu zifanye kazi?
3. Je ni kiasi gani imani yetu inaathiri maisha yetu ya kiroho na kijamii? Kama athari ni hasi je tutafute imani mbadala?
4. Kama unamwamini Mungu, ni jambo jema kumjua na kupokea uhakika wa milele?
5. Kwanini Daniel aliweka tumaini lake kwa Yesu?
6. Kwa njia ipi au zipi unaweza ukajifananisha na Daniel?

## Mungu - Je Mungu yupo?

Mijadala ya kifalsafa kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu imeanzia kwenye historia. Ushahidi wa kihistoria unaturudisha kwenye karne ya tano kabla ya Kristo (KK) kabla akina Socrate, ambao kwa mara ya kwanza walieleza uumbaji bila kumhusisha Mungu. Mtu mashuhuri katika kipindi na harakati hizo alikuwa ni Thales.

Falsafa ya kutoamini uwepo wa Mungu ilipata nguvu sana baada ya Ukomunisti na harakati za Darwin. Baadaye, ilichukua msimamo mkali wa kisiasa dhidi ya kuenea kwa falsafa ya Mungu na uumbaji.

Wale wasioamini uwepo wa Mungu husema: Mungu hayupo kama hawezi kuonekana au kuguswa. Hatuna uhakika kama Mungu yupo au hayupo kwa sababu sayansi bado haijathibitisha uwepo wake. Kwa hiyo wanadhani ulimwengu ulitokea kwa nasibu na kwa ajali tu na haiwezekani ukawa na muumbaji. Lakini wale wanaamini kuwa Mungu yupo wanasema: Kwa kuwa kila kitu kilichopo kina mwanzilishi na muumbaji, uwepo wa ulimwengu ni ishara kuwa ina muumbaji wake.

**Ushahidi dhidi ya falsafa ya uwepo wa dunia kwa nasibu.**

*Ushahidi wa kwanza ni muundo wa kila kitu.*

Kila kitu hapa duniani kina mpangilio na muundo mzuri ambao haiwezekani ikawa ilitokea kwa ajali. Kila wakati tukiona muundo mzuri kwenye kitu ina maanisha kulikuwa na weledi, ufahamu na usimamizi mzuri nyuma ya uundwaji wa kitu hicho. Kama hii ni kweli, basi falsafa ya uwepo wa dunia kwa nasibu sio tu haileti mantiki, bali pia ni kinyume na mantiki ya sayansi.

*Ushahidi wa pili ni namna viungo vya mwili vinavyofanya kazi*

Kila kiungo cha mwili wa mtu au mnyama kimewekwa sehemu yake kwa utashi wa hali ya juu kwa ajili ya kazi na madhumuni maalumu. Weledi huu hauendani na falfasa ya nasibu. Kwa mfano, twiga ana moyo wenye uzito wa kilo 13 (29lb) wenye shinikizo la damu mara mbili zaidi ya moyo wa tembo, ili kuweza kusukuma damu kupita kwenye shingo ndefu mpaka kichwani. Ana mishipa[2] jirani na ubongo inayofanya kazi kama

---

2

https://en.wikipedia.org/wiki/Giraffe#Neck;http://www.africam.com/wildlife/giraffe_drinking.

sponji kwa kufyonza damu taratibu wakati kichwa kimeinama ili kupunguza shinikizo la damu, la sivyo kichwa kingepasuka. Kama shinikizo ni kubwa sana, sponji humtaarifa twiga kuinua kichwa chake kabla madhara hayajatokea.

Je ni rahisi kuelezea weledi huu wa ajabu kwa falsafa ya nasibu? La hasha.

*Ushahidi wa tatu ni maadili ya kibinadamu.*

Maadili katika maisha ya kila siku haiwezekani kuwa yalitokea tu. Kwa mfano, bila uzioefu na miongozo fulani hatuwezi kusema kama kitu hiki ni kizuri na kingine ni kibaya au kitu hiki ni uongo na kingine ni kweli. Lakini kama tunatumia uzoefu na miongozo namna hii basi falsafa ya nasibu haitakuwa na maana. Kwanini? Kwa sababu tumeishi hivyo tangu zamani, na maarifa tuliyopata kwa uzoefu wa nyuma ndiyo yamekuwa mwongozo wa maisha ya sasa. Kwa mtindo huu tunasonga mbele tukiwa waangalifu ili kuepuka vitu hasi na viharibifu.

Kwa hiyo tunaona mifumo ya maisha ni matokeo ya uwezo wetu wa kutathimini na kuamua kiutashi na sio kwamba ilitokea kama ajali ili kutuongoza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa hiyo falsafa ya nasibu ni nadharia tu na haiendani na uhalisia wa maisha ya kawaida.

*Mifumo ya maadili ya kila familia duniani unakinzana na falsafa ya nasibu.*

Katika historia hata wazazi wasiomwamini Mungu walikwepa kuoa watoto wao. Kwa mantiki hiyo hata utaratibu uliokwishawekwa tangu mwanzo unapingana falsafa ya nasibu. Pia, hakuna mtu anayeweza kusema kuwa mtu huyu ni mwenza wangu au mtoto huyu tuliamua kuwa nae; kwa sababu kuchagua na kupanga hakuendani maisha ya nasibu au falsafa.

Kwahiyo unaona kila kitu duniani, ikiwemo sayansi, haikubaliani na falsafa ya kutokea kwa nasibu lakini huonyesha uwepo wa Muumbaji aliyesanifu na kuumba dunia.

Dunia imeumbwa na Mungu. Tunatakiwa kuangalia vitu vilivyotuzunguka ili kuelewa hili.

**Huyu Mungu ni nani?**

Naam, Mungu amefafanuliwa tofauti na dini nyingi. Lakini ni nani anayesema ukweli? Siyo mpango wangu katika kitabu hiki kujadili mitazamo kuhusu Mungu katika dini mbalimbali, lakini nina lengo la kulinganisha maoni ya Waislamu na Wakristo kuhusu mitazamo yao ya Mungu. Je, Uislamu na Ukristo hufafanua Mungu kwa mitazamo tofauti? Hebu tuone kadri tuwezavyo.

**Mungu katika Uislamu na Ukristo.**

*Je Mungu anaweza kuwa na mahusiano na watu kwenye mojawapo kati ya imani hizi?*

Biblia inasema: Mungu ana asili ya kujidhihirisha. Anajenga mahusiano binafsi na alikuwa na mahusiano binafsi na watu wengi kwenye Biblia.[3]

Korani inasema: Mwenyezi Mungu hana asili ya kujidhihirisha na hawezi kuwa na mahusiano binafsi na watu. Hii inafanana na falsafa ya kigiriki: kwenye falsafa ya kigiriki Mungu hana utu na hawezi kujidhihirisha. Sababu iliyofanya waislamu kuazima falsafa ya kigiriki ni kwa sababu sifa za Mwenyezi Mungu zinaendana na falsafa ya kigiriki tu.

Tunasoma kwenye biblia kuwa Mungu huona, husikia na huzungumza moja kwa moja na watu na kujidhihirisha kwa yeyote atakaye mchagua. Lakini Koran inasema kwenye Sura Al An'am (6) aya ya 103

---

[3]Mungu wa kwenye Biblia ni Mungu mwenye utu na wa mahusiano, kwa hiyo hawezi kujificha bali ni Mungu anayeonekana. Ana asili ya kuonekana kama amabavyo alijidhiirisha kwa wengi katika Agano la kale, aliongea maojha kwa moja na manabii wote na alijidhihirisha kama mtu kwenye Agano jipya.kuna mazingira anajificha kutegemeana na jinsi atavyoona inafaa.

kuwa Mwenyezi Mungu huona lakini haonekani, na Sura Ash-shura (42) aya ya 51 inasema Mwenyezi Mungu haongei na mtu yeyote bali huongea nyuma ya pazia. Kwa hiyo Qur'ani inasema Mungu hujificha na kamwe hajidhihirishi, lakini Biblia inasema Mungu hujidhihirisha.

Sasa kabla hatujaanza majadiliano ya kihoja, ngoja nikuulize swali jepesi. Je unatamani kumuona Muumba wako ana kwa ana?

Nimeshangazwa na majibu ya watu wengi kutoka kwenye misingi ya imani tofauti waliosema wangetamani kumuona Muumba wao. Tofauti na mtizamo wa Kiislamu, baadhi ya wanafalsafa, wanatheologia na washairi wa Kiislamu wa Mashariki ya kati pia wanatamani kumwona Mungu ana kwa ana.

Kwa ufupi, nataka nikwambie kuwa kamwe Mungu hatamani kujificha kwako kama unashauku ya kumuona.

**Kwanini Mungu hajifichi?**

*Mungu huonyesha upendo wake wazi wazi.*

Mungu ni Mungu wa upendo, hafichi upendo wake. Huwezi kusema mtu huyu ana upendo mpaka mtu huyo auonyeshe upendo wake kwenye mahusiano.

Mungu naye vivyo hivyo; hudhihirisha upendo wake kwako na kwa viumbe vyake kupitia mahusiano. Matokeo yake, Mungu lazima atengeneze mahusiano kwetu kwanza ndipo adhihirishe upendo wake kwetu. Tangu mwanzo Mungu alipopanga kuumba ulimwengu, pia alijumuisha mpango wa upendo wake. Katika uumbaji, Mungu alijidhihirisha kwa Adamu na Eva, waliweza kumwona Mungu na upendo wake.

Kama mungu wako hataki kijidhihirisha, basi yeye sio mungu wa mahusiano na hana faida katika maisha yako.

*Tunaweza kumfahamu Mungu vizuri kama akijidhihirisha.*

Kila mtu aliyeumbwa na Mungu anatakiwa kumfahamu Muumba wake. Je si vizuri kumfahamu Mungu binafsi bila kuhitaji mtu wa kati? Kumfahamu mtu binafsi bila kutegemea mtu wa kati hujenga urafiki wa karibu. Fikiri kama unataka kujenga familia, je haitakuwa bora kumfahamu wewe mwenyewe mwenzi wa maisha ya baadaye na kuungana nae? Kwa Mungu pia ni sawa. Kama ukitaka kuungana na Mungu, lazima wewe binafsi umfahamu

Neno la Mungu haliwezi kuwa dhahili kwako kama hatumfahamu Mungu binafsi. Kwa upande mwingine, hakuna mtu anayeweza kutufanya tukamjua Mungu

vizuri zaidi ya Mungu mwenyewe. Sasa kwanini Mungu hajifunui kwetu ili tumfahamu kibinafsi? Mungu hajifichi kwetu. Kama imani yako inasema Mungu hawezi kujidhihirisha kwetu na hajitambulishi, imani yao haiwezi kuwa ya kimungu.

Kama mtu hamfahamu Mungu kibinafsi anawezaje kuwa mjumbe wa Mungu? Hapana. Mjumbe wa kweli wa Mungu hutumwa na Mungu mwenyewe. Kama mtu hajamwona, hajasikia sauti wala hamjui Mungu, kwa mantiki ipi mtu huyo anaweza kusema anatoka kwa Mungu? Hakuna mantiki kwenye hili. Mjumbe wa kweli anatakiwa kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na Mungu, aijue sauti yake na kuwa na neno lake, la sivyo hawezi kuwa mkweli kwenye madai ya kusema anatoka kwa Mungu. Na kama hakuna msingi dhabiti kwenye imani, basi udanganyifu, nguvu na upanga vitakuwa ndiyo njia za kufanya ujumbe ukubalike. Kwa hiyo, kama Imani inafundisha kuwa mtume wako hajakutana na Mungu binafsi, basi unatakiwa kutafuta imani nyingine inayoruhusu mahusiano binafsi kati wa Mungu na wajumbe wake.

*Mungu wa upendo anataka kuwaongoza watu yeye m wenyewe.*

Hajawahi kusikia watu wanasema, “Mungu akuongoze”? hii ni kwa sababu watu hutamani kuongozwa na Mungu mwenyewe. Nina uhakika wengi

mtakubaliana na mimi kuwa hakuna wa kufanana na Mungu kwenye haki, uadilifu, utakatifu na fadhila. Nani mwingine anaweza kuongoza watu kama Mungu? Hayupo. Mungu anajua kuwa kama yeye mwenyewe atakuongoza, basi shetani hawezi kusogea karibu nawe. Lakini kama mtume akikuongeza, utakosa kinga dhidi ya ushawishi wa shetani. Kwa sababu hii, Mungu hajifichi, lakini hupenda kujidhihirisha na kukuongoza yeye mwenyewe. Kwahiyo , kama ukimruhusu Mungu akuongoze, itakuwa salama zaidi kwako badala ya kuongozwa na mtu wa kati au Nabii. Matokeo yake ni kwamba kama imani yako haikupi nafasi ya kuwa na mahusiano binafsi na Mungu, na inakulazimisha kumfuata Mtume bila kuhoji, imani hiyo haiwezi kuwa inatoka kwa Mungu.

*Mungu anataka kuleta amani duniani yeye mwenyewe.*

Kama Mungu ni mleta haki na shetani ni mleta dhuruma, je ni nani zaidi ya Mungu atamshinda shetani na kuleta haki katika maisha yako hapa duniani? Hakuna mwingine ila Mungu. Kama huu ndiyo ukweli, basi Mungu anataka kujithihirisha kwako na kuleta haki duniani. Kwa sababu mtume hawezi kumshinda shetani. Hivyo, kama imani yako inakufundisha kuwa Mungu hawezi kujithihirisha

kwako na kumshinda Shetani, inakudanganya na haijui namna ambavyo haki ya Mungu hupatikana.

*Mungu anataka kuwaokoa wanadamu yeye mwenyewe.*

Shetani ndiye kinara wa dhuruma na amemfunga mwanadamu kwa minyororo. Kama ndivyo ilivyo, nani anaweza kumuokoa mwanadamu aliyefungwa kutoka kwa shetani na dhambi?. Je mtu aliyefungwa anaweza kujiokoa mwenyewe toka kwa shetani? Hapana. Kwanza, yupo kwenye kifungo cha kiroho na mfungwa hawezi kujiokoa. Pili, shetani ni mkuu wa hili gereza la kiroho, ana nguvu kuliko mwanadamu, anamchukia mwanadamu, na pia haamini katika uhuru na ukombozi wa mtu yeyote. Hakuna mtu anayeweza kujiokoa. Kila mwanadamu anamuhitaji Mungu aje amuokoe. Mungu kuja haimaanishi amejificha.

Imani yako inakupotosha kama inasema unaweza kujiokoa mwenyewe toka kwa shetani kwa matendo yako mema. Kama hatujaokolewa na kuwekwa huru kiroho, hali hii isiyo ya kimungu inatuzuia kuweza kufanya zuri lolote linaloweza kumridhisha Mungu. Mungu ndiye asili ya upendo na haki. Huwezi kufikiri, kuzungumza na kutenda sawasawa na mapenzi ya Mungu isipokuwa tunakaa ndani ya pendo la Mungu na haki yake kwanza. Kwa maneno mengine, matendo yako hayatakuwa na mantiki kwa Mungu kama

usipoungana na Mungu na ushirika wako kwa shetani na dhambi kuvunjwa. Shauku ya Mungu ni kumuweka huru mwanadamu dhidi ya shetani kwanza. Uhuru dhidi ya shetani ni mwanzo wa matendo mazuri kwa Mungu. Kwa maneno mengine, kusudi la kwanza la Mungu kwako ni kujidhihirisha kwako na kukuweka huru. Matendo yanayomridhisha Mungu yanaanza pale unapokuwa umeokolewa na kuwekwa huru.

Kwa hiyo Mungu mwenye upendo hajifichi na hacheleweshi wokovu mpaka baada ya kifo.

**Je ni sawa kusubirisha wokovu wa mtu mpaka kesho wakati anaulilia leo?**

Kama shetani amewatenga wanadamu na Mungu na ufalme wake hapa duniani na kuwafanya wenye dhambi, wokovu wao lazima upatikane hapa hapa duniani. Je wale waliolazimishwa kutengana na kuishi mbalimbali hapa duniani hawatamani kuungana haraka iwezekanavyo? Je haitaumiza zaidi kama kuungana kwao kutacheleweshwa? Mungu na mioyo yetu pia ipo hivyo. Mungu hataki kuchelewa kuja kwetu. Hujidhihirisha kwetu hapa hapa duniani. Mioyo yetu haitatulia kama wokovu wetu utacheleweshwa. Kwahiyo imani yako haiwezi kupatana na moyo wa Mungu kama inamficha Mungu na kuchelewesha wakovu mpaka baada ya kifo.

Biblia humdhihirisha Mungu lakini Qur'ani humficha. Haipendezi kama mtu atamficha mtu wa muhimu sana kwako. Yesu alifundisha kuwa Mungu hajawahi kujificha kwako. Anakupenda. Pia, Yesu ni chanzo cha maneno haya yenye uhalisi na hoja hizi nilizokushirikisha. Kama moyo wako unaona hoja hizi ni kweli, na wewe unatakiwa kumfuata Yesu

**Wakati wa kutafakari 4**

1. Kwanini haina maana kuamini kuwa dunia ilitokea tu kwa bahati au ilijitokeza yenyewe?
2. Watu wengi duniani wanataka kuwa na mipango mizuri ya maisha yao ya baadae. Mpango unahitaji kanuni. Kanuni bora haiwezi kuundwa bila kulinganisha na uzoefu wa nyuma. Je falsafa ya uwepo wa nasibu inaendana na uhiari na ufanyaji maamuzi kwenye maisha yetu?
3. Je tuna uwezo wa kuhoji[4] na kupata ukweli?

---

[4]Kuna watu kati ya wafuasi wa dini zote wanaosema Mungu wao ndiye Mungu pekee wa kweli na wamepewa dini nzuri na bora kuliko zote Hebu fikiri, kama wafuasi wa dini zote duniani wangekuwa na mtizamo wa aina moja, na kuto amini kulinganisha imani, kuhoji imani yao, na kutafuta ukweli toka kwa watu wengine au kuishi bila changamoto au maswali. Je tuna awezaje kujua Mungu wa kweli kama hakuna kulinganisha?

4. Soma Rumi 2:14-16, halafu II korintho 4:2 na mwisho Galatia 3:24 na uone kama unaweza kuwasaidia watu kuilewa sheria ya Mungu wenyewe kupitia dhamiri zao na kuruhusu sheria ya Mungu kuwapeleka kwa Yesu.
5. Ndani ya mioyo yao, je watu wanashauku ya kumwona na kuungana na muumba wao?
6. Kwanini Mungu wa kweli hawezi kujificha?
7. Kama mtu hamfahamu Mungu kibinasfi, je anaweza kuwa mjumbe wa Mungu?
8. Kwanini tuache suala la wokovu mpaka baada ya kufa kama unapatikana leo? Je si vizuri kuokoka sasa hivi?

## Jinsi ya kutofautisha kati ya Mungu wa kweli na Mungu wa uongo?

Kuna Mungu mmoja tu ulimwenguni, lakini kuna tofauti kati ya huyu Mungu mmoja na miungu wengine ambao wameanzishwa na dini mbali mbali. Hivyo basi ni dini gani ilioanzisha Mungu wa kweli?

### Je, tunaweza kujua ni dini gani yenye Mungu wa kweli?

Ndiyo. Tuna macho ya kusoma na kuona, masikio ya kusikiliza, akili za kuchanganua mambo, mioyo ya kutathmini na kutambua ukweli na pia dhamira njema ya kusimamia ukweli kwa hali na mali. Hivyo basi tuna uwezo wa kumtafuta Mungu wa kweli, kumpata na kuishi nae. Mtu yeyote anaweza kusoma na kusikiliza tabia za miungu katika vitabu mbali mbali vya dini hizo. Tunaweza kufananisha na kutofautisha Mungu wa kweli na wauongo.

**Ni vigezo gani vya kutumia kujua Mungu wa kweli ?**

Kuna:

1. Vigezo vya kifalsafa
2. Vigezo vya misingi ya kiimani
3. Vigezo vya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimaadili.

**Vigezo vya kifalsafa**

*Kigezo cha kifalsafa cha kwanza ni lazima Mungu awe na utu.*

Mungu lazima awe na utu ili aweze kujenga mahusiano ya kiutu na watu na kuweza kuwasaidia. Mungu asiye na utu hawezi kujenga mahusiano yoyote ya kiutu na mtu akamsaidia au kumwongoza. Kwa hiyo Mungu kama huyu hana msaada na hawezi kutumainika. Kwa mfano, mungu kwenye Uislam hana utu, kwakuwa mtume Muhammad hakuweza kumwona Mungu, alimwelezea Mungu kama mungu asiyeonekana wala asiye jidhihirisha. Kufuatia kifo chake, wanafalsafa wa kiislam walijenga falsafa yao kutokana na maelezo ya mtume Muhammad na kumtafsiri Mungu kama asiye na utu, asiye fikika na asiye julikana.

Kama Mungu haonekani, basi hawezi kudhihirisha mawazo, maneno na hata matendo yake. Hii pia inamaanisha Mungu hana mawazo ya kudhihirisha mipango yake, wala maneno ya kuongea kuhusu mipango yake na wala uwezo wakuweka mipango yake kwenye matendo. Kwa maneno mengine hawezi kuongea kwa sababu mwenye utu tu ndiye anayeweza kuongea sio asiye na utu. Hawezi pia kuumba kwani uumbaji unahitaji maneno; kama tusemavyo "Mungu alisema na ikawa". Kwa sababu mungu wa Uislam hawezi kusema, basi hawezi kupewa sifa ya uumbaji.

Kwa hiyo asili ya kutokuwa na utu ya mungu wa Uislamu haikumruhusu kujidhihirisha wala kuwa na mahusiano ya kiutu na Muhammad. Kwa vile hawezi kuwa na mahusiano ya kiutu na yeyote, Kwa hiyo hataweza kusaidia wala kuokoa, kwa sababu kusaidia na kuokoa kuna hitaji mahusiano binafsi.

Waislam wengi wanasali na kuomba Mungu wao awaongoze katika njia ilio sahihi. Atawezaje kuwaongoza katika njia iliyo sahihi kama hawezi kujidhihirisha kwao ili awaongoze na kuwalinda? Mwongozo na ulinzi vyawezekana ikiwa tu kuna mahusiano binafsi, Quran inasema Mwenyezi Mungu hajionyeshi na wala hana uhusiano na mtu yeyote.

Kwa hiyo kigezo cha msingi cha kwanza cha kutambua Mungu wa kweli ni kwamba, lazima Mungu

ajithibitishe kuweza kuokoa watu kutoka kwa shetani na dhambi. Kwa hiyo, kama mungu wa dini yako hajionyeshi wala kujidhihirisha, basi huyo si mungu wa kweli.

*Kigezo cha pili cha kifalsafa ni lazima uwepo wa Mungu utende kazi kila mahali.*

Mungu anaweza kuwa nasi kwa vitendo. Kwa vile sote binadamu na Mungu tuna tabia ya utu, pia tunaweza kuhisi utu wa Mungu kibinafsi kama yuko nasi na ndani yetu.

Tuna kila sababu ya kusema Mungu yuko ndani yetu. Waislam wengi hutupilia mbali falsafa ya Qura'ni kuhusu Mungu na kutangaza uwepo wa mungu ndani yao. Nimesikia mara nyingi sana waislam wakidai "Mungu yu ndani ya damu yao. Na yuko karibu nao kuliko mishipa ya damu." Je, kweli Mungu yuko na waislam? Je, hili laweza kuthibitika na sababu za msingi? Hapana. Ngoja niwaeleze kwanini jibu ni hapana.

Kama Mungu yuko pamoja nawe, basi ina maana yuko pamoja nawe kwa uhakika, huruma na upendo wake wote. Ni Mungu mwema, mpole mwenye rehema na huruma, kwa hiyo hatamani kukuacha na mashaka katika sehemu yoyote ya maisha yako, badala yake hutupa kujiamini 100% kwa siku zijazo. Ukisema

hakupi ujasiri wa kumwamini basi ina maana hakupi mwongozo na huyo si Mungu wa kweli

Wewe kama mwislamu unasema kwamba Mungu yuko pamoja nawe, ni mwanga wa njia yako, na anakuongoza kikamilifu. Ngoja nikuulize swali muhimu la kiroho. Je, umeokoka, na unauhakika wa kwenda mbinguni ama paradiso? Jibu lako, la mtume wako na la Qura'ni yote ni "Hapana". Hii ina maana mungu wako hajakupa uhakika kuhusu hatima yako. Inawezekanaje Mungu mwenye uhakika awe nawe na bado usiwe na uhakika? Hii ina maana ya kuwa Mungu wa uhakika ama Mungu wa kweli hayupo pamoja nawe lasivyo ungekuwa na uhakika. Kwa maneno mengine dini haijaweza kukuunganisha na Mungu wa kweli. Uwepo wa Mungu unaweza kuthibitika pale tu tunapookolewa na Mungu hapa duniani na kuwa na uhakika wa kwenda mbinguni ama paradiso.

*Kigezo cha tatu ni lazima Mungu ajulikane.*

Mungu wa kweli ni yule unayeweza kumjua kibinafsi, ni yule unaye weza kumfuata kulingana na kuzoena naye. Huwezi kumfuata mtu usiyemjua. Na kwa Mungu pia ni vivyo hivyo. Hataki umfuate bila kumwelewa vizuri, au kwa kupitia mtu mwingine. Anataka wewe uwe pamja naye kupitia mahusiano binafsi.

## Vigezo vya misingi ya kiimani vya kumtambua Mungu wa kweli

*Kigezo cha kwanza cha kiimani ni kwamba Mungu lazima awe mwadilifu.*

Hii ina maana Mungu mwadilifu hawezi kuwa na matendo maovu au kujaribu kuyahalalisha; kwasababu asili yake ni mkamilifu na hana uovu. Kwa hiyo ukiona kwenye kitabu cha mungu wako kwamba ni muumbaji wa dhambi na maovu, au ameyahalalisha kwenye baadhi ya mazingira, Mungu huyo hawezi kuwa Mungu wa kweli. Unapaswa utathmini vizuri maneno na matendo ya Mungu wako kama unataka kujua kama imani yako ni ya mbinguni au siyo.

*Kigezo cha pili cha kiimani ni kwamba Mungu lazima awe ni mwenye haki.*

Hii ina maana kuwa Mungu hawezi kusema na kufanya mambo yasiyo ya haki. Kwa mfano: Mungu hawezi kuwapa Mitume na viongozi haki zaidi ya wengine kwa sababu ni mwenye haki. Hawezi kuwapa wanaume haki zaidi ya wanawake au kuwaruhusu wanaume kuwapiga wake zao. Hawezi kuwapa baadhi ya wafuasi wake haki zaidi ya wengine. Hawezi kuchochea makundi na kuhamasisha watu kutokujali haki za wengine. Kama mungu wako amehalalisha matendo yasiyo ya haki kama haya, basi huyo si Mungu wa kweli.

*Kigezo cha tatu cha kiimani ni kwamba Mungu lazima awe mtakatifu.*

Hii inamaanisha Mungu hawezi kutenda dhambi, wala kuumba dhambi, wala kuhamasisha dhambi au kuhalalisha dhambi kwa namna yoyote. Je, inawezekana Mungu aliye mtakatifu kuwapotosha watu na kuwafanya wadhambi? Hapana haiwezekani kabisa. Hivyo basi, ukiona mungu wako anapotosha watu na kuwafanya wadhambi, huyo hawezi kuwa mtakatifu. Na mungu kama huyo hawezi kuwa mfano kwa watu.

*Kigezo cha nne cha kiimani ni kwamba Mungu lazima awe na upendo na upole.*

Hii ina maana Mungu huheshimu na kuwapenda watu na huwakaribisha kwake kwa hekima, upole na amani. Kwa kuwa yeye mwenyewe alituumba, yeye mwenyewe pia lazima aoneshe njia za upendo na upole za kuleta umoja baina ya watu. Kama vile mzazi na watoto wake, inabidi akujie kwa upendo na nia ya kukufundisha ili umfuate yeye kwa jitihada na kuwa naye. Mungu hatakiwi kuwa kama mtu katili ambaye hajali haki zako wala uhuru wako wakufanya maamuzi. Kama mungu wako hana upendo na upole kama huu, huyo si mungu wa kweli na dini yake haiwezi kuzaa upendo, upole na amani kati ya watu.

Sasa ni wakati mwafaka wa kukueleza vigezo vya kijamii, kisiasa na kiuchumi vya kumtambua Mungu wa kweli.

## Vigezo vya kijamii

Mungu wa kweli hana ubaguzi wowote iwe wa kijinsi, rangi, utaifa, kiimani, wadhifa au kitu chochote kinachoweza kutenganisha watu. Mungu wako hawezi kuwa wa kweli kama anawapa haki zaidi wanaume kuliko wanawake, kwa mabwana kuliko watumwa, kwa wafuasi wake kuliko watu wengine.

## Vigezo vya kisiasa

Mungu wa kweli huanzisha na kukuza uongozi wa staha badala ya udikteta. Machoni pa Mungu aliye mkubwa kuliko wote ndiye aliye mnyenyekevu na mtumishi kwa wote. Mungu wako si mungu wa kweli kama anawapa majukumu ya kidikteta kwa manabii wake au wafuasi wake.

## Vigezo vya kiuchumi

Mungu wa kweli huamini ya kuwa watu wote, wafuasi na wengine wanastahili kupokea ujira sawasawa na muda na kazi wanayofanya. Mungu wa kweli hadharau haki, kupuuza au kutoza kodi kubwa kwa wasio wafuasi.

## Vigezo vya kimaadili

Mungu wa kweli hahalalishi kusema uongo, kudanganya au kitendo chochote kisicho cha maadili bila kujali mazingira yoyote. Mungu wa kweli ni mtakatifu na utakatifu wake siku zote ni kupingana na dhambi iwe imetendwa na mfuasi wake ama mtu asiye mfuasi wake. Mungu wako si wa kweli kama anaruhusu wafuasi wake kusema uongo na kudanganya wengine.

Kuna miungu ya uongo na imani nyingi duniani. Hutaweza kutambua kama unamfuata Mungu wa kweli au wa uongo bila kujifunza Mungu wa kweli yupoje. Vigezo hivi vilinisaidia kumtambua Mungu wa kweli na kujenga uhusiano wa karibu na muumba na mwokozi wangu. Ni maombi yangu kwamba viwe vya msaada pia katika maisha yako ili uweze kuiishi furaha ya Mungu daima.

## Wakati wa kutafakari 5

1. Kama kweli tumeumbwa kwa mfano wa Mungu je, hatutaweza kumjua muumba wetu?
2. Kama tunaweza kutofautisha kati ya lililosawa na lisilosawa, zuri na baya je, hatuwezi kutofautisha kati ya Mungu wa kweli na mungu wa uongo?
3. Kama mungu anahamasisha dhambi, je huyo ni Mungu wa ukweli?

4. Je, ni vyema kuwa na uhusiano wa binafsi na Mungu au si vyema?
5. Ni wakati gani tunaweza kuthibitisha kwamba tuna uwepo wa Mungu ndani yetu?
6. Nani anaweza kumwelezea Mungu vizuri zaidi, ni yule mwenye uhusiano naye binafsi au yule asiye na uhusiano binafsi na Mungu?
7. Kama una amini Mungu binafsi, mwombe akuongoze katika maisha yako binafsi.

# Tofauti kati ya Mungu wa Uislamu na Mungu wa Ukristo.

Baadhi ya watu wanasema waislamu na wakristo wote ni wafuasi wa Mungu mmoja. Hawajui maandiko katika Uislamu yanaongelea mungu mwingine tofauti na Mungu wa Ukristo. Kwa sababu hii nataka kulinganisha kati ya maandiko ya Biblia na Qur'ani ili tujionee utofauti mkubwa uliyoko kati ya mungu wa Uislamu na Mungu wa Ukristo.

## Tofauti ya kwanza: mungu wa Uislamu hawezi kuwasaidia watu.

Kama nilivyojadili hapo awali, mungu wa Uislamu anaelezewa kuwa mungu asiye na mahusiano na Qura'ni yenyewe hata na wasomi wa dini ya kiislamu. Kwa hiyo hawezi kujenga mahusiano yoyote ili kusaidia. Unaweza ukasema kwamba ingawa mungu wa Uislamu hana mahusiano binafsi lakini anawatuma malaika ili kusaidia. Hii ni falsafa ya uongo. Kwa nini? Kwasababu mungu asiye na uwezo wa kujenga uhusiano awezaje sasa kujenga uhusiano na malaika ili kumfanya mjumbe wake kwa wanadamu. Haiwezekani mungu asiye na mahusiano yoyote kuwa na mahusiano binafsi na mjumbe wake.

Kwa hiyo tunaona kwamba Mungu wa Uislamu hawezi kutegemewa kusaidia kwa sababu ya asili yake. Lakini Mungu wa Ukristo anaweza kusaidia. Mungu wa Biblia ana utu, ana mahusiano na watu anatenda na anaweza kusaidia. Katika kitabu cha Isaya sura ya 45 msatari wa 2 Mungu wa wakristo anasema: nitakwenda mbele yako na kusawazisha milima. (NIV) Tunaona ya kwamba Mungu anatembea na watu wake.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa kusudi. Ili kuweka kusudi maishani mwetu, uwepo wa utu wa Mungu na mwongozo ni lazima. Maneno "uwepo na mwongozo" yanaweza kutumika tu tunapo muongelea Mungu mwenye uwezo wa kujenga mahusiano. Na ndio maana mitume wa Yesu waliandika kuwa walishuhudia ufunuo wa Mungu. Mtume Yohana anasema Mungu alifanyika mwili na akakaa kati yetu nasi tukauona utukufu wake amejaa Neema na kweli (soma Yohana 1:14)

Kwa hiyo unaona kwamba mungu wa Uislamu hawezi kujidhihirisha na kusaidia. Lakini Mungu wa Ukristo ana asili ya kujidhihirisha mwenyewe ili kuwaongoza watu, kuwasaidia na kuwaokoa.

**Tofauti ya pili:mungu wa Uislamu ni muumbaji wa mema na mabaya.**

Mungu wa Ukristo ni muumbaji wa mema tu. Mungu wa Uislamu anajulikana kama mkuu katika uumbaji wa yote mema na mabaya, na mhamasishaji wa dhambi na kuwapotosha wanadamu. Mungu wa Ukristo ni mkuu katika mema tu. Asili yake ni utakatifu na uadilifu. Na hawezi kuwaza kamwe kuwapotosha wanadamu ama kuumba dhambi.

Sura Al Hadid (57) mstari wa 22, Sura Al A'raf (7) mstari 16 na Sura Ash Shams (91) mstari 8 maandiko haya ya Qur'ani yana thibitisha kwamba mungu wa kiislamu ndiye aliyebuni taabu, dhambi na upotoshaji na kuvileta katika uumbaji wake. Lakini Mungu wa Biblia hahusiki na ubunifu, mpango wala uumbaji wa dhambi na upotoshaji. Mungu mwema, mwadilifu, mtenda haki, mwenye upendo na upole hawezi kupotosha watu. Kazi yake ni kuwatakasa. Kama mungu wa Uislamu si mkweli na ni muumbaji wa dhambi, basi hataweza kuongoza watu kwenye njia ya kweli.

Kwa kuhusisha mungu na uongo na dhambi, Qur'ani inapotosha watu. Uumbaji wa dhambi ndiyo dhambi yenyewe, kwa hiyo mungu wa Uislamu ni mwenye dhambi wakati Mungu wa kweli hawezi kuwa na dhambi. Pili ni kwamba watu hawataona umuhimu wa

kuacha dhambi kwa kuwa mungu wa Uislamu ameshindwa kuacha dhambi. Kama mungu ameumba dhambi kwa ajili ya watu, kwa nini watu wasitende dhambi? Mungu muumba dhambi ni kikwazo kwa kuleta ukweli katika jamii. Ki ukweli Mungu mwaminifu hawezi kuumba dhambi kwa sababu ya asili yake ya utakatifu. Kwa hiyo mungu anayesemwa na Qur'ani si wa kweli.

Mungu wa Biblia ni Mungu wa kweli. Injili ya Yesu Kristo katika kitabu cha Yohana sura ya 2 mstari wa 21 imeandikwa "Hakuna uongo katika ukweli."(KJV) na pia katika kitabu cha Yakobo sura ya 3 mstari wa 17 kinasema " lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi; tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu; imejaa huruma na matunda ya matendo mema; haina fitina, haina unafiki." (MKJV)

## Tofauti ya tatu: mungu wa Uislamu yupo kinyume na uhuru wa kuchagua

Sura Al Ahzab (33) katika aya ya 36 inasema kwamba hakuna aliye na haki ya kupinga maneno ya Muhammad, mtume wa Uislamu. Lakini kwa wa Kristo katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati sura ya 18 mstari wa 22 inasema tusikubali kila neno la manabii bali una haki ya kuyakataa au kuyakubali baada ya kuyapima.

## Tofauti ya nne: mungu wa Uislamu anapingana na fursa sawa

Tunajua kulingana na Qur'ani na vitabu vya dini kwamba Muhammad anahaki zaidi kuliko waislamu wengine, wanaume wakiislamu wana haki kuliko wanawake wa kiislamu, waislamu wenye ngozi nyeupe wana haki kuliko waislamu weusi na waislamu kwa ujumla wana haki zaidi kuliko wasio waislamu[5]. Lakini imani ndani ya Kristo Yesu ndiyo inayotufanya tuwe sawa na iwe kwa myahudi au si myahudi, mtumwa au alie huru, mwanaume au mwanamke. (Wagalatia 3:28: Wakolosai 3:11)

## Tofauti ya tano; mungu wa Uislamu ana amini katika mfumo dume.

Katika sura An Nisa (4) mstari wa 34 na Sura Sad (38) msatri wa 44 ya Qur'ani ina sema ya kuwa wanaume wana haki ya kuwapiga wake zao. Kwenye Sura An Nisa (4) aya 15 hadi 16, wanaume wana haki ya kuwafungia wake zao kwenye chumba ili kuwa adhibu kwa ukosefu wa kimaadili mpaka watakapo kufa. Lakini kwa makosa hayo hayo wanaume wanachapwa viboko na kutembea huru.

---

[5] Angalia rejea zifuatazo na rejea chini ya kichwa "Uongozi ndani ya Uislamu ni mtafaruku"

Injili ya Yesu Kristo hairuhusu kamwe matendo ya kusikitisha kama hayo; katika kitabu cha Waefeso sura ya 5 mstari wa 25 na 28 inasema lazima mwanaume ampende mke wake kama anavyo jipenda mwenyewe.

**Tofauti ya sita: mungu wa Uislamu anafurahia unyanyasaji.**

Qura'ni Sura Al Tawba (9) aya ya 28 inaongelea jinsi wasio waislamu ni wachafu: kwenye Sura Al Anfal (8) aya ya 55 ina sema wasio waislamu ni wabaya kuliko dubu; katika Sura Al Bagharah (2) aya ya 65: sura Al Meada (5) aya ya 60 na sura Al Juma (62) aya ya 5 imeandikwa ya kwamba wayahudi na wakristo ni nguruwe, nyani na punda. Lakini katika injili ya Yesu Kristo hakuna tofauti kati ya wayahudi na wengine, wote ni sawa mbele ya macho ya Mungu aliye waumba kwa mfano na mkono sawa.

**Tofauti ya saba: mungu wa Uislamu ndiyo chanzo cha mmomonyoko wa maadili**

Sura Al Anfal (8) aya ya 30 na sura Yunus (10) aya ya 21 in sema Mwenyezi Mungu ndiye mdanganyifu bora kuliko wadanganyifu wengine wote. Sura Al Bagharah (2) aya ya 225, sura Al-e Imran (3) aya ya 28 na sura An Nahl (16) aya ya 106 zina wahimiza waislamu kusema uongo pale inapo wabidi. Lakini injili katika kitabu cha Yohana sura ya 2 mstari wa 21 imesema:

hakuna uongo unaotokana na ukweli. Pia katika kitabu cha Kutoka sura ya 23 mstari wa kwanza na pili zinasema: usitoe habari za uongo. (NIV) Usi shirikiane na mtu mwovu ili kuwa shahidi mbaya. usijumuike na genge la watu kutenda uovu wala usijumuike na genge la watu kutoa ushahidi mahakamani ili kupotosha haki. (NIV)

Umeona utofauti? Mungu wa Ukristo anasema usiseme uongo kamwe, lakini mungu wa Uislamu anasema inategemeana na mazingira.

**Tofauti ya nane: mungu wa Uislamu anazalisha madikteta.**

Sura Al Anbiya (21) aya ya 23 inasema: Yeye hahojiwi kwa ayatendayo, na wao ndio wanao hojiwa kwa wayatendayo. Sura Al Ahzab (33) aya ya 36 inasema: Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Sura Al Mujadila (58) aya ya 20 na 21 inasema wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na mtume wake ni miongoni mwa watu watakao dhalilishwa sana. Mwenyezi Mungu ameandika: “Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.”

Unaona kuwa uongozi katika dini ya Uislamu una misingi ya kidikteta kwanzia mizizini hadi matawi. Lakini ngoja uangalie uongozi wa kwenye Biblia ulivyoundwa kwa kuwapa uhuru watu.

Katika kumbukumbu la Torati sura ya 18 mstari wa 22 inasema kuwa kama nabii hayuko sahihi, msimwogope wala msimtii.

> *Atakaponena nabii kwa jina la Bwana, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena Bwana; kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope. (Kumbukumbu la 18:22 EVS)*

Katika kitabu cha Isaya sura ya 1 mstari wa 18 Mungu anawaambia watu wake; Njoni, basi, tuhojiane. Unaona kwamba katika Biblia watu wana haki ya kutumia uhuru wao wa kuchagua waliyopewa na Mungu kuhoji maneno ya Mungu au manabii wake nakujiepusha na utii usiyo na mashiko. Kwa nini? Kwasababu uhuru wa kuchagua ni zawadi kutoka kwa Mungu na Mungu anaheshimu uhuru. Inashangaza sana hasa uongozi wa Yesu. Kama kiongozi yeye mwenyewe aliwaosha mitume wake miguu (Yohana 13:5) na kuhusu ubora wa kiongozi anasema: Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao

huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu yeyote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; (Mathayo 20:25-27)

Kwa hiyo unaona kuwa Yesu anafundisha kuwa unatakiwa kufisha mbegu ya udikteta moyoni mwako. Hii itakusaidia kuheshimu uhuru wa kila mtu bila kujali utaifa, asili wala imani yake.

## Tofauti ya tisa: mungu wa Uislamu hana hekima.

Ni aina gani ya hekima, kwamba Mwenyezi Mungu mwenyewe anawaweka watu dhambini na kuvunja sheria, alafu anawataka wamsifu kwa kile alichokifanya.? Hekima ya kweli haiwafungi watu minyororo ya dhambi, bali inakuwa mwanga wa uhuru kwao. Mungu wa Biblia haku umba watu wenye dhambi. Wanadamu wenyewe ndiyo waliokuwa chanzo cha kuanguka kwao dhambini. Lakini Mungu mwenye moyo wa ubaba alijitoa na bado anaendelea kujitoa kwa ajili ya kuwaokoa. Kuna tofauti kubwa kati ya mungu wa Uislam na Mungu wa Ukristo.

**Tofauti ya kumi: mungu wa Uislam ndiye aliyempotosha shetani na kumfanya adui wa wanadamu.**

Katika Sura Al A'raf (7) aya ya 16 inasema shetani alipotoshwa na kufanywa mdanganyifu na Mwenyezi Mungu. Kwa nini? Kwa sababu alitaka kuumba mleta matatizo kwa watu hasa kwa wale ambao wangempinga. Je, si jambo lakustaajabisha kwamba huyu ndiye anayeitwa mwenye huruma katika kila sura ya Qur'ani?

Mungu wa Ukristo yuko tofauti sana. Hakumpotosha shetani. Shetani mwenyewe ndiye alietumia uhuru wake vibaya, alimwasi Mungu na akawa chanzo cha dhambi na uvunjaji wa sheria duniani. (Mwanzo 1:31, Ezekieli 28:14-17, Yuda 6) Mungu yupo kinyume na shetani katika kila jambo, na anataka kuwaweka huru watu hata maadui wake kutoka kwenye mikono ya shetani.

**Tofauti ya kumi na moja: mungu wa Uislamu ana tumia majini kueneza Uislamu**

Katika Sura Al Jinn(72) aya ya 1-13 ina sema Mwenyezi Mungu anatumia majini kueneza dini ya Uislamu. Kitabu kuhusu maisha ya Muhammad (kama kilivyo andikwa na Ibn Ishaq) kinasema katika ukurasa wa 106 hadi 107 kwamba hana uhakika kama sura ya kwanza

ya Qur'ani sura Al Alagh (96) ilifunuliwa kwake na Mwenyezi Mungu ama shetani.

Sababu ya mungu wa Uislamu kutumia majini katika kazi zake ni kwa sababu anaviashiria vya mungu wa kipagani. Kwani ni katika upagani tu ndipo majini yanaaminika. Mungu  wa kweli hawezi kuongozana na majini ili kueneza dini yake. Kwa hiyo unaona kwamba ni vigumu kutenganisha dini ya Uislamu na tamaduni za kipagani. Tamaduni na imani za kipagani zimekua sehemu ya Qur'ani kitabu kinacho aminika kuwa kitakatifu na cha kimbingu. Katika Qur'ani tunasoma kwamba majini ni watumishi wa manabii.

Mungu wa Ukristo sio tu hatumii majini kueneza maneno yake bali pia anawaweka watu huru dhidi ya majini na kuwaponya. Mungu ni mtakatifu, mwenye haki na mwadilifu na anajua majini hueneza udhalimu na hayasemi ujumbe wa kweli.

**Tofauti ya kumi na mbili: mungu wa Uislamu anawaacha wafuasi wake waaminifu na mashaka kuhusu hatima yao.**

Katika Qur'ani Sura Mariam(19) aya ya 68 inasema waislamu waaminifu hupelekwa jahannamu mara baada ya kufa na watasubiri kule pamoja na waovu mpaka siku ya hukumu. Hii imejenga hofu kubwa kati ya waislamu waaminifu ikiwemo Muhammad, hawana

uhakika kama wataweza kukidhi vigezo siku ya hukumu. Hofu hii ya kiroho ya kuto kuwa na uhakika imevunja mioyo ya waislamu wa kweli na hakuna hata mmoja wao mwenye ujasiri wa  kujibu swali kama wataokolewa au la. Jibu ni “Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayejua”

Lakini wakristo waaminifu wataenda kwa Mungu mara tu watakapokufa. Swala la uzima au kifo kwa wakristo lilishapatiwa ufumbuzi. Unaingia kwenye ufalme wa uzima wa milele ungali hai duniani kama ukichagua kumfuata Kristo aliye hai na mbinguni. Kama ukifanya hivyo utashinda hukumu na kamwe hautahukumiwa tena. Utafika unaenda mbiguni.

### Tofauti ya kumi na tatu: mungu wa kiislamu hapatikani duniani

Kwenye Uislamu huwezi kuupata ufalme wa Mungu hapa duniani. Kwa sababu mungu hapatikani na kwa hiyo  na ufalme wake haupatikani.

Kila siku waislamu husema Mungu yuko pamoja nao. Lakini hii ni tofauti na misingi ya Qur’ani na Uislamu ambayo inaamini kuwa mungu hajidhihirishi. Aidha Mungu wa Ukrito ni Mungu anayejidhihirisha na anayepatikana. Amejifunua katika Yesu Kristo ili kukuokoa na kukuunganisha naye ili uwe na mahusiano ya milele naye. ukisha kumruhusu akuokoe

katika Jina la Yesu Kristo utakuwa wake milele na hakuna kitakacho kutenga naye.

## Tofauti ya kumi na nne: mungu wa Uislamu ana mbingu ya kipagani

Hakuna taarifa ya uwepo wa Mungu katika paradiso ya Uislamu kwenye Qur'ani. Lakini Qur'ani hiyo hiyo inaendelea kuwaahidi wanajihadi na wale watakao pata upendeleo wa Mwenyezi Mungu kuwa watakwenda paradiso na kuwafurahisha pamoja na wasichana wazuri mabikra. (Qur'ani 37:48:78: 33) Hii ilikua imani ya kipagani enzi za Muhammad.

Siyo kama paradiso ya kiislamu, mbingu kwenye kitabu kitakatifu cha Ukristo sio sehemu ya tamaa za binadamu. Ni kiti cha enzi cha Mungu, sehemu ya furaha na amani ya milele na Mungu. Katika Injili yake Kristo anatufundisha  wafuasi wake kuwa tutakuwa na Mungu mbinguni (Yohana 14:1-6) injiii ya kristo inasema:

Mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, watasimama mbele ya kile kiti cha enzi, na wakimsifu Mungu kwa kuwaokoa. (Ufunuo 7:9)

Kwa hiyo unaona mbingu kwenye kitabu kitakatifu cha kikristo iko mbali kabisa na maovu ya paradiso ya

kiislamu. Mungu wa Ukristo yuko tofauti sana na mungu wa Uislamu. Anaaminika na ni mkuu kuliko Mwenyezi Mungu katika kila jambo. (Ufunuo 19:16)

Nimewapa sababu zote hizi ili yamkini unaweza uhamasike kuisoma injili ya Yesu Kristo wewe mwenyewe na kujionea ukweli kwa macho yako. Asanteni kwa kutumia muda wenu na mimi.

**Wakati wa kutafakari 6**

1. Je, mungu wa kiislamu anaweza kutembea na watu wake na kuwapa kusudi maishani? Kwa nini?
2. Kwa nini sote tunahitaji kumfuata Mungu wa biblia na sio wa Qur'ani?
3. Je, sifa za mungu wa Uislamu zinaathiri maisha ya watu kama watamfuata?
4. Je, kuna umuhimu gani kwetu kumfuata Mungu wa kweli na kumdhihirisha kwa wengine?
5. Sasa tumwombe Mungu wa kweli atuongoze yeye mwenyewe ili tuwe mfano wake kwa wengine.

## Je, mungu wa Uislamu anaweza kuwa kiongozi mzuri?

Hatuwezi kujibu swali hili ipasavyo bila kufahamu sifa za kiongozi mzuri na jinsi anavyo fanya kazi kwa kutumia macho ya dhamiri zetu. Ngoja tuangalie sifa na matendo ya kiongozi mzuri.

### Kiongozi mzuri anatoa hatima nzuri na salama kwa wafuasi wake

Unahitaji kufika mahali fulani; yeye anajua njia na unahitaji mwongozo wake sahihi na uliyo nyooka. Kiongozi mzuri anapo ahidi kukufikisha mwisho wa safari yako, inamaana yuko tayari kusimamia ahadi yake na kuitekeleza kwa gharama yoyote. Anakuhakikishia kwamba utafika; hasa kwasababu yeye ni mkuu na anauwezo wote wa kushinda vikwazo kwa hiyo unamwamini asilimia 100%. Kiongonzi mzuri anajua vitisho na hatari zote za njiani na anajua namna bora ya kupambana navyo. Kiongozi mwema hawezi kushirikiana na wapanga maovu ili kuwa tishio kwa wafuasi wake, bali hupingana nao ili kujenga imani thabiti mioyoni mwa wafuasi wake.

Je, Mwenyezi Mungu ana hatma ilio nzuri na salama kwa wafuasi wake na je, anawahakikishia wafuasi wake ya kwamba yeye mweyewe hata kuwa tishio kwao? Je,

ana sifa zote za kuwafanya watu wa mwamini kwamba ata waongoza na kuwafikisha salama? ngoja tuangalie safari na Mwenyezi Mungu inaishia wapi?

Kwenye Qur'ani sura ya Mariam(19) aya ya 67 hadi 72 tunajifunza kwamba Mwenyezi Mungu atawachukua wafuasi wake waaminifu pamoja na walio waovu nakuwakusanya jahannamu kwa ajili ya hukumu. Baada ya hukumu waovu watabaki jahannamu lakini baadhi ya walio waaminifu wataweza kwenda paradiso kama matendo yao mazuri yatakuwa mengi kuliko maovu, na kama wataweza kuvuka daraja dogo jembamba la Sirat[6]

Katika aya hizi mungu wa Uislamu ana waambia wafuasi wake waaminifu kwamba "Mmekuwa waaminifu kwangu kuliko watu wengine ili kunifurahisha. Lakini siwapi uhakika wa thawabu katika hilo. Mnaweza kubaki jahannamu na kuteseka milele" Ati ni kiongozi mzuri!

---

[6]'Sirat' ni daraja jembamba sana, ni jembamba na lenye makali kama kali ya kisu, ndilo linalo tofautisha kati ya jahannamu na paradiso. Inasadikika kwamba ni walio waaminifu tu wenye uwezo wakuvuka na kuingia mbiguni. Lakini hata mtume wa Uislamu hana uhakika kama ataweza kulivuka daraja hilo.

Unaona kwamba chini ya uongozi wa mungu wa Uislamu, waovu wanapokea wanachostahili. Walifanya yote waliyo yataka duniani wakijua wataishia jahannamu na sasa Mwenyezi Mungu anawapeleka jahannamu. Lakini maskini! wale wafuasi waliyo kuwa waadilifu walimwamini Mwenyezi Mungu, walijinyima mambo mengi ya duniani kwa matumaini Mwenyezi Mungu atawapeleka mbinguni, lakini sasa nao wamekuwa na mwisho sawa na waovu. Lo!

Kwa hiyo ujumbe wa Qur'ani upo wazi kuhusu watu waovu; haina habari njema kwao kwani watabaki jahannamu. Lakini pia haina habari njema kwa wenye haki kwani nao wanaweza kubaki jahannamu. Hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu ni adui wa wasio fuata Uislamu. Na kulingana na mistari hii inaonekana si rafiki pia hata kwa waislamu wake wenye haki. Anajiita 'mungu wa rehema" mwanzoni mwa kila sura ya Qur'ani ila anawatesa waislamu wake wenye haki kwa kuwapitisha jahannamu kabla ya hukumu.

Kama kweli ni mungu mwenye rehema kwa nini awatendee sawa wenye haki na waovu? Je hii ndiyo tafsiri ya rehema kulingana na Qur'ani? Kama huruma za Mwenyezi Mungu haziwezi kuwalinda wenye haki na taabu za jahannamu, kwa nini Mwenyezi Mungu asiitwe mwongo na mdhalimu? Huu ni mfano halisi wa uwongozi usio sahihi wa Mwenyezi Mungu.

Je, Mungu wa kweli asingeona vyema kuwapeleka wenye haki moja kwa moja mbinguni. Ndiyo. Mungu wa kweli anaweza. Mungu wa Biblia hufanya hivyo. Mungu wa Uislamnu hafanyi hivyo kwa sababu si mungu wa kweli. Haijalishi jinsi gani mwislamu atakuwa mwenye haki, mungu wake atampeleka jahannamu kwanza sehemu yenye taabu na kutisha kwa hukumu. Na kuna uwezekano atabaki huko milele.

**Qur'ani inasema njia ya paradiso haijulikani.**

Sura ya Luqman (31) aya ya 34 inasema: ...Hakika kuijua Saa kuko kwa Mwenyezi Mungu Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho...

Kwa maneno mengine ni kwamba mungu wa Uislamu anajua ni wenye haki wepi watabaki jahannamu lakini hafunui kwa yeyote siri hio hata Muhammad. Amewaacha waadilifu wake wote bila uhakika.

Je haushangazwi na uongozi wa mungu wa Uislamu? Anakusihi umfuate lakini hujui ni wapi anakupeleka. Unawezaje kumfuata mtu anaye ficha malengo yake na hakwambii wapi anakupeleka? Na kama sivyo, sasa basi ni kwa nini umfuate mungu mwenye sifa hizo? Mungu wa Uislamu anamwacha hata Muhammad kwenye mashaka.

Kwenye sura ya Al Ahghaf (46) aya ya 9 Muhammad anasema: Wala sijui nitakavyo fanywa wala nyinyi.

Unaona kwamba hata mtume wa Uislamu anamfuata mungu amabae malengo yake hayajulikani na ni kwasababu hii hana uhakika wa wokovu wake. Je, si huzuni sana ya kwamba iwe Muhammad ama mwenye haki yoyote mwislamu hawana uhakika na wapi wanakoelekea, lakini bado wanawalazimisha na wengine pia wawafuate kuelekea kusikojulikana? Waliwachinja wengi kwa kutokuwafuata.

Chakusikitisha zaidi, Muhammad anaita kutokua na uhakika wa uongozi wa mungu ni habari njema. Katika sura ya Al A'raf (7) aya ya 188 Muhammad anasema: Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ninge jizidishia mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini.

Katika aya hii Muhammad anataka kusema ya kwamba badala ya yeye kukusanya haki ya Mungu , alikusanya uovu unao tokana na shetani kwasababu Mungu hakumpa akili na hekima vya kutosha. Mwishoni mwa aya hii imeandikwa Muhammad ni mtoa onyo na mtangaza habari njema. Anauita ni kukosa ufahamu, hekima, matendo mema na uwepo wa uovu kama habari njema. Je, waweza kuamini hili? Je ukosefu wa ufahamu ni jambo jema? Utaziitaje

habari njema kama zimetoka kwa mwovu? Utaitaje, kwenda jahannamu jambo jema? Utaitaje kutokuwa na uhakika wa kwenda mbinguni habari njema? Je unaita kushindwa kwa waislamu wenye haki na Mwenyezi Mungu habari njema? Utawezaje kweli kumwita Mwenyezi Mungu kiongozi mzuri wa kiroho kama amesababisha nabii wake pamoja na wafuasi wake kutokuwa na uhakika wa siku za mbeleni?

Natamani mngepata muda wa kusoma injili na kujionea jinsi gani Mungu anawatunza watu wake. Anafundisha ya kuwa hakuna kitu kizuri kama kuwa na uhakika maishani mwako.

**Hatima ya Muhammad dhidi ya. hatima ya manabii wa Biblia.**

Hebu tuone tofauti ya hatima ya Muhammad na hatima ya manabii wa Biblia.

Katika kitabu cha Kutoka sura ya 32 aya ya 31 – 32 inasema jina la Musa limeandikwa katika kitabu cha milele na mahali pake ni mbinguni. Kwa hiyo wakati Musa anaishi kati ya wafuasi wake alijua kabisa ameokolewa, na mungu ame mtayarishia nafasi yake mbinguni. Nabii Danieli katika kitabu chake Sura ya 12 aya ya kwanza inasema majina ya wafuasi wa Mungu yameandikwa katika kitabu cha uzima wa milele. Nabii wa Biblia anasema wafuasi wa Mungu wa kweli wasiwe

na hofu wala kuogopa kwa sababu makao yao ya milele ni mbinguni.

Majina ya Musa, Danieli, manabii wengine na wafuasi wa Mungu yameandikwa kwenye kitabu cha uzima. Lakini Qur'ani inasema hakuna jina la Muhammad wala la mwislamu yeyote lililoandikwa katika kitabu cha uzima. Hakuna mwenye uhakika na hatima yake kwenye Uislamu, Je unaona utofauti?

## Yesu Kristo anawaongoza wafuasi wake na kuwapa uhakika

Injili inatufundisha kwamba pale tu unapomwamini Yesu, uhusiano wako na jahannamu unafutika na unalindwa na maovu.  Uhakika wa wokovu ndiyo kiini cha ujumbe wa injili kwa maisha ya duniani, kwa sababu Mungu wa kweli hawaachi watu kwenye mashaka.

Yesu alisema katika injili ya Yohana sura ya 5 aya 24; amini amini nawambia yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yule aliyenipeleka yuna uzima wa milele. Wala haingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. (MKJV)

Je, si ajabu sana kwamba viongozi wa Uislamu wanasema Torati na injili vyenye uhakika vitabu

vyenye uongo bali waita Qur'ani kitabu kikamilifu hata kama hakina uhakika.

**Mwenyezi Mungu anawapotosha watu**

Hebu nikupe vitu vingine vya kushangaza kuhusu sifa za uongozi za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu sio tu kiongozi mbaya bali pia anawapotosha watu, kwa mujibu wa Qur'ani Sura ya Ibrahim(14) aya ya 4 ina sema Mwenyezi Mungu humuacha akapotea amtakaye.

Hebu fikiria kibao kina ning'inia kwenye kifua cha kiongozi kimeandikwa "napotosha watu" je utamwamini huyo mtu kukuongoza? Kama sivyo, basi ni vyema pia usimwamini Mwenyezi Mungu anayepotosha watu.

Hebu nikupe mfano wa kusikitisha kuhusu uongozi wa Mwenyezi Mungu. Sura ya An Nisa (4) aya ya 88 inasema: Ee Muhammad unayepotoshwa na Mwenyezi Mungu, kamwe hautaweza kuipata njia.

Katika sura hii ya Qur'ani inasema mungu anapotosha kiasi kwamba hata kutafakari kwa Muhammad hakuna maana. Kwanini umfuate mtu anayekupotosha kiasi kwamba hakuna njia ya kuweza kurudi. Unaona kuwa uko pamoja na mungu wa kiislamu amabye yeye mwenyewe ni kikwazo cha maisha yako ya kiroho, na hakuna atakaye kuokoa ukimwamini.

Ni kwa sababu hii niliacha Uislamu. Niligundua mungu wa Uislamu sio tu hana uongozi mzuri bali pia ni tishio katika maisha yangu ya kiroho. Kwa hiyo kubaki mwislamu ingekua hasara ya kiroho kwangu.

**Katika Biblia Mungu ni mchungaji mwema.**

Sasa ngoja nikupe mifano kutoka katika Biblia. Utashangaa moyo wa upendo Mungu alionao kwa wafuasi wake na utaelewa kwanini niliamua kumfuata Mungu wa Ukristo. Ona mambo anayoyafanya Mungu wa Biblia kwa wafuasi wake.

Yakobo katika Torati anasema (Mwanzo 48:15); Mungu amekuwa mchungaji wangu maisha yangu yote hadi na sasa. (ESV)

Nabii Daudi katika Zaburi sura ya 23 aya ya 1 na 3 inasema; bwana ni mchungaji wangu ...hunihuisha nafsi yangu nguvu mpya. Huniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.(ESV)

Nabii Isaya anasema: atalilisha kundi lake kama mchungaji atawakusanya wanakondoo mikononi mwake, nakuwachukua kifuani mwake, nao wanyonyeshao atawaongoza polepole. (Isaya 40:11 MKJV)

Nabii Ezekieli asema: mimi mwenyewe nitawalisha kondoo zangu nami nitawalaza asema bwana Mungu. (Ezekieli 34:15 ESV)

Ona Yesu anavyosema: mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema hutoa maisha yake kwa ajili ya kondoo wake (Yohana 10: 11)

Moyo wa Mungu wa Biblia ni tofauti sana na moyo wa mungu wa Qura'ni

## Mungu wa Uislamu hana msimamo

Ngoja nikupe mifano zaidi jinsi gani mungu wa Uislamu hawezi kuwa kiongozi mzuri na mkweli.

Mwanzoni mungu wa Uislamu aliamini kwamba dini isilazimishwe

Muhammad alipokuwa Makka na hakuwa na wafuasi wengi wala ushawishi mkubwa wa kisiasa mungu wake alisema katika Sura ya Al Bagharah (2) aya ya 256: dini hailazimishwi. Na katika Sura Al Kahf (18) aya ya 29 alimwabia Muhammad : Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae

Lakini mungu wa Uislamu alibadilisha mawazo baadaye. Muhammad alipopata wafuasi wengi na

kuanzisha jeshi mungu wake alimwambia katika Sura ya Al Tawbah (9) aya ya 33 kuifanya dini ya kiislamu ishinde na kutawala dini zingine zote.

Katika sura ya Al Anfal (8) aya ya 12 Mwenyezi Mungu anasema; Nitatia woga katika nyoyo za walio kufuru. Basi wapigeni juu ya shingo na wapigeni kwenye kila ncha za vidole

Kwa mara nyingine Muhammad alipoishiwa na nguvu mungu wake alisema hivi katika sura ya Al Bagharah (2) aya ya 62: Hakika Walio amini, na Wayahudi na Wakristo, na Wasabai; yeyote atakaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na akatenda mema basi watapata malipwa yao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.Lakini katika sura ya Al Bayyina (98) aya ya 6 inasema: wakristo na wayahudi na waabudu miungu ni wabaya kuliko viumbe vyote na watakwenda jahannamu.

Unaona mungu wa Uislamu anachokifanya? Mwazoni anasema wakristo na wayahudi wataenda paradiso kama watafuata imani zao. Lakini badaye anasema wataenda jahannamu kama hawatafuata Uislamu. Je, mungu wa kweli huonyesha mkanganyiko wa namna hii.? Mungu aliyechanganyikiwa awezaje kuwaongoza watu katika njia iliyo sahihi?

Hata ndani ya sura moja mungu wa Uislamu huzungumza maneno yanayo pishana. Sura ya Al-e Imram (3) aya ya 55 inasema: nitawaweka wakristo juu ya wasiyo mwamini Yesu, mpaka siku ya ufufuo. Lakini aya ya 19 na 85 ya sura hiyo hiyo inasema: dini sahihi ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. Hakuna dini nyingine itakayokubalika isipokuwa Uislamu.

Sijambo la kushangaza kwamba katika sura moja, Mwenyezi Mungu anasema kumfuata Kristo ni kipaumbele chake cha kwanza cha kiroho, lakini anajisahau na kusema tena katika sura hiyo hiyo kwamba kila mtu lazima afuate Uislamu?

Katika sura ya Al Bagharah (2) aya ya 65 mungu wa Uislamu anasema kwamba alikasirikia wayahudi waliyovunja sheria za Musa kuhusu sabato au jumamosi na aliwageuza kuwa nyani. Lakini kwa upande mwingine anawaomba waislamu kuwashawishi wayahudi kuiacha sabato ili wawe waislamu na kufuata sala za ijumaa.

Je hili si jambo la ajabu? Upande mmoja mungu wa Uislamu anawazuia wayahudi wasiiache dini yao, na upande wa pili anawaua kama wasipoiacha sabato na kuwa waislamu!

Je, Mungu mwaminifu na ajuaye yote hawezi kusema dini nyingine ni nzuri lakini abadilishe mawazo yake

siku inayofuata na kusema ni mbaya na wafuasi wake wauawe? Hapana kabisa. Mungu wa Uislamu alifanya hivyo kwa sababu si mungu na kiongozi wa kweli

**Mwenyezi Mungu pia amewapotosha waislamu kuhusu Yesu**

Sura ya Al-e Imran (3) katika aya ya 55 inasema; Ewe Isa! Mimi nitakufisha, na nitakunyanyua kwangu, na nitakutakasa na wale walio kufuru. Lakini katika Sura ya An Nisa(4) aya  ya 157 na 158 inasema ya kwamba wayahudi hawakumsulubisha na kumuua Yesu bali Mungu alimchukua kwake. Pia katika sura ya Al Maeda (5) aya ya 117 inasema Yesu alimwambia Mungu: ...nilishuhudia matendo ya wayahudi kipindi nilipoishi kati yao; lakini kwa kuwa wewe Mungu ulinisalimisha kwa kifo (فِلَمّاتَوَفّيتَنى = Falamma Tavaffaytani) wewe mwenyewe umewaona... Na katika sura ya Mariam(19) aya  ya 33 inasema Yesu alisema: Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa, na siku nitakayo kufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai

Kwa hiyo unaona jinsi gani mungu wa Uislamu anawapotosha waislamu kuhusu Yesu. Upande mmoja anasema Yesu alikufa na upande w a pili Yesu hakufa. Uongozi wa Mwenyezi Mungu unachanganya na si wakuaminika.

Hebu nikupe mifano migine miwili ya ujumbe wa Mwenyezi Mungu unaopingana

Katika sura ya Al Anbiya (21) aya ya 34 na 35 Mwenyezi Mungu anamwambia Mohammad ya kuwa hakumpa mtu yeyote uzima wa milele kabla ya Muhammad. Kila nafsi itaonja mauti... imeandikwa katika sura ya Al-e Imran (3) aya ya 185 kwamba kila nafsi itaonja mauti.

Kulingana na aya hizi kila mtu kabla ya Muhammad kuanzia Musa, Yesu na wengine wote walikufa na hata Muhammad atakufa.

Je Mungu wa Uislamu anajua kweli anachokifanya? Anathibitisha katika sura za Al-e Imran, Al Maida, Mariam na Al Anbiya ya kwamba Yesu alikufa na lazima kila mtu atakufa, lakini katika sura ya An Nisa anakana kuhusu kifo cha Yesu. Hii inamaanisha mungu wa Uislamu hana uhakika na anacho taka kusema juu ya maisha ya Yesu. Ina changanya sana! Mungu wa kweli anaweza kuchanganyikiwa? Hapana haiwezekani kabisa.

Mungu wa Uislamu anasema Muhammad alikufa lakini Yesu yuko hai mbinguni. Yesu yuko hai na Muhammad amekufa! Kwa nini Mwenyezi Mungu hakuwasihi waislamu wamfuate Yesu anayeishi milele lakini alisihi wamfuate Mohammad aliyekufa milele?

Nini kilicho fanya Qur'ani inamtambulisha kama anayewapotosha watu na kuwapeleka wafuasi wenye haki jahannamu?

### Matokeo ya upagani

Ni wapagani tu wanaoamini miungu yao inaweza kufanya vitu kama hivyo. Muhammad aliharibu sanamu za kipagani bila ya kujua kuwa picha ya Mungu aliyokuwanayo akilini ilikuwa ni ya mungu wa kipagani, kwamba ilitakiwa kwanza aitoe picha hio kichwani na moyoni mwake.

Vitu hivi visizyo vya kimaadili sio sifa za Mungu ambaye Yesu alimdhihirisha. Mungu wa kweli ni kiongozi mzuri, ana upendo na hutoa uhakika wa kwenda mbinguni kwa wafuasi wake. Hakika unahitaji kumfuata Yesu.

### Wakati wa kutafakari 7

1. Mungu anatakiwa kuwa kiongozi bora. Ni sifa gani za kiongozi bora?
2. Je, unajisikiaje ukipotoshwa na mtu? je itakuwaje kama ni mungu ndiye amekupotosha?
3. Kwa nini mungu wa Uislamu hawezi kuwa kiongozi mzuri ?
4. Je tunahitaji kiongozi mkweli wa kiroho katika maisha yetu duniani? Kwa nini?

5. Je tutaweza kwenda mbinguni kama hatutamfuata Mungu wa kweli?
6. Kuna umuhimu gani wa kumfuata kiongozi mzuri?

# Je! Una Amani na Mungu Kupitia Uislam?

Je, Uislamu una uwezo wa kuleta amani kati yako na Mungu? Je! Unaweza kusema, "Mimi nina uhakika asilimia mia moja kuwa upande wa Mungu, nitakwenda mbinguni kwa Mungu na sitakwenda jahannamu katika siku zijazo"?

Hivi ndivyo imani ya kweli inachoweza kukufanyia. Inaweka mikono yako mikononi mwa Mungu na inathibitisha maisha yako baada ya maisha ya hapa duniani.

**Je, Uislamu ni imani ya kweli ya kuleta amani?**

Je! Uislamu umeweza kuweka mikono yako mikononi mwa Mungu hadi sasa na kukuambia kuwa uhusiano wako na Mungu ni wa milele? Je! Unaweza kusema kwamba kwa sababu ya Uislamu una imani na amani ndani ya moyo wako sasa na huna wasiwasi juu ya milele yako? Je, unajua Muislamu yeyote katika historia ya Uislamu ambaye alikuwa na uwezo wa kusema, "Mimi niko huru sasa, nimeokolewa na mimi nimepatanishwa kweli na Mungu na nitakuwa pamoja naye milele."

Wewe na mimi tunajua kwamba hata Muhammad hakuweza kuthibitisha umoja huo na Mungu ambao

unaweza kudumu milele na kumpa uhakika wa milele. Alisema kwamba hakujua ambacho kingetokea kwake baada ya kifo.

Mungu hana haja na umoja wa mdomo tu au wa juu juu. Mungu ni mkamilifu na anataka umoja mkamilifu. Kwa sababu, ni umoja mkamilifu tu unaweza kuleta amani ya milele kati ya Mungu na watu wake, hasa wale wanaodai kuwa manabii Wake. Kwa hiyo, wakati nabii anasema kwamba hajui juu ya maisha yake baada ya maisha ya hapa duniani, inamaanisha kuwa hana umoja na Mungu na hajui umoja wa kweli na amani na Mungu ni nini.

Hapa ndipo nilipokuwa na hofu sana juu ya maisha yangu ya kiroho wakati nilipokuwa mwislamu. Nilijiambia mwenyewe kwamba nabii wa Uislamu alikuwa Mwislamu mwadilifu. Alikuwa namba moja katika kufuata maagizo ya Uislamu na kuwa mwaminifu kwa mungu wake. Licha ya matendo yake yote mema, alisema kuwa hatimaye haijulikani kwake, ikiwa angekwenda mbinguni au angeipoteza nafasi yake.

Niligundua kutakuwa na kitu si sawa katika Uislamu, vinginevyo, pasingekuwapo na ukosefu wa uhakika wowote ambao ungewatisha Waislamu. Uislamu inamaanisha "kujisalimisha" kwa Kiarabu. Muislamu

inamaanisha "yule aliyesalimishwa kwa Mungu." Je, si kujisalimisha huku ndiko kungefaa kuunda uhakika kwa Waislamu kuhusu maisha yao ya baadaye? Ikiwa silo, basi ni faida gani ya kujisalimisha kwa mungu wa Uislamu? Nilijiuliza, "Kwa nini niwaite wengine kujisalimisha katika Uislamu na kuwa wabaya kama mimi? Kwa nini mimi nifuate Uislamu na kuruhusu kutokuwa na uhakika kunitese kila siku? "Nilikuwa na bahati wakati maswali haya yalipoanza kuwa sehemu ya maisha yangu ya kila siku.

Je! Umewahi kupata nafasi ya kujiuliza maswali haya katika akili yako na kupata jibu lolote? Ni muhimu kwako kupata njia inayokuokoa kutoka kwa aina zote za wasiwasi, inayokupatanisha na Mungu na kukupa amani ya milele ndani ya moyo wako. Mungu wa kweli anatamani wewe umruhusu kuingia katika maisha yako ya hapa duniani na kukupa uhakika wa milele. Imani yoyote inayodai kuwa ni kutoka kwa Mungu lazima iwe nuru ya hamu ya Mungu na iweze kukupatanisha naye.

## Hata wapagani nao hawana amani kuhusu hatma ya maisha yao

Uislamu haujaweza kukupa uhakika kuhusu maisha yako ya baadaye. Unahitaji kufuata imani tofauti ambayo inaweza kukuunganisha na Mungu na kukupa uhakika kamili. Uislamu hauna tofauti na upagani.

Wapagani wanasema kama Waislamu na wanasema kuwa hawajui nini kitatokea kwao baada ya kufa. Wapagani pia wanaogopa kuhusu maisha yao ya baadaye kama vile Waislamu.

Je! Ni mungu wa aina gani mungu wa Uislamu ambaye anaitwa mwenye huruma lakini hawezi kuharakisha kusaidia Waislamu kwa hofu yao ya baadaye? Waislamu wanaomba mara tano kwa siku, wanafunga mwezi mzima kila mwaka na kufanya mambo mengine yote wanayoombwa kufanya, lakini bado wanaogopa na wana hofu kama wataweza kuitimiza safari yao ya kiroho ya kwenda paradiso au kuishia katika Jahannamu. Huruma ina maana kuwa na utu, na kumjali mtu kwa upendo. Ikiwa unaomba na kulia kwa mungu wako kila siku ili akuelekeze kwenye njia sahihi na kukuondolea hofu, kwa nini haiondoi hofu yako na kujaza moyo wako furaha na faraja? Kuna kitu si sawa hapa. Labda Mungu si mwenye huruma au Waislamu hawaifuati njia sahihi. Lakini kila mtu wa dini duniani anaamini kwamba Mungu ndiye chanzo cha huruma. Ikiwa ndivyo, basi Mungu hajawahi kuchelewesha huruma yake kwa wale wanaomlilia. Kwa hiyo, Uislamu si dini ya kweli kwani inachelewesha huduma ya Mungu kwa watu.

Ukifuata imani ya kweli, Mungu ataujaza moyo wako ujasiri, amani na furaha. Ujasiri kwa sababu Mungu ni

Mungu mwenye kujua yote na atakuonyesha hatma yako; amani kwa sababu utakuwa mikononi mwake, mahali salama sana na hakuna chochote kitakachoweza kuwatenganisha na upendo na utunzaji wake; furaha kwa sababu utashinda hofu milele. Hakuna chochote kati ya hivi kwenye Uislamu.

## Uislamu si dini sahihi ya kuleta amani

Yote mliyoyasikia tangu utoto hadi sasa ni kwamba Uislamu ni dini ya mwisho na kamili na Mungu yuko kwa Waislamu. Ingawa hakuna sababu yoyote ya msingi katika Uislamu iliyo tolewa kwa mojawapo ya madai hayo.

Unaposema kwamba Mungu yu pamoja na wewe lakini huna uhakika kuhusu maisha yako baada ya kifo, basi unaweza kuona kwamba Uislamu unakuacha bila matumaini kuhusu maisha yako ya baadaye. Dini isiyo na matumaini haipaswi kuitwa kamili. Kwa sababu kuwa pamoja na Mungu inamaanisha kuwa wewe huna hofu ya kwenda kuzimu na una uhakika wa asilimia mia moja ya kuwa kama uko na Mungu duniani, utakuwa pia pamoja na Mungu mbinguni baada ya kufa. Mungu ni Mungu wa amani kwa ulimwengu huu na ulimwengu wa baadaye. Akiwa pamoja nawe, anakupa ujasiri wa kuwa pamoja naye katika ulimwengu wote. Ikiwa mungu wa Uislamu au mungu

mwingine yeyote hakupi ujasiri wa maisha ya baadaye, hawezi kuwa Mungu wa kweli.

Ujumbe wa Uislamu unakinzana. Inasemekana kwamba Waislamu wako pamoja na Mungu katika maisha yao duniani, lakini haijulikani kama watakuwa pamoja na Mungu katika maisha ya baadaye au wataenda kuzimu.

**Utii kwa Mwenyezi Mungu hauna mwisho wa amani.**

Umoja na amani na Mungu duniani lazima upelekee umoja wa milele na amani na Mungu katika maisha ya baadaye na kutoa uhakika kamili kwa watu. Hapa ndipo tofauti kubwa kati ya Uislamu na imani ya kikristo unajionyesha. Injili ya Yesu Kristo inasema, ikiwa u pamoja na Mungu sasa, utakuwa pamoja Naye milele. Lakini Qur'ani inasema, ikiwa u pamoja na Mungu sasa, haijulikani kama utakuwa pamoja na Mungu baada ya maisha au kwenda kuzimu.

Unaona umoja huo na Mungu ni umoja wa kweli katika Injili. Inaanzisha urafiki kati yenu na Mungu kwa namna ambayo inaendelea milele. urafiki halisi lazima uwe wa kina , wa muda mrefu na wakuaminika. Urafiki na mungu wa kiislamu sio wa kina. Ni hofu ambayo inaharibu uaminifu, amani na faraja.

Kwa hiyo tunaweza kuona kuwa utii kwa Mungu katika Uislamu sio kweli bali ni bandia. Kama ingekuwa kujisalimisha kwa ukweli, kusingeunda utata na hofu katika Waislamu kuhusu maisha yao baada ya kifo, bali kungewapa kujiamini milele ya kwamba wako pamoja na Mungu.

Kwa mujibu wa Injili ya Yesu Kristo, ikiwa umejisalimisha kwa Mungu na ukaungana naye duniani, kamwe hawezi kuacha agano lake, lakini hutimiza agano lake milele na huujaza moyo wako uhakika. Kwa hiyo, umoja na Mungu katika maisha yetu duniani utatupeleka mbinguni ili tuwe na Mungu milele.

Kwa hiyo, mtu anapokuuliza ikiwa una amani na Mungu kupitia Uislam, jibu lako la kweli linapaswa kuwa "hapana" kwa vile Uislamu haukuhakikishii kuhusu maisha yako ya baadaye. Kisha unahitaji kumkimbilia mtu huyo na kumwomba akupe ushauri juu ya nini cha kufanya ili kuwa na amani na Mungu na kuokolewa kutokana na hofu yako kuhusu hatma yako. Utaona mwanga wa mbingu ndani ya mtu huyo ikiwa yeye ni mfuasi wa Yesu Kristo. Utajifunza jinsi ya kuungana kwa ukweli na Mungu katika kila nyanja ya maisha yako na kuwa na amani naye. Utajifunza pia jinsi ya kuwa na amani na wengine.

**Umoja ni chanzo cha amani utakupa amani ya milele.**

Mungu ndiye chanzo cha amani. Umoja ni chanzo cha amani utaleta amani katika maisha yako mwenyewe. Kisha utakuwa na amani, mleta amani na utakuwa na amani na wengine pia. Kwa maneno mengine, ikiwa huna amani na Mungu wa kweli, huwezi kuwa na amani halisi na watu, ama katika familia yako mwenyewe au nje. Unapoungana na Mungu na kuwa na amani na Mungu, huruma yake inakuwa sababu inayohamasisha uhusiano wako na wengine; Kwa hiyo unakuwa mleta amani badala ya kuwachukia watu. Unaweza kusema basi, "Ikiwa Mungu ni mwenye huruma kwangu wakati mimi ni mwenye dhambi, mimi pia ni lazima nijaribu kuwa na huruma kwa wengine ambao ni kama mimi."

Tabia hizi za huruma, za upendo na za amani ziko katika imani ya Yesu Kristo si kwa Uislamu wa Muhammad. Yesu hachukii, wala kulaani au kuua wadhambi lakini daima huwafikia kwa huruma na hii inaruhusu wema kufanya kazi badala ya chuki. Kwa Yesu Kristo, upendo, wema na amani vinaweza kubadilisha watu kwa wema, na sio chuki na ukatili. Hakuna mstari hata mmoja katika Injili nzima ya Yesu Kristo unaofundisha chuki dhidi ya wenye dhambi au

watu wanaokupinga. Injili haiwafundishi wafuasi wake kuwaua wengine.

Yesu alinibadilisha mimi na mamilioni ya wengine kwa njia ya upendo wake wa ajabu na wema. Alifungua macho yetu kuona kwamba chuki haiharibu tu maisha ya wengine bali pia inaleta uharibifu wa amani katika maisha yetu na familia zetu.

Kwa hiyo, tunaweza kuona jinsi gani umoja wa kweli na amani na Mungu hutufanya watulivu na kutuongoza katika njia ya kuungana na wengine kupitia upendo na wema na kuishi kwa amani nao. Pia tunaweza kuelewa sasa kwa nini Uislamu haukuweza kuleta amani; kwa sababu, udhalimu katika Uislamu ni mwingi zaidi kuliko wema na msamaha.

Ujumbe wangu kwako ni huu: Unahitaji kuwa na amani na Mungu sasa, na hiyo inawezekana tu kwa kupitia Yesu Kristo. Pia unahitaji amani na familia yako na wengine. Hii inawezekana tu kwa kupitia Yesu Kristo.

Je! Unataka kuwa na amani na Mungu, katika familia yako na katika uhusiano wako na wengine? Ikiwa una nia thabiti, unahitaji uwe na dhamiri yako ya kuyazingatia malengo yaliyothibitishwa ambayo nimekuwa nikizungumza nawe.

**Amani ya kweli haitawezekana bila ya uongozi wa Mfalme wa Amani**

Nani mfalme wa amani? Je, unafikiria ni nani awe Mfalme wa Amani?

*Ana moyo wa Mungu*

Mfalme wa amani lazima awe mtu ambaye ana moyo wa Mungu ili aweze kuwafikia watu kama Mungu anavyofanya.

*Anaheshimu haki za wengine*

Mfalme wa amani hafanyi ubaguzi bali anaamini katika haki ya kila mtu, bila kujali kama ni marafiki au la, kwa kuwa Mungu ametuumba sote na uhuru wa kuchagua.

*Yeye ni mwenye ukarimu*

Kwa kuwa Mungu ni mwenye ukarimu na ameumba ulimwengu kwa wote, kwa kuwa yeye huleta mvua zake kwa wote, mfalme wa amani pia lazima awe mkarimu kama Mungu ili aweze kushinda mioyo ya adui zake kwa kupitia ukarimu.

*Yeye kamwe hakimbilii kuanzisha vita.*

Pia, Mfalme wa amani hakimbilii kamwe kuanzisha vita, kwa sababu lengo lake ni kuwaleta watu kwa njia ya maarifa na ufahamu ili kuleta amani kati yao.

Ukisoma na kulinganisha Injili kutoka kwa Mkristo, na Qur'ani, basi utaelewa kwamba mfalme wa amani ni Yesu.

Miaka mia saba kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, Nabii Isaya alitabiri juu yake hivi: Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa juu ya bega lake; na jina lake ataitwa wa ajabu, Mshauri, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani. Kwa kuzaliwa kwa Yesu Kristo unabii huu ulitimizwa: Injili inasema katika kitabu cha Wakolosai sura ya 1 mstari wa 19 na 20 kwamba utimilifu wote ulikaa ndani ya Yesu Kristo ili kuunganisha vitu vyote mbinguni na duniani kwa Mungu.

Yesu Kristo ndiye Mfalme wa amani. Anaweza kuunganisha yote mbinguni na kwa kila mmoja. Mfuate Yesu ili uweze kuungana na Mungu na uwe na amani ya milele pamoja naye.

## Wakati wa kutafakari 8

1. Ina maana gani kuwa na amani na Mungu?
2. Kuna umuhimu gani wa kuwa na amani na Mungu na ni kwa njia ipi inaathiri maisha yetu ya kijamii?
3. Mungu anafanya jukumu gani katika kuanzishwa kwa amani?
4. Tunahitaji kufanya nini ikiwa imani yetu haijatuunganisha na Mungu?
5. Je! Kuna sababu yoyote kwamba imani katika Kristo inakuunganisha na Mungu? Ikiwa ndivyo, unapaswa kufanya nini basi?

# Je! Qur'ani ni Neno la Mungu wa Kweli?

## Unajuaje kama Kitabu kimetoka kwa Mungu au La?

Tunahitaji kujua kama maneno ya kitabu hicho yanafanana na sifa za Mungu wa kweli au la. Tunahitaji kutathmini maneno ya kitabu hicho kutoka kila pembe. Hiki ndicho tutakachokifanya kwa maneno ya Qur'ani, tutayatathmini kwa ukamilifu ili kila mtu, mwenye elimu au asiye na elimu, atambue kwamba Qur'ani haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu wa kweli.

## Je, Mungu wa Uislamu huzungumza Maneno?

Tathmini ya kwanza ni kuona kama mungu wa Qura'ni anaweza kusema maneno au la. Ikiwa hawezi, basi hakuna mtu anayeweza kuthibitisha kuwa Qur'ani inatoka kwa Mungu.

Mungu mwenye sifa ya utu tu ndiye anaweza kuwa na maneno ya kiutu ambayo yanahusiana na wanadamu kama viumbe vyenye utu. Mungu wa Uislamu ni mungu asiye na uhusiano wa kibinafsi, kwa hivyo hawezi kuwa na maneno ya kibinafsi na ya kirafiki ili awe na uhusiano binafsi. Hii ina maana kwamba mungu wa Muhammad, kinyume na Mungu wa Musa na manabii wengine, hakuweza kuwa na mawasiliano

ya kibinafsi naye, na hakuwahi kusikia sauti au neno kutoka kwa mungu wake. Kwa hivyo, Qur'ani haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu.

Biblia ni Neno la Mungu. Kwa nini? Kwa sababu Mungu wa Biblia ni wa kibinafsi na ana uhusiano, na Yeye anajieleza kwa maneno moja kwa moja kwa watu Wake. Mungu aliongea na Musa na manabii wote wa kibiblia binafsi, na walisikia maneno ya Mungu kutoka kwake binafsi na kwa masikio yao wenyewe. Uzoefu binafsi wa manabii hao pamoja na Mungu ulikusanywa pamoja kama Biblia na kama nuru kwa maisha ya watu. Matokeo yake, Mungu wa kweli lazima awe binafsi ili aweze kujielezea mwenyewe kwa maneno na ili kuwe na kitabu. Mungu wa Uislamu sio binafsi na kwa hiyo hawezi kuwa na kitabu. Qura'ni haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu wa kweli.

**Je! Mungu wa Uislam anatoa Uhakika?**

Tathmini ya pili ni kuona kama mungu wa Qura'ni anatoa uhakika wa wokovu. Ikiwa sivyo, basi Qur'ani haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu wa kweli.

Qur'ani katika Sura za Luqman (31) na Al Ahqaf (46) inasema wazi kwamba hakuna mtu anayejua nini kitakachotendeka kwake baadaye. Sio tu kwamba Qur'ani haitoi uhakika huo, pia inasema katika Sura

Maryam (19) kwamba Waislamu wote wenye haki watapelekwa jahannamu kwanza kwa hukumu.

Neno la Mungu aliye hai lazima liwape watu wake uzima wa milele, kuwaweka mbali kabisa na jahannamu; Kwa kuwa Qur'ani haiwezi kuwaweka wafuasi wake mbali na jahannamu, basi sio neno la Mungu.

Je! Mungu wa kweli atawapeleka wafuasi wake jahannamu hata kwa muda mfupi? Hapana kabisa. Qur'ani inasema hivyo, kwa sababu sio neno la Mungu wa kweli.

Kitabu na maneno ya Mungu wa kweli lazima yawe na uwezo wa kujenga uhusiano wa milele kati ya Mungu na wafuasi wake, lakini Qur'ani haina mamlaka hiyo.

Kitabu cha Mungu wa kweli kinakupa uhakika kwamba sasa umeunganishwa na Mungu na umeokolewa milele; Uhusiano wako na Shetani na Jahannamu unafutwa milele; baada ya kufa, utapelekwa moja kwa moja mbinguni kwenye ushirika wa milele na Mungu.

Qur'ani haikuweza kumpa Muhammad, kiongozi mkuu wa Uislamu na mtu aliyependwa zaidi na Allah, amani na uhakika juu ya hatma yake. Kwa sababu hii, alikufa bila imani ya wokovu wake. Je! Mungu wa kweli angeweza kumkatisha tamaa mpendwa wake? Hakika

sivyo. Tatizo siyo Mungu; tatizo ni Qur'ani. Haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu.

## Je! Qur'ani inazungumzia Mungu wa maadili?

Tathmini ya tatu ni kuona kama mungu wa Qur'ani ni mungu wa maadili au la.

*Qur'ani inasema kwamba Mungu ni mdanganyifu*

Sura Al-Imran (3) aya ya 54 na Sura Al Anfal (8) mstari wa 30 zinasema kuwa Mungu ndiye mdanganyifu kuliko wote; Sura Yunus (10) mstari wa 21 unasema kwamba Mungu ni mwepesi kudanganya; na Sura Al-A'raf (7) mstari 99 unasema kwamba hakuna mtu anayeweza kuepuka udanganyifu wake.

Kweli? Je! Qur'ani ni sahihi, kumwita Mungu wa kweli kuwa mdanganyifu? Hakika si sahihi. Mungu mtakatifu, mwenye haki na huruma hawezi kuwa mdanganyifu. Qur'ani ina tatizo la msingi kwa kumwonyesha Mungu kama mwovu; haiwezi kuwa ya Mungu wa kweli.

*Qur'ani inasema kwamba Mungu ni mshirika na wahaini.*

Sura Al Isra (17) katika mstari wa 16 inasema kuwa Mungu anawahamasisha watu kufanya mambo ya uasherati ili aweze kuwa na sababu ya kuwaangamiza.

Je, Mungu mwenye upendo na huruma ya kweli anaweza kubadili asili yake na kutenda mambo kama ya Shetani? la hasha! Maneno kama hayo kutoka kwenye Qur'ani ni ushahidi wazi kwamba haiwezi kuwa neno la Mungu wa kweli.

*Qur'ani inasema kwamba Mungu anadanganya ili kuwanasa wale wanaompinga*

Sura Al-A'raf (7) katika mstari wa 182 na 183 na pia Sura Al Ghalam (68) katika mistari ya 44 na 45 inasema: Wale ambao wanakataa njia zetu tutawaangamiza pasipo wao kujua udanganyifu wangu (kaydi).

Kwa nini basi anafanya kinyume na kanuni yake mwenyewe na kupambana na uhuru wa kuchagua? Kwa hakika, Muumbaji haogopeshwi na uhuru wa kuchagua aliyowapa viumbe wake aliyo waumba mwenyewe.

Ndugu zangu, ni jambo la kuvunja moyo sana kwamba zaidi ya Waislam bilioni wanafuata Qur'ani hii bila kujua kwamba iko kinyume na Mungu wa kweli. Je! Mungu mwenye nguvu anahitaji udanganyifu na uongo ili kuwaangamiza wale wanaompinga? Je, yeye ni dhaifu sana kiasi kwamba hawezi kuwasiliana kwa kusema ukweli badala ya kutumia uongo na udanganyifu? Ni jambo la kushangaza kwamba Qur'ani

inamshusha Mungu mkuu kwa kiwango cha sisi wenye dhambi. Kwa upande mwingine, Mungu amewapa watu uhuru wa kuchagua kumkubali au kumpinga.

*Qur'ani inasema kwamba Mungu alimrasimisha Shetani kuwa mdanganyifu*

Sura Al-A'raf (7) aya ya 16 inasema kwamba Allah alimdanganya Shetani ili aweze kuwadanganya watu. Je, ni kweli kwamba Mungu mwenye huruma humpa silaha adui mbaya ili awaumize wanadamu? Je! Unaamini kwamba mama au baba mwenye upendo huajiri adui kuharibu mtoto wao?

Ni maombi na matumaini yangu kwamba utaisoma Injili ya Kristo na Biblia nzima kuelewa kuwa Mungu mwenye huruma hajamdanganya Shetani, wala hajapanga mambo mabaya ya kuharibu watu. Kwa kumpa Mungu sifa mbaya kama hizi zenye kuvunja moyo, Qur'ani haiwezi kuwa neno la Mungu wa kweli.

*Qur'ani inasema kuwa Allah alipanga waovu wamuumize Muhammad*

Sura Al An'am (6) katika aya ya 112 inasema: hali kadhalika tumemfanyia kila nabii maadui - mashet’ani wa kiwatu, na kijini, wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba-pamba, kwa udanganyifu. Na

angelipenda Mola wako mlezi, wasingelifanya hivyo. Basi waache na wanayo yazua.

Mungu wa kweli kamwe hashirikiani na majini ili kumuumiza nabii wake mpendwa. Mungu wa kweli anaokoa kutoka kwa waovu. Kwa kuwa Qura'ni inasisitiza ushirikiano wa Mungu na majini, haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu wa kweli.

*Qur'ani inasema kuwa Allah hutumia mapepo kueneza Uislamu*

Kwa upande mmoja Quran katika Sura Al-A'raf (7) mstari wa 27 inasema: Mungu alifanya mashet'ani marafiki kwa wasio imani. Kwa upande mwingine, tuliona, kwamba alipanga majini kumuumiza nabii wake, Muhammad. Sasa, Qur'ani katika Sura Al Jinn (72) mstari wa 1 hadi 2 inasema: Sema O Muhammad: imefunuliwa kwangu kwamba kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: hakika sisi tumesikia Qur'ani ya ajabu inaongoza kwenye uongofu, kwa hiyo tumeiamini na wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu mlezi.

Mungu wa Uislamu aliumba mapepo kama viumbe wabaya ili kumfuata Shetani na kuwa marafiki na wapagani na wasiokuwa Waislam na pia kumuumiza Muhammad, lakini kisha huwaongoza mapepo hao

kuacha urafiki na wasiokuwa Waislamu na kuwa marafiki na wafuasi wake ili kueneza Uislam.

Je, huyu mungu amechanganyikiwa? ni rafiki wa nani mungu huyu? Je! Mungu wa kweli hukubali mapepo kuwa wafuasi wake wa kweli? Je! Mungu wa kweli hutumia mapepo kueneza maneno Yake? Kwa mafundisho hayo ya ajabu, Qur'ani haiwezi kuwa kitabu cha Mungu wa kweli.

*Qur'an pia inamhusisha Mungu na uumbaji wa dhambi*

Sura Ash Shams (91) katika mstari wa 7 na 8 inasema kwamba Mungu alihamasisha dhambi katika wanadamu. Sura Al Balad (90) katika mstari wa 4 inasema kwamba Mungu alimuumba mwanadamu kwa shida na taabu. Sura za An Nisa (4) mstari wa 88; Al Araf (7) mstari wa 178 na Ibrahim (14) mstari wa 4 zote zinasema kwamba Mungu anapotosha.

Qur'ani inamtambulisha Mungu kama mwanzilishi wa vitendo vya uasherati na vya kuvunja sheria au kuwaongoza watu kupotea na kuwafanya kuwa wenye dhambi. Ina mtambulisha Mungu kama mtu ambaye moyo wake na akili hufukuzia dhambi. Mungu si kama mwanadamu. Anachukia vitendo vya dhambi na kupotosha. Maneno ya Qur'ani sio tu hayatoki kwa Mungu lakini pia hayawaongozi waislamu kwa Mungu.

## Je! Mungu wa Qur'ani anaamini katika haki sawa?

Tathmini ya nne ni kuona kama mungu wa Qur'ani anaamini kuwa watu wote ni sawa au la.

Qura'ni huhusisha ubaguzi na Mungu. Quran inasema katika Sura Al Bagharah (2) mstari wa 65 na Sura Al Maeda (5) mstari 60 na Sura Al Anfal (8) mstari wa 55 na Sura Al A'raf (7) mistari 175 hadi 177 na Al Tawba (9) mstari 28 kwamba wasiokuwa Waislamu ni wachafu na wanyama, lakini katika Sura Al-e Imran inasema kwamba Waislamu pekee ni wanadamu, wema na wasafi.

Madai haya ya Qur'ani hayawezi kuwa mafundisho ya kweli kikanuni na kiroho wala kijamii na kimaadili. Kwanini? kikanuni na kiroho, kwa sababu Qur'ani yenyewe inasema kwamba Waislamu kama wengine wote ni wenye dhambi. Ni sababu gani ya kiroho iliyobaki hapa ili kuwafanya Waislamu kuwa bora zaidi kuliko wengine? Hakuna. Kijamii na kimaadili madai hayo sio ya kimungu wala ya kweli. Je! Unawezaje kuweka mwislamu, Mkristo, Myahudi, Mhindu au wengine, kila mmoja aliumbwa na Mungu mmoja, utasemaje kwamba huyu ni mwanadamu lakini wengine ni wanyama? Mungu, aliyewaumba, anajua kwamba wote ni wanadamu, lakini Qur'ani haijui ukweli huu na huwaita wanyama. Unaona kwamba

Qur'ani haifanani na moyo wa Mungu na kwa hiyo haiwezi kuwa imekutoka kwa Mungu

## Je! Mungu wa Qur'ani anaheshimu uhuru wa kuchagua?

Tathmini ya tano ni kuona kama mungu wa Qur'ani anaheshimu Uhuru wa Uchaguzi au la

*Kwa Qura'ni Waislam tu ndiyo wana haki ya kuishi*

Qur'an inamtambulisha Mungu kama mtu mwenye kiu na damu ya wapinzani wake na wasio Waislam. Zaidi ya nusu ya Qur'ani, zaidi ya nusu ya wasifu wa Maisha ya Muhammad na sehemu kubwa ya Hadithi ni juu ya kuchukia na kushambulia wasio Waislamu na kumwaga damu yao kwa kutokuwa tayari kujiunga na Uislam. Wakati nabii na mwandishi wa Uislamu hutumia zaidi ya nusu ya maisha yake katika kushambulia wapinzani wake na wasio Waislam, basi unatarajia wafuasi wake wafanye nini na wapinzani wao na wasio Waislam? Ni aina gani ya maisha ambayo wasio Waislamu wataishi chini ya uongozi wa serikali ya Kiislamu?

Qur'an na vyanzo vingine vya Uislam vinatufunulia kwamba hawapaswi kuwa na uhuru au maisha mazuri (Suras 8:39; 48:29; 17:16). Matumizi ya nguvu na upanga hayawezi kuleta kujitoa kwa moyo.

Je, inawezekana kuwa na mtazamo kama huo kwa Mungu wa kweli na mwenye busara? Hapana. Qur'ani si sahihi kuhusu Mungu.

*Quran inasema kwamba Mungu analazimisha imani yake*

Kutoka Sura An Nisa (4) aya 89 na Nahl (16) mstari 106 tunaelewa kwamba Waislamu hawaruhusiwi kutumia uhuru walio pewa kutoka kwa Mungu wa kuchagua, kuacha Uislamu na kufuata imani wanayotaka. Kutoka Sura Al Bagharah (2) mstari wa 217 pia tunaelewa kwamba Waislamu wana uhuru usio na kikomo wa kuwakaribisha wasiokuwa Waislam kujiunga na dini yao na hata kuwalazimisha kukubali Uislamu, lakini itakuwa mbaya zaidi kuliko kuuwawa ikiwa wasio Waislamu wanakaribisha Waislamu kwenye dini yao.

Kwa hiyo, waislamu wana uhuru usio na kikomo wa kueneza Uislam; Wasio waislamu hawawezi, lakini kama wakifanya, watauawa. Uhuru huo wa upande mmoja ni uhuru wa ubaguzi na wakikatili, na hauwezi kutoka kwa Mungu wa kweli. Qur'ani haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu wa kweli na mafundisho hayo.

**, Quran ina mpango mzuri wa familia?**

Tathmini ya sita ni kuona kama Qura'ni ina mpango mzuri wa familia au la.

Qur'ani inawahimiza watoto wasiwaheshimu wazazi wao na ndugu zao. Sura Al Tawba (9) mstari wa 23 inawauliza watoto wadogo: Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanastahabu ukafiri kuliko Imani. na katika nyinyi atakaye wafanya ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhaalimu.

Qur'ani sio tu inawahimiza watoto kuasi dhidi ya wazazi wao, lakini pia inawahimiza kuua jamaa zao wasio Waislam. Sura Al Tawba (9) aya ya 123 inasema: Enyi mlio amini! piganeni na wale makafiri walio karibu yenu, na wakute ugumu kwenu. Na jueni, Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wacha Mungu.

Ndugu zangu, kutowaheshimu wazazi na kuua jamaa na wengine kwa ajili ya imani yao ni batili kwa Mungu wa kweli. Qur'ani haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu kulingana na maneno haya.

**Je, Qur'ani haikubadilishwa?**

Tathmini ya saba ni kuona kama Qur'ani ilibadilishwa au la.

*Qur'ani inasema kuwa Waislamu waliibadilisha*

Sura Al Baghara (2) mstari wa 106 unasema: ishara yoyote tunayoifuta au tunayo isahaulisha tunaileta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake. Hujui kwamba Mwenyezi mungu ni muweza wa kila kitu? (Nobel Koran). Sura An Nah (16) aya ya 101 inasema: Tunapobadilisha ishara pahala pa ishara nyingine, na Mwenyezi Mungu anajua anayo telemsha, wao husema: Ee Muhammad wewe mzushi. Bali wengi wao hawajui kitu.

Kutoka kwenye aya hizi na nyingine zinazofanana katika Qur'ani, tunaelewa kuwa nguvu za kisiasa za Muhammad zilivyozidi akaongezeka alibadili baadhi ya aya za awali za Qur'ani ambazo hakuzipenda na kuweka alizozipenda. Ili kuhalalisha matendo yake, aliwaambia watu kwamba Mungu aliifuta mistari hiyo kwa sababu haikuwa halali tena kwa Mungu, na aliwafunulia mistari bora. Jambo la kushangaza! Je! Inawezekana kwa Mungu kusema kuwa ana mstari bora kuliko ya awali wakati kila mstari anawosema ni kamilifu kwa sababu yeye ndiye Mungu mkamilifu? Je! Mungu hakuwa na ufahamu wa milele kwamba baadhi ya mistari yake ingekuwa inahitaji kubadilishwa katika siku zijazo ili apate kuisahihisha ili asiruhusu Qur'ani isiyokamilika ikaangukia mikononi mwa Muhammad?

Kwa kuondoa maneno yake ya awali, watu walikuwa na mashaka na wakamkosoa Muhammad, na baadaye waliuawa kwa upinzani wao. Kwa nini usiweke maneno kamili na ya mwisho tangu mwanzo ili kuepuka kukosolewa na kuua watu? Je! Mungu wa kweli atawachanganya watu kama hivi na kuwafanya kuchukiana? Kwa hivyo, unaweza kuona kwamba Qur'ani inathibitisha kwamba baadhi ya mistari yake ilifanywa kuwa batili kwa kubadilishwa na kuwekwa iliyo bora. Qur'ani isingesema kamwe kwamba mistari yake haifai kama ingekuwa imetoka kwa Mungu wa kweli.

*Hadithi pia zinasema kuwa Qur'ani imebadilishwa na haijakamilika*

Enzi za Muhammad na baada ya kifo chake, kulikuwa na nakala 8 za Qur'ani zinazotofautiana kila moja kwa sehemu nyingine. Muhammad hakuwa na uhakika ni nakala gani iliyokuwa sahihi lakini alidhani kwamba iliyo kuwa mikononi mwa mkwewe, Ali, ingeweza kuwa ndiyo sahihi. Baada ya kifo cha Muhammad, mgawanyiko kati ya warithi wake sio tu ulizuia uwezo wa kuidhinisha tafsiri aliyoichagua Muhammad bali ilimpelekea kiongozi mkuu, Othman, kuidhinisha Qur’ani ya sasa ambayo inakosa vifungu vingi.

Salim ibn Gheys (90 Hijra) katika kitabu chake, Siri ya Familia ya Muhammad, anasema kwamba Aya nyingi

hazipatikani kwenye Qur'ani ya sasa. Mistari mingi ililiwa na kondoo (au mbuzi); pamoja na baadhi ya mistari kutoka Suras Al-Nur (24), Al-Ahzab (33) na Al-Hujraat (49) ilipotea.

Ikiwa Qur'ani yenyewe na vitabu vya kale vya Uislam vinasema kwa sauti moja kwamba Qur'ani ilirudiwa, ikabadilishwa na kwamba mistari yake mingi haipo, Qur'ani inawezaje kuitwa kitabu kikamilifu na kutoka kwa Mungu?

Biblia haina madai ya kubadilishwa. Surah Al Hijr (15) katika mstari wa 91 inasema kwamba Qur'ani iliguswa na kubadilishwa. Hakuna sehemu yoyote kwenye Biblia ambayo inasema kwamba ilibadilishwa au kuharibiwa.

Viongozi wa waislamu  hawafundishi kwamba Qur'ani imebadilishwa au kwamba mistari yake mingi ilipotea, lakini kwa urahisi husema juu ya vitabu vya Wakristo na Wayahudi wakisema kwamba vilibadilishwa. Aya za Qur'ani zenyewe zinasema kwamba ilikuwa imeghushiwa. Je! Kitabu hiki cha kughushi kinawezaje kutoka kwa Mungu?

Qur'ani inasema katika aya ya Sura Al An'am (6) ya 34 na 115, na Sura Ynus (10) mstari wa 64: Hakuna mtu anayeweza kubadilisha maneno ya Mungu, na katika Sura Al Hijr (15) mstari wa 9 inasema: kwa sababu Mungu atailinda. Sasa, tunaelewa kuwa Qur'ani

imebadilishwa. Kwa hiyo, ikiwa ni neno la Mungu, hakuna mtu aliyeweza kuibadilisha.

Biblia na Injili ya Kristo ina kinga kutokana na shida za Quran. Mungu wa Biblia hawafanyi wafuasi Wake kuwa mateka wa dhambi, Shetani na waovu, lakini anawaokoa.

**Wakati wa kutafakari 9**

1. Kuna dini nyingi duniani na wafuasi wa kila dini wanadai kwamba dini yao ni kutoka kwa Mungu. Je, tuna uwezo wa kutathmini na kuona kama dini inatoka kwa Mungu au la?
2. Waislam wengine wanasema kwamba Qur'ani inatoka kwa Mungu kwa sababu zaidi ya Waislam bilioni wanaamini kwamba inatoka kwa Mungu. Unadhani/unafikiria nini? Je, ukweli au uovu hupimwa kwa wingi au ubora?
3. Je! tuna zana yoyote ya kuthibitisha kwamba Qur'ani haiwezi kuwa imetoka kwa Mungu wa kweli?
4. Je, tuna wajibu wa kugundua Neno la kweli la Mungu na kuliishi ?
5. Ikiwa unaamini kwamba Mungu yuko tayari kukuongoza kupata ukweli au kuwasaidia wengine kuugundua ukweli, chukua muda katika sala sasa.

## Je, Uislamu ni dini ya mwisho na kamilifu?

Viongozi wa Uislamu wamewaambia Waislamu kuwa Uislamu ni dini ya mwisho na bora zaidi. Je, huu ni ukweli? Je! Wana sababu yoyote ya msingi, kikanuni, kifalsafa, kiroho au hata ya kijamii ya kuthibitisha madai yao? Ukamilifu una maanisha nini katika Uislamu? Je! Ina maana kwamba Uislamu umeyajibu maswali yote ya msingi kuhusu maisha vizuri zaidi kuliko dini nyingine zote? Je, inamaana ya kwamba Uislamu umeleta mambo mapya na habari njema zaidi ambayo haikuwepo katika dini nyingine za kabla ya Uislamu? Je, ni vitu vipya vipi vyema ambavyo Uislamu umevileta ambavyo dini nyingine kabla ya Uislamu hazikuwa navyo ili Uislamu uweze kudai ukamilifu kwa sababu hiyo?

Je! Wewe, kama Mwislamu, umewahi kufikiria juu ya swali hili na kupata jibu lo lote? Unajua, kila mmoja wetu anawajibu wa kugundua sababu za madai yetu, ikiwa tunataka kuwa na ujasiri binafsi au kuweka wazi msimamo wetu kwa wanafamilia wetu na watu wengine.

Hebu niwaambie kwa ufupi katika utangulizi kabla ya kueleza sababu zangu ambazo zinaonyesha kuwa Uislamu sio tu haukuleta mambo mema mapya, bali

pia uliharibu maadili mema ya kidini yaliyokuwa yametoka kwa Ibrahimu, Musa na Yesu. Madai ya Uislamu kuwa kamilifu si ya kweli bali ni propaganda tu.

### Uislamu unamhusisha Mungu mambo yasiyo na mashiko

Sababu ya kwanza ya kuonyesha kwamba Uislamu hauwezi kuwa dini kamilifu ni kwa sababu unamhusisha Mungu na mambo ya siyo na mashiko. Je, Uislamu unamtambulishaje Mungu?

Sura Al Hashr (59) mstari wa 23 na 24 inasema kuwa Mungu ni mtakatifu, mwenye amani, utukufu na hekima. Lakini Suras Al-e Imran (3) katika mstari wa 54 na Al Anfal (8) mstari wa 30 inasema kuwa Mungu ndiye mdanganyifu bora kuliko wote. Sura Al Baghara (2) katika mstari wa 225, Sura Al-e Imran (3) mstari wa 28 na Sura An Nahl (16) mstari wa 106 mistari yote hii inasema kwamba Mungu aliwaruhusu Waislamu kusema uongo katika mazingira fulani.

Je, unaweza kuona mkanganyiko mkubwa katika aya hizi? Kwa upande mmoja, Mungu anaitwa mtakatifu, mwenye amani, mkuu na mwenye hekima, lakini kwa upande mwingine anaitwa mdanganyifu bora kuliko wote. Je! Mungu mwenye asili ya utakatifu, amani, mkuu na mwenye hekima awezaje wakati huo huo

kuwa mdanganyifu pia? Na Je, mungu mdanganyifu awezaje kuitwa mkuu na hekima?

Mungu anaitwa mtakatifu kwa sababu anachukia udanganyifu na kamwe hawezi kudanganya. Mungu mkamilifu haruhusu udanganyifu na uongo. Na, dini kamili haiwezi kumwita Mungu kuwa mdanganyifu au muongo. Ukimwita Mungu mdanganyifu, basi inamaanisha yeye si mkamilifu. Sasa itawezekanaje dini yenye mungu asiye mkamilifu iitwe dini kamilifu?

Je! Utamwitaje mtu mkamilifu ikiwa anafundisha udanganyifu na uongo? Je! Unaita imani yake kuwa imani kamilifu? hapana huwezi. Hii ni sawa na Uislamu. Kwa kuwa Uislamu unamwita Mungu wao mdanganyifu na mwongo, haiwezi kuwa dini kamilifu.

**Uislamu hauna jibu kamili kwa swali la maisha**

Sababu ya pili kwanini Uislamu hauwezi kuwa dini kamili, ni kwa sababu haina majibu kamili zaidi kwa maswali ya maisha ukilinganisha na dini nyingine.

Mtazamo wa Uislamu kuhusu maisha ya hapa duniani, siku ya hukumu na maisha baada ya kifo hauna ubora wowote kuliko dini nyingine zinazozingatia matendo ya watu ili kupata wokovu. Kwa nini basi Uislamu unaitwa kamili zaidi kuliko dini nyingine? Kama dini nyingine zote kabla ya Uislamu, Uislamu pia iliwafundisha

Waislamu kwamba maisha ya duniani ni uwanja wa vita kati ya mema na mabaya, na wokovu umejikita kwenye utakaso wa mara kwa mara kwa kutenda matendo mema hapa ulimwenguni. Mafundisho kuhusu siku ya hukumu na maisha baada ya kifo pia yalifanana kwa ukaribu. Kiukweli kabisa, dini nyingine zilikuwa bora zaidi kuliko Uislamu katika suala hili. Tofauti na Uislamu, hawakufundisha kwamba kuwalazimisha watu dini au kuwaua wengine ndicho kingewapeleka paradiso.

Kwa kulinganisha na imani katika Kristo, Uislamu hauwezi kabisa kudai ukamilifu kuzidi Ukristo. Injili inasema kwamba Yesu hana dhambi, yuko hai mbinguni na ndiye njia ya uzima ya kwenda mbinguni. Lakini Qur'ani haijawahi kuzungumza juu ya Muhammad kama hivi.

Qur'an yenyewe inathibitisha kwamba Yesu hana dhambi, na anaishi mbinguni, lakini haiwafundishi watu kumfuata Yesu kwa sifa zake hizi nzuri. Badala yake, inawahimiza watu kumfuata Muhammad ambaye alikuwa mwenye dhambi, alikufa na hayuko mbinguni. Ni wazi kabisa kwamba Ukristo wenye kiongozi asiye na dhambi na aishiye milele ni kamili zaidi kuliko Uislamu wenye kiongozi mdhambi ambaye alikufa akiwa na mashaka juu ya hatma yake.

Kwa hivyo unaweza kuona kwamba Uislamu hauna maelekezo bora zaidi ya usafi wa maisha ya duniani au kuhusu siku ya hukumu au maisha baada ya kifo kuliko dini nyingine. Kwa hiyo, kuuita Uislamu dini kamili si jambo la busara.

## Uislamu uliharibu dini zilizo mwamini Mungu mmoja.

Sababu ya tatu kwa nini Uislamu hauwezi kuitwa dini kamilifu ni kwa sababu uliharibu dini zote zilizokuwa na imani kwa Mungu mmoja katika Peninsula ya Arabia na nchi jirani.

Wafuasi wa dini ya imani ya Mungu mmoja ("One-God") walienea pwani zote za Arabia mpaka Uislamu ulipoanzishwa. Dini hizi ziliitwa dini za Abrahamu. Sura Al Mo'menun (23) katika mstari wa 84 hadi 90 na Sura Lughman (31) katika mstari wa 24 na 25 inathibitisha kuwa watu wengi wa Kiarabu walimwamini Mungu mmoja. Badala ya kulinda dini hizi za Ibrahimu, Uislamu uliwaangamiza na kuwalazimisha wafuasi wake kujiunga na Uislamu.

Dini ya Hanif ni mfano mmojawapo. 'Hanif' lilikuwa jina la kikundi maarufu cha kidini Kilichohubiri imani kwa Mungu wa Ibrahimu na kukataa kuabudu miungu mingine. Walikuwa Waarabu kutoka kabila la Muhammad mwenyewe, Quraish. Hadithi ya maisha ya

Muhammad iliyoandikwa na Ibn Ishagh inathibitisha kwamba Wahanifi walimwamini Mungu mmoja na walikuwa wafuasi wa dini ya Ibrahimu. Baada ya Muhammad kuleta Uislamu, Muhammad pia aliita dini yake dini ya Ibrahimu (S.3: 95; 4: 125; 6: 161) licha ya yeye kuharibu na kukataa imani nyingine za Ibrahamu.

*Uislamu ulihalalisha Ibada ya sanamu kwa muda mfupi.*

Wahanifi walikuwa na nguvu kuliko Muhammad katika imani yao kuhusu Umoja wa Mungu. Walikuwa kinyume na aina yoyote ya ibada ya sanamu na waliamini sana kwamba Mungu alikuwa Mmoja. Lakini Muhammad aliwaagiza Waislamu kuabudu sanamu tatu tofauti wakati akiwa Makka. Alisoma mstari katika Sura An Najm (53) ambao ulikuwa baada ya mstari wa 19. Ulisema kuwa sanamu tatu za; al-Lot, mungu wa uzazi, al-Uzza mungu wa nguvu na Manat, mungu wa hatima walikuwa viumbe waliyo barikiwa, na walikuwa wakimsaidia Mwenyezi Mungu katika kazi yake. Baada ya kusema haya, Muhammad na wafuasi wake walisujudu sanamu hizi na kuziabudu.

Unaona kwamba Qura'ni ilimwamuru Muhammad na wafuasi wake kuabudu sanamu tatu badala ya Mungu. Waislamu huko Makka waliabudu sanamu hizi chini ya uongozi wa Muhammad kwa muda fulani hadi walipohamia Medina. Walipo kuwa Medina

Muhammad alikiri kuwa aya hiyo ya Quran ilikuwa imetoka kwa shetani. Wala Wahanifi wala Wakristo wala Wayahudi wala Wazorohastia na wala Wasabe hawakuamini wala hawakufanya ibada ya sanamu. Walikataa vikali ibada za aina hiyo. Msimamo wao wa kiroho kuhusu Umoja wa Mungu ulikuwa mkubwa zaidi kuliko msimamo wa Muhammad. Muhammad hakufurahia sio tu msimamo wao juu ya imani yao kwa mungu mmoja, bali pia aliwalazimisha kuufuata Uislamu.

Basi je, Uislamu na ibada zake za sanamu na vita juu ya imani kwa Mungu mmoja wawezaje kuitwa dini kamilifu zaidi kuliko nyingine ambazo zimejiweka mbali na kila aina ya ibada ya sanamu? Haiwezekani. Hata hivyo, aya ya kuabudu sanamu iliondolewa kwenye Qura'ni baadaye. Baada ya kifo cha Muhammad, aya hii iliondolewa kwenye Qura'ni na warithi wa Muhammad. Waliamini kwamba ilitoka kwa shetani na ilibidi kuondolewa. Wasomi wa kale wa Uislamu wameweka aya hiyo katika vitabu vyao ambavyo bado tunaweza kuvifikia. Mstari halisi unasoma hivi: "Hawa ndio wanawake walioinuliwa, na sala zao za kweli zakuwaombea zinaweza kutarajiwa".

*Ni kwa sababu gani Muhammad aliruhusu ibada ya sanamu?*

Sababu yake kuu ilikuwa shinikizo la kisiasa. Amlipoteza mke wake mwenye kumhimiza na mwaminifu, Khadijah, na mjomba wake, Abutalib, ambao walikuwa kama ngao yake dhidi ya shinikizo la waabudu sanamu ambao alimpinga huko Makka. Kwa sababu hiyo, alijisikia mpweke na akakosa nguvu za kupinga shinikizo la viongozi wa Makka dhidi yake na marafiki zake waislamu. Kwa sababu ya ugumu huu aliamua kufanya mabadiliko kidogo ya siasa zake ili kukubalika na wapinzani wake. Kwa sababu hii, aliruhusu ibada hizi tatu muhimu za sanamu za Quryshi. Hii ilimpa uhakika wa usalama wake huko Makka kwa muda fulani mpaka alipokimbia kwenda Medina.

Haijalishi ilikua kwa sababu gani, Muhammad na wafuasi wake waliabudu sanamu, kwa kiroho inaitwa "kufanya washirika wa Mungu". Wala Ibrahimu wala Musa wala Yesu, ambao walikuwapo kabla ya Muhammad, hawakuidhinisha ibada yoyote ya sanamu, lakini Muhammad na Qur'ani waliruhusu ibada hizo, ingawa ilikuwa kwa muda mfupi.

Unaona kwamba Uislamu wa Muhammad sio dini kamilifu kuliko zote. Madai ya ukamilifu yalikuwa na

imekuwa propaganda za kisiasa tu, ingawa ni kinyume na moyo wa Mungu.

**Uislamu unaruhusu uhusiano katili**

Sababu ya nne kwa nini Uislamu hauwezi kuwa dini kamilifu ni kwa sababu ya uhusiano wake wa kikatili na watu.

Nimeshajadili katika mazungumzo yangu ya awali kuhusu Uislamu kuruhusu waume kupiga wake zao; hii ilikuwa haikubaliki wakati wa Ibrahimu, Musa na Yesu. Je, kumpenda mke wako na kuishi naye kama mwanadamu mwenzako kunafanya dini yako kuwa bora au kumpiga? Uislamu hauwezi kuwa dini kamilifu.

Uislamu pia unaweka kikwazo kwamba chochote kilichofundishwa na Muhammad, watu wanapaswa kukitii bila maswali. Hii pia ilikuwa haikubaliki katika imani ya Ibrahimu, Musa na Yesu

Uislamu pia huwafundisha watoto kupuuza malezi ya wazazi wao kama wazazi wao si waislamu. Mtazamo huu huwezi kuitwa mkamilifu kwa kuwa ni kinyume na matakwa ya Mungu aliye waumba watu na uhuru wa kuchagua na kuwasihi watoto kuwaheshimu wazazi wao. Uislamu pia unawahimiza waislamu kuwa

wanapaswa kuzitokomeza dini nyingine zote na kuwalazimisha wafuasi wake kuufuata Uislamu.

Hivyo unaweza kuona kwamba Uislamu si tu bora kuliko dini za awali, bali ni katili na una kasoro nyingi katika mtazamo wake kwa familia au watu wengine.

Uislamu umejiondoa wenyewe kwenye maadili bora. Dhamiri huita upendo, furaha, msamaha, amani, uvumilivu, wema, fadhila, upole, na kujidhibiti ni vitu vizuri katika mahusiano. Kwa nini? Kwa sababu tabia hizi huleta watu pamoja ili kushirikiana wenyewe katika njia ya ubunifu ili kupata matokeo bora zaidi, kuishi kwa amani pamoja na kufurahia uwepo wa kila mmoja.

Lakini Uislamu unapingana na tabia hizi. Tabia ya Uislamu kwa wapinzani wake na wasio Waislamu ni ya mateso na uharibifu. Uislamu unatoa haki zaidi kwa waume na kuwafundisha kuwapiga wake zao. Uislamu ni tishio kwa upendo wa kweli kati ya mume na mke mmoja, na unamwagiza mtu awe na wake wengi. Uislamu ni tishio kwa Waislamu wa wastani, wasiokuwa Waislam na wote ambao hawafuati kikamlifu maadili ya Kiislam. Kwa mitazamo hii ya kikatili Uislamu hauwezi kuitwa kuwa dini kamilifu.

**Uislamu hautoi uhakika wa wokovu**

Sababu ya tano kwanini Uislamu hauwezi kuwa dini kamilifu ni kwa sababu hautoi uhakika wa wokovu.

Wakati uhakika wa wokovu ni ujumbe muhimu sana wa Mungu, Uislamu hauna ujumbe huo. Hakuna Mwislamu anaweza kuzungumza kuhusu maisha ya baada ya kifo chake kwa kujiamini. Mungu wa Uislamu alimwacha hata Muhammad wake mpendwa na mashaka na alikufa akiwa na hofu ya hatma yake. Mungu wa Uislamu hawezi kuwaokoa waaminifu wake katika maisha yao hapa duniani na kuwapa furaha kamili.

Hakuna anayeita mashaka na hofu ukamilifu. Mungu wa dini kamilifu lazima afanye kazi yake kikamilifu, awaokoe watu katika maisha yao ya hapa duniani na kuwapa uhakika na furaha. Je! Sio jambo la kukatisha tamaa kwamba mungu wa Uislamu huwahakikishia Waislamu wanaomfuata Shetani kuwa asilimia mia moja watakwenda jahannamu, lakini kamwe hawapi uthibitisho wa asilimia mia moja wafuasi wake wenye haki kuwa watakwenda paradiso?

Wafuasi wote wa Biblia, iwe nabii au mfuasi wa kawaida, wana uhakika wa wokovu na kwenda mbinguni au paradiso.

Sasa Uislamu utakuwaje kamilifu kuliko dini nyingine bila ya uhakika wa wokovu? Haiwezekani.

Neno "ukamilifu" ni neno nzuri na la kutia moyo. Lakini mara nyingi hutumiwa kwa urahisi sana. Uislamu ni mojawapo ya dini zinazojiita kamilifu. Kuna watu na imani nyingi ulimwenguni zinazojiita kamilifu. Lakini ni jukumu letu binafsi kuchunguza madai yao na kugundua kama kuna ukweli katika madai yao au la. Kwa hili, tutaweza kuwa na uwezo wa kujiokoa wenyewe na familia zetu kutokana na uongo. Uongo ni mbaya bila kujali kama unatoka katika imani yetu, au familia zetu, au baba zetu au kutoka kwa wengine, tunahitaji kuwa na ufahamu wa hilo na kujikinga nalo.

Unaona kwamba viongozi wakuu wa Uislamu kutoka kwenye madhehebu ya Sunni na Shia wote wamekuwa wakisema kuwa Uislamu ni dini kamilifu kwa zaidi ya miaka 1400. Lakini vitendo vyao vimeonyesha kwamba hawawezi kuwa wanasema ukweli katika madai yao. Kwani viongozi wa dhehebu moja huwaita wafuasi dhehebu lingine wasioamini au makafiri, kwa maana hiyo kulingana na maagizo ya Qur'ani lazima waangamizwe. Katika kipindi cha miaka 1400 iliyopita, vikundi hivi viwili vimeua mamilioni ya wafuasi wa kila mmoja. Ikiwa Uislamu ni dini kamilifu, kwanini imeshindwa kuutumia ukamilifu wake kuleta uhusiano

wa amani kamili kati ya madhehebu haya ili kila dhehebu liweze kuheshimu utawala wa mwenzake, na waishi kwa amani na kuheshimiana? Tatizo sio wao. Tatizo liko kwenye misingi ya Uislamu. Ni Uislamu ambao umeruhusu uondoaji na uharibifu wa wale wenye fikra tofauti na zao. Qur'ani ingekuwa kama Injili ya Yesu Kristo, ambayo inatoa upendo kwa wapinzani na maadui, hakuna Mwislamu angefurahia kifo cha mtu yeyote. La hasha! Qur'ani si kama Injili. Hakuna sababu nzuri ya msingi ya kuuita Uislamu dini ya mwisho na kamilifu.

**Wakati wa kutafakari 10**

1. Kuna watu wengi ulimwenguni ambao wanadai kuwa imani yao pekee ni chaguo sahihi na kamilifu kwa ulimwengu. Hata hivyo, dai moja tu ndilo linaweza kuwa la kweli, na wengine lazima wawe wanasema uongo. Tunawezaje kugundua dai la kweli?
2. Je! Una sababu zozote za kuonyesha kwamba Uislamu hauwezi kuwa dini ya mwisho na kamilifu? Toa mifano.
3. Kwa nini waislamu na wasio waislamu wanahitaji kuwa na sababu nzuri za kufuata imani zao?
4. Mungu hujisikiaje anapohusishwa na dini fulani kwa uongo?

5. Ikiwa umegundua kuwa Njia ya Yesu Kristo ndiyo Njia pekee ya kweli, je sio wakati sahihi sasa wa kuweka imani yako kwake?

# Nani kati ya Yesu au Muhammad - anaweza kuwa kiongozi mzuri?

Kigezo gani cha kiroho cha kiongozi mzuri kwako, mwenye dhambi au asiye na dhambi? Nimewauliza watu swali hili hili kwa muda wa miaka 20 sasa. Je ni kiongozi yupi atakaye weza kukuongoza vizuri kiroho, mwenye dhambi au asiye na dhambi? Je ni gari gani litakalo faa kwenda safari, zuri au bovu? Je utaweza kuishi maisha mazuri na mke au mme mwenye upendo na mkarimu au mgonvi na asiye na huruma?

Watu daima hufurahia kiongozi mzuri, mke mzuri, gari zuri au kitu kingine chochote kinachofanya maisha yao kuwa mazuri zaidi. Kwa nini? Kwa sababu Mungu alituumba kwa namna ambayo mioyo yetu daima ina hamu ya mambo mazuri na yaliyo kamilifu. Hatutaki kamwe kuwa na familia mbaya, mke, nyumba, kiongozi, gari au kitu kingine chochote kibaya. Hakuna mwenye lengo la kwenda sokoni na kununua vitu vibaya. Unapenda kutumia pesa yako kwa mambo mazuri. Mafanikio yako katika mambo mazuri. Makampuni makubwa ya kimataifa yamefanikiwa kwa sababu ya viwango vyao vizuri. Wanatumia kiasi kikubwa cha fedha ili kutengeneza bidhaa nzuri na za kuaminika ili kuvutia wateja, na si kuwapoteza.

Katika maisha ya kiroho, ni vivyo hivyo. Kwa kuwa Mungu ni mzuri na mkamilifu, anatamani vitu vizuri na vikamilifu, na anatarajia tufuate mfano Wake mwema na mkamilifu. Mungu anataka tumfuate kiongozi mkamilifu na anayetoka mbinguni. Mungu hupenda kuchagua kiongozi asiye na dhambi badala ya mwenye dhambi. Anataka tumfanye kiongozi asiye na dhambi kuwa mfano wetu. Hata Qura'ni yako katika Sura Az Zomar (39) kupitia mstari wa 17 hadi 18 inasema: ....tangazeni habari njema kwa .... Wale wanao sikiliza, na kuyafuata mazuri yaliyomo ndani yake. Aya hizi zinakuambia kwamba unahitaji kusoma Qur'ani na kutambua ni nani bora zaidi na kisha kumfuata mtu huyo.

Hebu tuangalie Qura'ni; ikiwa Yesu hana dhambi na ni mkuu kiroho kuliko Muhammad, ninyi Waislamu basi mnahitaji kumfuata Yesu aliye mfano mzuri badala ya Muhammad.

## Qura'ni inasema kwamba Yesu ni mtakatifu na masihi

Sura Al-Imran (3) mstari wa 45 na Sura An Nisa (4) mstari wa 171 inasema kwamba Yesu ndiye Kristo. Neno "Kristo" linamaanisha nini? Kristo linamaanisha "Mpakwa mafuta"; Yule ambaye Mungu amempaka mafuta kwa Roho Wake kwa ajili ya utumishi Wake. Mungu mwenyewe anapompaka mafuta mtu, ina

maanisha mtu huyo ni mtakatifu na hana dhambi. Hakuna sehemu yoyote kwenye Qur'ani inayosema kwamba Mungu alijifunua kwa Muhammad na kumpaka mafuta kwa ajili ya utume wake.

Unaona kwamba Yesu Kristo ana nafasi kubwa na ya juu kiroho kuliko Muhammad katika Qura'ni. Sasa je, unahitaji kumfuata yupi, Yule aliyeguswa na mungu mwenyewe, au yule ambaye hakumwona Mungu na wala hakuguswa naye?

## Qura'ni inasema kuwa Yesu ni Neno takatifu la Mungu

Kwa mara nyingine, Sura Al-e Imran (3) katika mstari 45 na Sura An Nisa (4) katika aya 171 zinasema kuwa Yesu ni Neno la Mungu. Katika falsafa ya kidini, Mungu pekee ndiye anayeitwa "Neno". "Neno" ni jina la kifilosofia la Mungu. ukiwauliza wanafalsafa wa kiislamu "Mungu ni nani?" watakujibu yakuwa, "Yeye ni Neno." Inashangaza kwamba Qur'ani inamwelezea Yesu kwa namna ile ile ambayo Mungu ameelezewa katika falsafa ya Uislamu. Kwa maneno mengine, Qur'ani inasema kuwa Yesu ni Neno la Mungu, inamaanisha kwamba "Ana asili ya Mungu"

Hebu nikwambie jinsi gani Mungu kama "Neno" anavyofanya kazi kati ya watu. Katika uhalisia, Mungu Neno anajielezea Mwenyewe kwa njia mbili. Njia ya

kwanza ni kupitia maneno yaliyoandikwa, na njia ya pili ni kupitia ufunuo binafsi. "Kupitia maneno yaliyoandikwa" inamaanisha kwamba Mungu Neno anajielezea Mwenyewe kupitia Maandiko matakatifu. "Kupitia ufunuo binafsi" inamaanisha Neno (Mungu) anajifunua mwenyewe kama alivyo. Kupitia maandiko matakatifu Mungu anaelezea sifa zake na mpango wake kwa ajili yetu ili tujitayarishe kukutana naye binafsi. Mungu anajifunua kwetu binafsi ili kutufunulia utukufu wake kwetu ili tuwe makini naye na kujitayarishe kumwalika yeye na maneno yake ndani ya mioyo yetu. Kwa maneno mengine, kama Mungu asipo jidhihirisha kwetu na asipo ishi ndani ya mioyo yetu, maneno yake hayatakuwa na mifano hai katika maisha yetu.

Ngoja nikupe mfano ili ukusaidie kuelewa zaidi: Ni uwepo binafsi wa baba yako wa duniani ambao una fanya maagizo yake yawe na uzito kwako kama mtoto wake. Ikiwa baba yako amejificha na haonekani kwako, basi utakosa uhusiano wa karibu naye na hii hufanya maelekezo yake yasiwe na uzito katika maisha yako halisi. Hii pia ni sawa na uhusiano wako na Mungu. Ikiwa Mungu hana uhusiano wa karibu na wewe, umbali wake unafanya maneno yake yawe mbali nawe.

Kwa kuwa Qur'ani inasema kwamba Yesu aliguswa na Mungu mwenyewe na pia inamwita Yesu kwa jina la

Mungu, inamaanisha kuwa Yesu pekee ndiye ambaye anaweza kuleta Neno la Mungu lililoandikwa au Maandiko Matakatifu ndani ya moyo wako na kukuokoa. Hiki ndicho cheo kitakatifu cha juu kabisa ambacho Qura'ni inampa Yesu lakini haimpi Muhammad

Muhammad hawezi kufanya maandiko matakatifu kuwa na umuhimu halisi katika maisha yako. Muhammad sio Neno la Mungu, kwa hivyo hawezi kuunda uhusiano wa karibu kati yako na Mungu. Ndiyo sababu alisema kwamba hakuwa na uhakika juu ya maisha yake ya baadaye, na pia hakuweza kuwahakikishia wafuasi wake hatima yao. Pili, sio kama Yesu, Muhammad hakuwa na uhusiano binafsi na Mungu na kwa hiyo hawezi kumwelezea Mungu kwa watu kama Yesu alivyofanya.

Kwa hiyo kwa mujibu wa Mafundisho ya Qur'ani, tunaona kwamba Yesu anatambulishwa kwa jina la Mungu na ana nafasi kubwa zaidi ya kiroho kuliko Muhammad. Ninyi Waislamu mnahitaji kumfuata Yesu badala ya Muhammad.

## Qur'ani inasema kuwa Yesu ni Roho wa Mungu

Sura An Nisa (4) katika mstari wa 171, Sura Maryam (19) mstari wa 17 na Sura Al Anbiya (21) katika mstari wa 91 imeandikwa kwamba Yesu ni Roho wa Mungu.

Kwa kimakosa, baadhi ya wasomi wa Kiislam wanasema kwamba hiyo sio Roho ya Mungu bali ni roho nyingine au ni malaika kutoka kwa Mungu ambaye alizaliwa na Mariamu. Hii ni kinyume na mafundisho ya Qura'ni. Katika sehemu kadhaa za Qura'ni ya Kiarabu imeandikwa kwamba Mungu alimtuma Roho wake kwa Mariamu na sio moja wapo wa roho zake au malaika. Kuna tofauti kati ya Roho wa Mungu na malaika wa Mungu au moja wapo wa roho nyingine za mungu, haya ni mambo mawili tofauti. Ikiwa Mungu alitaka kumtuma malaika wake, angeweza kusema wazi kwamba alimtuma malaika wake. Kwa kuwa yeye hupenda kuzungumza maneno ya uwazi na yasio na utata. Kwa hiyo, wale ambao wanatafsiri hii kama mmoja wa malaika wa Mungu wanabadilisha maana halisi ya maneno ya Qur'ani zao wenyewe.

Basi tuseme kwamba ni malaika aliyekuja kwa Mariamu na akazaliwa kama Yesu Kristo. Bado nafasi ya kiroho ya Yesu Kristo itakuwa kubwa kuliko nafasi ya kiroho ya Muhammad. Kwa sababu malaika yu daima na Mungu, anaishi milele na anajua kila kitu kuhusu ulimwengu wa yasioonekana. Lakini Muhammad anasema katika Sura Al-A'raf (7) aya ya 188 kwamba hajui kitu chochote kutoka ulimwengu wa yasioonekana. Kwa hiyo, Yesu anajua kila kitu cha

Mungu, lakini Muhammad hajui. Pia tunajua kwamba Muhammad alikufa na hayuko mbinguni.

Kwa hiyo, tunaweza kuona kama neno "Roho wa Mungu" linatafsiriwa kama malaika au linatafsiriwa kama lilivyo katika mfumo wake wa Kiarabu, katika hali zote mbili zinaonyesha kuwa nafasi ya kiroho ya Yesu Kristo iko juu kuliko nafasi ya kiroho ya Muhammad. Kwa hiyo ni vizuri zaidi kwako umfuate yeye aliye na nafasi ya juu ya kiroho kuliko Muhammad.

## Qur'ani inasema kwamba Yesu ni Muumbaji na Mponyaji

Sura Al-Imran (3) aya ya 49 na Sura Al Maeda (5) aya ya 110 zinasema kuwa Yesu alimuumba ndege, akafufua wafu na kuwaponya vipofu.

Kwa mujibu wa Qura'ni, Yesu bado yu hai na anaishi mbinguni. Kwa kuwa Yeye yu hai, bado ana uwezo wa kuumba, kuponya na kuwafufua wafu, lakini Muhammad hakuwa na mamlaka hayo ya kutoka mbinguni. Watu wote wanahitaji mtu wakuwaponya na kuwarudishia uzima. Ni lazima kumheshimu mtu anaetoa uhai zaidi ya yule asiye na uwezo huo. Je, si jambo jema kama Yesu angekuwa kiongozi wako na ungekuwa na uhakika wa uponyaji na uzima? Ingekuwa vizuri umfuate Yesu.

## Qura’ni inasema kwamba Yesu ni mtakatifu na hana dhambi

Sura Maryam (19) katika aya ya 19 inasema kwamba Yesu Kristo hana dhambi na ni mtakatifu. Hakuna mtu anaitwa asiye na dhambi kwenye Qur'ani isipokuwa Yesu. Qur'ani huwaita manabii wengine wote na Muhammad wenye dhambi. Baadhi ya Waislamu wanaamini kwamba Muhammad hana dhambi. Imani hiyo ni kinyume na mafundisho ya Qura'ni.

Angalia kile Qura’ni inachosema juu ya Muhammad: Sura Muhammad (47) katika mstari wa 19 inamwambia Muhammad: .... omba maghufira kwa ajili ya dhambi yako na ya waumini wanaume na waumini wanawake. Sura Al Fath (48) katika aya ya 2 inasema: Mwenyezi Mungu akusamehe Muhammad kwa makosa yako yaliyotangulia na yajayo. Sura Ghafir (au Al Mo'men) (40) katika aya ya 55 inasema [kwa Muhammad]: Naomba msamaha kwa dhambi zako. Katika Sura Al-A'raf (7) mstari wa 188 Muhammad anasema: ... na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ningejizidishia mema zaidi, wala ovu lisinge nigusa.

Ikiwa Muhammad alikuwa mtu asiye na dhambi, asinge weza kusema  haya. Yeye anakiri kwamba uovu ulimgusa na kumfanya atende dhambi. Aya zote hizi zinasema kuwa Muhammad alikuwa mwenye dhambi. Pia, Sura Loghman (31) katika mstari wa 34 na Sura Al

Ahghaf (46) katika mstari wa 9 inasema kwamba Muhammad hakuwa na uhakika wa wokovu wake baada ya kifo. Hii ina maana kwamba Muhammad hakuwa na uhakika kama dhambi zake zimesamehewa, vinginevyo asingekuwa na wasiwasi juu ya siku zijazo.

Unaona kwamba Qura'ni inamwita Muhammad mwenye dhambi, lakini Yesu ni mwenye haki, mtakatifu na asiye na dhambi. Mwenye dhambi hawezi kukuongoza kwenye utakatifu na haki. Unahitaji kumfuata Yesu asiye na dhambi badala ya kumfuata Muhammad mwenye dhambi.

## Qura'ni inasema kwamba Yesu yuko hai mbinguni

Sura Al-Imran (3) katika mstari wa 55 na Sura An Nisa (4) katika mstari wa 158 inasema kwamba Yesu alipaa mbinguni. Lakini Muhammad alikufa na kwa mujibu wa Sura Maryam (19) mistari ya 66 mpaka 72 hayuko mbinguni.

Qura'ni yenyewe inakwambia kuwa Yesu yuko hai mbinguni lakini Muhammad alikufa na hayuko mbinguni; anasubiri hukumu ya siku ya mwisho. Ndiyo maana sisi sote tunahitaji kumfuata Yeye aliye hai na mbinguni. Yeye tu ataweza kutuongoza kwenda mbinguni, kwa sababu Yuko mbinguni.

Unaona kwamba hata Qura'ni inamwonyesha Yesu kuwa ni mkuu zaidi kuliko Muhammad. Kama ukisoma Injili ya Yesu Kristo utastaajabishwa kabisa. Mfuate Yesu Kristo.

**Wakati wa kutafakari 11**

1. Waislam wengine wanasema kwamba ingawa Yesu ameelezewa kuwa asiye na dhambi na ni mkuu kiroho zaidi ya Muhammad katika Qura'ni, lakini Mungu alimchagua Muhammad kukamilisha kazi yake duniani. Unafikiria nini? Je, Mungu alikabidhi ukamilishaji wa Kazi yake kwa mwenye dhambi badala ya mtu asiye na dhambi?
2. Tuseme Mungu anampa kazi yake ya mwisho mwenye dhambi badala ya mtu asiye na dhambi. Je, hii haipotoshi watu katika kufikiri kwamba Mungu hapendi usafi bali dhambi? Je hii haiwezi kusababisha watu wakamfuata kila kiongozi wanaomtaka kwa vile Mungu hana kiwango kizuri cha kumchangua kiongozi ?
3. Tukizungumza kimantiki, je si jambo zuri kumfuata kiongozi wa kiroho asiye na dhambi kama mfano wetu badala ya yule mwenye dhambi?
4. Injili ipo katika lugha za kiislamu duniani. Je! Hufikirii kwamba Waislamu wanahitaji kusoma Injili wenyewe na kuhamasiswa binafsi na sifa za Yesu Kristo?

5. Waombeeni Waislamu wawe na ujasiri wa kuisoma Injili.

## Uongozi katika Uislamu ni wa vurugu

Kama unavyojua, tukifanya majadiliano kuhusu kila kitu cha msingi maishani mwetu bila kutumia dhamiri zetu inaweza kutuletea kuwa wapuuzaji, watu wenye itikadi kali na wasio kubali kubadilika. Hii pia ni kweli ukilinganisha na uongozi. Na, ni kwa sababu hii, ningependa kuuliza maswali machache ya msingi na kupata majibu yake kabla ya kuanza mjadala wetu wa leo ili tuweze kuendelea kuwa na akili na mioyo huru.

**Ni uongozi wa aina gani ungependa kuuona katika familia au jamii yako?**

Je, ni kiongozi mwenye unyenyekevu ambaye anajiona kama mtumishi wa familia na jamii yake, asiye na ubaguzi kati ya wanaume na wanawake, au kati ya mwenyeji na mgeni, na mwenye kukubali kukosolewa? Au kiongozi ambaye ni dikteta na mbaguzi, asiye kubali kurekebishwa, mwenye kukandamiza au kuwaangamiza wapinzani wake?

Kwa uzoefu wangu binafsi, kwa miaka mingi ya kujifunza juu ya tamaduni nyingi na safari yangu ya kwenda sehemu mbali mbali ulimwenguni. Inanionyesha kwamba watu hupenda kuwa na kiongozi mzuri na mnyenyekevu. Nina uhakika kwamba dhamiri yako pia inathibitisha hili. Je! Ungependa kiongozi anayewatendea wafuasi wake na wengine haki sawa,

bila kujali imani zao, utaifa au rangi yao, au kiongozi anayewabagua wengine au hata kuwaangamiza ikiwa hawatamfuata au kuifuata imani yake? Kwa mara nyingine dhamiri zetu zinatuambia kwamba kiongozi mzuri ni yule atakayekaa mbali na aina zote za ubaguzi.

Kiongozi wa Kiislam sio tu anabagua kati ya mume na mke, mwanamume na mwanamke, mwenyeji na mgeni, lakini pia ana haki kisheria ya kuwaangamiza kama hawatamfuata. Hebu niwafunulie haki za kisheria za kuwabagua na kuwatenga wengine ambazo dini ya kiislamu humpa kiongozi wake.

## Ubaguzi ndani ya familia

Sura Al Baghara (2) katika mstari wa 228 na Sura An Nisa (4) katika aya ya 34 inasema kwamba wanawake ni tabaka la chini. Sura An Nisa (4) katika mstari wa 11 na 176 inasema kuwa mabinti wanapata nusu ya urithi kuliko wanaume. Sura Al Baghara (2) katika mstari wa 282 imeandikwa kuwa mashahidi wanawake wawili ni sawa na shahidi wa kiume mmoja. Sura Al Ahzab (33) katika mstari wa 33 pia inasema kwamba wanawake wanapaswa kuishi nyumbani kimya na hawapaswi kwenda nje. Sura An Najm (53) katika mstari wa 2 inatuambia kwamba Muhammad ndiye mmiliki wa wake zake. Sura An Nisa (4) katika mstari wa 34 na Sura Sad (38) katika mstari 44 inatuambia kwamba waume wanaweza kuwapiga wake zao. Hakuna shaka

kwamba wale ambao wanaifuata kiukweli Qur'ani hufanya ubaguzi huu wa kifamilia katika maisha yao halisi ya kila siku.

*Kiongozi wa kiume wa familia ana haki ya kuwaua wanafamilia*

Sura Al Tawba (9) katika mstari wa 123 inasema: Ninyi mnaoamini (Waislamu), waueni walio kufuru walio karibu nanyi, jamaa na majirani, ili waweze kuujua na kuutambua ukatili wenu. Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaotimiza matakwa yake.

Hii ina maana kwamba Mwislamu mwenye kutii matakwa ya Qur'ani ana haki za kidini za kupigana na wanafamilia wake wa karibu, marafiki na majirani na hata kuwaua ikiwa hawatajiunga na Uislam. Hivyo, kiongozi wa Kiislamu ana haki ya kuharibu maisha ya wanafamilia yake, marafiki na majirani kwa ajili ya dini yake.

## Ubaguzi ndani ya jamii

Tumeangalia aya kutoka Qur'ani ambazo zinahalalisha ubaguzi ndani ya familia. Sasa hebu tuangalie ubaguzi ndani ya jamii.

Sura Al Ahzab (33) mstari wa 36 inasema: Si kwa muumini, mwanaume au mwanamke, jambo lolote


likiamuliwa na Mwenyezi Mungu na mtume wake kutakuwa hakuna chaguo lingine lolote ila kuufuata uamuzi wake. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Qura'ni, kiongozi wa Kiislamu ana haki ya kutokuulizwa chochote katika uongozi wake na mtu yeyote. Sura Al Mujadila (58) katika mstari wa 20 inasema: Wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake watakuwa miongoni mwa wale watakaoteseka.

Katika masomo ya uongozi, uongozi wa namna hii unaitwa uongozi wa Njia moja au udikteta ambao kiongozi anatarajia wafuasi wake wamfuate kwa kila asemalo.


Ukurasa unaofuata hapo chini unalinganisha uongozi wa Muhammad na uongozi wa Yesu. Mshale wenye kuelekeza upande mmoja unaonyesha mtindo wa uongozi usio na kuwahusisha watu katika uongozi wakati, mshale wenye kuelekeza pande zote mbili unaonyesha uongozi wa wazi ambao unahitaji ushirikiano wa wafuasi au wajumbe. Kwa hiyo unaona kuwa mawasiliano katika uongozi wa Muhammad ni mawasiliano ya njia moja, kutoka juu kwenda chini, na watu hawana haki ya kutoa maoni yao, lakini mtindo wa uongozi wa Yesu unawahusisha watu na wana uhuru kamili wa kujieleza wenyewe kila mmoja na kwa viongozi wao.

## Ulinganifu kati ya uongozi wa Muhammad na Yesu

### Uongozi wa Muhammad




### Uongozi wa Yesu




Ngoja nikupe mfano wa ukatili uliyoko katika uongozi wa Kiislamu. Hadithi ya 330 katika Kitabu cha 89 na toleo la 9 la Bukahri inasema kwamba Muhammad alisema: "Nilitaka kutoa agizo la kukusanya kuni na kisha kumwambia mtu atangaze Adhana[7] kwa ajili ya

[7] Wito kutoka kwa minaret kwa ajili ya sala za pamoja.

sala na kisha niagize mtu awaongoze watu kwenye sala na kisha ningepita nyuma yao na kwenda kuchoma nyumba za wanaume ambao hawakujitokeza kwa ajili ya sala. "

Muhammad kama mwenye mamlaka ya juu katika uongozi wa Kiislam alichagua kuacha jukumu lake la lazima la kuhudhuria sala na kwenda kuchoma nyumba za watu ambao hawakuwepo katika sala za pamoja. Kiongozi wa kiislamu wa sasa pia ana wajibu wa kufuata mfano wa uongozi wa Muhammad na kuwa na ukatili dhidi ya wale wasiosali. Uongozi wa kiislamu una msingi wa majadiliano ya njia moja. Unaona kwamba una uhuru wa kumfuata kiongozi wa Kiislamu lakini huna uhuru wakumkosoa, kumwacha au kuwa mpinzani wake. Uislamu umeruhusu unyanyasaji, uvamizi na kifo kwa wale wanaotaka kutumia uhuru wao waliyopewa na mungu wakuwapinga au kuwaacha viongozi wao. Kiongozi wa Kiislam yuko kinyume na uhuru. Wale wanaomkosoa kiongozi wa Kiislam wanaishi maisha ya taabu

Sura Al Anfal (8) katika mstari wa 6, 12, 13, 22 na 31 huwaita wale wanaomkosoa kiongozi viziwi, bubu na wanyama wabaya sana; ncha za vidole na vichwa vyao vinapaswa kukatwa. Kuna marejeo 146 ya Jahannamu katika Qur'ani. Marejeo 9 tu kati ya hayo ni ya makosa ya kimaadili kama mauaji, wizi, na kadhalika. 137

yaliyobaki ni kwa wale wanaomkosoa Muhammad au wasiomfuata. Ni kwa sababu hii kiongozi wa Kiislamu anaweza kufanya maisha ya wapinzani wake kuwa kama jahannamu..

## Ubaguzi dhidi ya wasio Waislamu

Maisha ya wasiokuwa Waislamu yanakuwa mabaya zaidi chini ya uongozi wa Kiislam. Sura Al-e Imran (3) katika mstari wa 110 unasema; Waislam ni bora zaidi kuliko wasio Waislamu. Sura Al-A'raf (7) katika mistari ya 176 na 177 na Sura Al Anfal (8) katika mstari wa 55 inasema kwamba wale wasiojiunga na Uislamu ni mbwa na wanyama wabaya sana. Sura Nisa (4) mstari wa 89 inasema: Msiwafanye marafiki miongoni mwao mpaka wahame kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu na wakikengeuka basi wakamateni na waueni popote mnapo wapata;. Sura Al Fath (48) katika aya ya 29 inasema kwamba Muhammad ni mtume wa Mwenyezi Mungu; Na wale walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Kwa hiyo wasio Waislamu hawawezi kuwa salama mikononi mwa kiongozi wa Kiislam.

## Kiongozi wa Kiislamu anaagizwa kuwatengenezea matatizo mataifa mengine

Sura Al-e Imran (3) katika mstari wa 85 inasema: Hakuna dini nyingine itakayokubalika isipokuwa

Uislamu. Sura Al Ahzab (33) katika aya ya 27 inasema: Mwenyezi Mungu aliwapa Waislamu ardhi, makao na utajiri wa wasio Waislam kwa ajili ya urithi - hata nchi ambayo waislamu hawakuwahi kukanyaga: kwa maana nguvu za Mwenyezi Mungu ni sawa na vitu vyote. Sura Al Anfal (8) katika mstari wa 39 inasema: Kwa hivyo piganeni na makafiri mpaka wasiwepo wasioamini tena na wote wajisalimishe kwa dini ya Mwenyezi Mungu pekee.

Unaona kwamba kiongozi wa Kiislamu ana haki ya kisheria kabisa kutoka kwa uislamu kuwa adui wa ulimwengu. Hivyo kiongozi halisi wa Kiislamu ana haki kutoka kwa Uislamu sio tu kupuuzia uhuru wa familia yake, watu na ulimwengu, lakini pia kuilazimisha imani yake kwa wengine.

Kwa kulinganisha na mitindo mingine yote ya uongozi duniani, uongozi wa Kiislamu ni mtindo wa uongozi usio na maendeleo na uwajibikaji. Kwa nini uongozi wa Uislamu haujali uwajibikaji na hauna maendeleo? Kwa sababu, uwajibikaji, unahitaji kuheshimu uhuru wa watu wa kuchagua katika mahusiano. Lakini kama tulivyojifunza kutokana na mistari ya Qura'ni, hakuna mtu aliye na uhuru wa kuchagua ikifika kwa maamuzi ya Muhammad.

## Ubora sio muhimu kwa kiongozi wa kiislamu bali nguvu

Katika Hadith ya Dawud Namba 2527 ya Kitabu cha 14 Muhammad alisema kuwa vita kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni jambo la lazima kwa Waislam chini ya kila kiongozi wa Kiislamu, iwe ni mwenye imani au la; Sala pia ni jambo la lazima kwa Waislamu wote chini ya kiongozi wa Kiislamu, hata kama kiongozi huyo ni mwaminifu au mwasi hata kama ametenda dhambi ya mauti. Unaweza kuona kwamba watu wamenyimwa nafasi yao ya kuepukana na watawala ambao hutenda dhambi za mauti.

Huu siyo uongozi bora bali ni uongozi wa wenye kui ya madaraka ambao huwalazimisha watu kuwafuata pasipo maswali. Kwa hiyo kigezo cha uongozi katika Uislam ni kutumia nguvu na sio ubora wa kiongozi unaomfanya astahili cheo cha uongozi

Kiu ya madaraka husababisha kiongozi kupuuza uwezo wa watu kufanya maamuzi yao binafsi kuhusu maisha yao wenyewe. Kiu ya madaraka humpotosha kiongozi nakumfanya ashindwe kuelewa kwamba wanadamu wanaweza kuboresha hali zao tu, kwa kutumia majadiliano na busara. Kiu ya madaraka pia humpotosha kiongozi na kumfanya afikiri kwamba anahitaji maoni na uzoefu wa wengine kwa ajili tu ya kuboresha ustawi wake mwenyewe. Kiu ya madaraka

hufanya kiongozi ashindwe kuelewa kwamba lazima awajibike kwa jamii yake ambayo imemweka katika nafasi hiyo. Bila shaka kiu ya madaraka itadidimiza shauku ya kujenga mahusiano ya kweli na jamii yake, na pia itamfanya asiaminiwe na kuogopwa. Na hofu hio itapelekea watu kushindwa kuwasilisha mawazo yao. Watu hawataweza kuaminiana tena, na hivyo mlango wa ubunifu na maendeleo utafungwa pia. Ndiyo maana hakuna ubunifu au maendeleo katika nchi yoyote ya Kiislamu inayoendeshwa na viongozi halisi wa Kiislamu. Ukosefu wa ubunifu pia utafunga mlango wa mafanikio na faraja.

## Kiongozi wa Kiislamu anatarajia watu wamtii tu

Neno "Uislamu" linamaanisha utii kwa Kiarabu. Uupende Uislam au la, huna chaguo bali kutii katika kila kipengele, iwe kiroho, kijamii au kisiasa. Ikiwa hutaki, basi unachukuliwa kama kafiri, lazima ushugulikiwe kulingana na maelekezo ya Sharia ambayo hunyima haki sawa, au mateso ikihitajika au kupoteza maisha yako.

## Uongozi katika Kristo misingi yake ni upendo, huruma na ushirikiano.

Uongozi katika Yesu Kristo ni wa tofauti na uongozi wa Kiislamu katika kila nyanja. Uongozi katika Kristo

unathamini uwepo wa wote, marafiki na wengine. Marafiki na wengine ni sawa machoni pa Mungu ambaye Kristo anamdhihirisha (Soma Mathayo 5: 43-48; Wagalatia 3:28; Kutoka 23: 9, 22:21). Upendo na wema ni vipaumbele vikuu vya uongozi katika Yesu Kristo (soma 1 Yohana 4:19).

Uongozi katika Kristo sio wa kutawala, bali ni mlango wa mafanikio na maisha bora zaidi ili kila mtu ahimizwe kuendelea kufanya kazi na wengine kwa upendo, fadhili na ushirikiano. Uongozi katika Kristo huwaleta watu, marafiki na wageni, kwa uaminifu ili wote waweze kuzalisha mambo mazuri. Ni uongozi wa ushirikiano ambao kila mtu anaweza kutoa maoni yake, iwe ni mawazo ya kumpinga au kumuunga mkono kiongozi (2 Timotheo 2: 24-25; Kumbukumbu la Torati 18:22; Isaya 1:18) kwa vile lengo sio chuki bali kupata vidokezo vya kufikia mafanikio.

## Uongozi katika Kristo umejikita katika utumishi zaidi

Injili inapingana na ukatili na kuchochea usawa na uhuru. Yesu alisema: Yeyote anayetaka kuwa mkuu kati yenu, na awe mtumishi wenu .... Mwana wa adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumikia, na kutoa maisha yake kuwa faida ya wengi (Mathayo 20: 25-28). Yesu

pia alisema: Ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.(Yohana 13:14, ESV).

### Uongozi katika Kristo ni wa amani kwa wote

Kama nilivyokwisha kusema mara kwa mara, Injili inasema: Hapana Myahudi wala myunani, hapana mtumwa wala aliye huru, hapana mtu mume wala mtu mke; kwa maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu (Wagalatia 3:28, KJV). Pia inasema: Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote (waebrania12: 14, NIV); Haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgonvi; bali kuwa mwanana wa watu wote, awezaye kufundisha: mvumilivu akiwaonya kwa upole wao washindanao naye ili kama ikiwezekana Mungu awape kutubu na kuijua kweli. (2Timotheo 2: 24-25, NIV); Yeyote asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo (1 Yohana 4: 8, NIV). Hizi ni sifa za uongozi katika Yesu Kristo.

### Unashauku ya kumfuata kiongozi gani ndani ya moyo wako?

Kiongozi wa Kiislam ambaye kipaumbele chake ni wafuasi wake kumtii bila sababu, na wasipojisalimisha hupoteza kila kitu. Au uongozi ndani ya Kristo ambapo kiongozi anaagizwa kuwa mtumishi wako na watu

wana uhuru wa kutoa maoni yao, iwe ni ya kupendeza au ya upinzani, bila shida yoyote? Yesu Kristo ni wa kipekee katika kila nyanja, hata katika uongozi. Fuata uongozi wake.

**Wakati wa kutafakari 12**

1. Imani za watu zina umuhimu gani katika kutengeneza maadili ya maisha yao, ikiwemo uongozi?
2. Ni sifa gani za kiongozi bora?
3. Je! Unapenda kuwa kiongozi mzuri (baba au mama) kwa familia yako na kuwa na kiongozi mzuri katika jamii yako?
4. Kuna ugumu gani wa kutambua imani ambayo ina vigezo bora vya uongozi?
5. Kuna faida gani za kiongozi mnyenyekevu?
6. Je! Unapata mfano bora wa uongozi katika Yesu Kristo au la? Kwa nini?
7. Kuna umuhimu gani wa kumfuata Yesu Kristo kama Yeye ni mfano bora wa uongozi? Je, itaathiri vipi mahusiano yako na familia yako na wengine?

## Sharia ya Uislamu au Upendo wa Kristo -kipi ni mfumo bora zaidi?

Hakuna shaka kwamba kila imani katika ulimwengu huathiri maisha na mahusiano ya wafuasi wake na kuanzishwa kwa sheria katika jamii hiyo. Uislamu pia umeathiri maisha, uhusiano na sheria za jamii za kiislamu kwa njia ya "Sharia" yake ambayo imetoa misingi yake kutoka kwenye Qura'ni, maisha ya Muhammad na maneno ya Muhammad na wafuasi wake.

Sharia inaonyesha njia ya maisha kwa kila mwislamu. Inawafundisha Waislamu kwamba mfano wa Muhammad lazima utawale mataifa yote na kuwafanya kuwa Waislamu katika kila nyanja. Katika ngazi ya kifamilia baba au mume wa familia hupewa wajibu wa kuanzisha kanuni za Sharia, na katika ngazi ya nchi na kimataifa inawajibu wa serekali kutekeleza kanuni za Sharia. Mifano ya kanuni hizi ni sheria kuhusu chakula, mitala, umri wa ndoa, kutotii, ukosoaji, kiwango cha adhabu, pombe, uzinzi, makafiri, Jihadi, nk.

### Lengo kuu la Sharia ni Kutaka kila kitu na mtu awe mwislamu

Sharia ina masharti. Hauna usalama ikiwa hufuati Uislamu. Lakini mkazo mkuu katika njia ya Yesu Kristo

ni upendo usio na masharti. Huu upendo usio na masharti huathiri maisha, mahusiano na sheria za wafuasi wa Yesu Kristo ili kuwaandaa kwa ajili ya amani na wengine.

Injili ya Kristo inasema katika kitabu cha 1 Wakorintho sura ya 13 mstari wa 1 na 2: nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, mimi nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. tena nijapo kuwa na unabii, na kujua siri zote namaarifa yote, nijapo kuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima kama sina upendo, si kitu mimi. (ESV)

Ndugu zangu, kitabu chenye upendo wa ajabu sana na upole kinakataliwa na viongozi wa Kiislam kwa sababu tu jina la Muhammad halipo ndani yake. Hawajui kwamba upendo kama huo kutoka kwa Mungu wa kweli ni bora kuliko majina ya manabii wote.

Nitawapa mifano kutoka Sharia ya Uislamu na kuilinganisha na Injili ya Kristo. Kisha wewe mwenyewe utafurahi kujua kwa nini jina la Muhammad haliwezi kuwa katika Injili.

## Kati ya, Sharia ya Uislamu au Injili ya Kristo, ni kipi kinaheshimu familia vizuri zaidi?

Familia ni kitu muhimu sana kwa Mungu kwani alianza ulimwengu na familia, Adamu na Hawa. Lakini katika Sharia ya Uislamu, mume ni bora kuliko wake

zake na anauwezo wa kuwapiga. Sura Al Baghara (2) katika mstari wa 228 inasema kwamba wanaume wana manufaa zaidi kuliko wake zao. Ni kwa sababu ya manufaa haya Sura An Nisa (4) mstari wa 34 na Sura Sad (38) mstari wa 44 zina wapa haki ya kuwapiga wake zao. Sura Nisa (4) katika mstari wa 15 na 16 pia inasema kwamba wanaume wana haki ya kuwafungia wake zao kwenye chumba kwa kosa la uasherati mpaka wafe. Lakini kwa uasherati huo huo, wanaume huchapwa viboko na kuwa huru.

Kwa nini Qur'ani inampa mume mamlaka juu ya wake zake na kumpa haki ya kuwapiga wake zake na kuwaua? Sababu za Qura'ni ni kama zifuatavyo:

Sura An Nisa (4) aya ya 34 inasema kwamba Mwenyezi Mungu amewapa wanaume uwezo zaidi wa kutawala wanawake na kuwaamuru watii. Matoleo mbalimbali ya Qur'ani yanasema kwa mfano, katika Sura Al Ahzab (33) mstari wa 23 kwamba kati ya Waislamu, wanaume pekee ndiyo wamekuwa waaminifu kwa agano lao na Mungu. Kwa maneno mengine, wanawake hawawezi kutimiza agano lao na Mungu na daima wanahitaji kurekebishwa na wanaume.

Muhammad nabii wa kiislamu pia anatoa sababu yake kwa nini wanaume wana haki zaidi kuliko wanawake? Alisema katika Hadith ya Al Bukhari Namba 301, katika kitabu cha 6 toleo la 1 kwamba Wanawake wana upungufu wa akili.

We unaonaje? Je! Kweli unafikiri kwamba wanaume wanatimiza agano lao na Mungu vizuri zaidi kuliko wanawake? Je! haimaanishi, "Usimwamini mama na dada yako?"

Kwa mujibu wa Qur'ani, wewe, kama mvulana au mwanaume, unachukua thamani ya mara mbili zaidi kuliko dada yako au mama yako katika kushuhudia au kupokea urithi. Hii ina maana kwamba kama mama au dada yako atakujulisha kitu fulani, hupaswi kumwamini isipokuwa tu mwanamke mwingine akishuhudia jambo hilo hilo. Lakini kama baba yako au kaka au mwanaume akishuhudia jambo fulani, anaweza kuaminiwa. Jaribu kufikiria kwamba katika jamii ni wanaume tu wanaoaminiwa na sio wanawake!

*Wasomi maarufu wa Kiislam wanasema wanawake wamepotoka*

Hadith namba 113 ya Bukhari katika toleo la 7 inasema kuwa mwanamke aliumbwa kutoka kwenye ubavu wa mwanamume, akiwa amepotoka. Kupotoka huku ni asili yao ya kudumu na haiwezi kuponywa. Hadith ya waislamu namba 3467 katika Kitabu cha 8 inasema kwamba mwanamke aliumbwa kutoka kwenye ubavu na kwa vyovyote hawezi kuwa sawa au kunyooshwa kwa ajili yenu; hivyo kama unataka kufaidika na yeye, faidika naye wakati upotofu umebaki ndani yake. Na kama ukijaribu kumnyoosha, utamvunja, na kumvunja maana yake ni kumtaliki. Hadith ya Davud namba 2155

katika kitabu cha 11 inasema kwamba Muhammad alisema: Ikiwa mmoja wenu ameoa mwanamke au amenunua mtumwa, asema hivi: "Ewe Mwenyezi Mungu, nakuomba kwa mema yaliyo ndani yake, na kwa tabia uliompa; Ninakimbilia kwako kujikinga na uovu uliyo ndani yake, na kwa tabia hiyo uliyompa. " ....

Hadith namba 219 ya Bukhari, katika kitabu cha 88 na toleo la 9 inasema: Wakati Muhammad aliposikia habari kwamba watu wa Uajemi walimfanya binti wa mfalme Khosrau kuwa Mfalme wao (mtawala), alisema, "Halitafanikiwa kamwe taifa kama hilo linalofanya mwanamke kuwa mtawala wao. "

Kwa kuwa Muhammad na Qur'ani waliwatambulisha wanawake kama viumbe waovu, waandishi wengine watasema nini kuhusu wanawake?

Sura Al Room (30) katika mstari wa 21 inasema kuwa wanawake wameumbwa kwa ajili ya wanaume. Fakhraldin Razi (1149 AD) mwanafilosofia wa Sunni katika kitabu chake cha ufafanuzi At-Tafsir al-Kabir wakati akizungumza juu ya aya hii alisema: "aliumbwa kwa ajili ya mwanamume" ni ushahidi tosha kwamba mwanamke ni mnyama. Hadi Sabzevari (1797) mwanafalsafa wa Shia katika ufafanuzi wake Sadr al-Mota'aleghin anasema: Ni kweli na nisawa kabisa wanawake ni kati ya wanyama bubu. Wana asili ya wanyama.

Ni ajabu sana kwamba waandishi hawa waliheshimiwa na kuitwa wanafalsafa na kupokea heshima kubwa kutoka kwa serikali zao hadi sasa.

Injili ya Kristo haisemi mambo yakuvunja moyo kama hayo juu ya wasichana na wanawake.

## Mume na mke ni sawa machoni pa Mungu wa Injili

Injili inasema katika kitabu cha Wagalatia sura ya 3 mstari wa 28 kwamba mume na mke wana thamani sawa kwa Mungu. Katika kitabu cha Waefeso sura ya 5 mstari wa 25 na 28 inasema kwamba mtu anapaswa kumpenda mkewe kama mwili wake mwenyewe. Katika kitabu cha Wakolosai sura ya 3 mstari wa 19 inasema: Ninyi waume, wapendeni wake zenu, na msiwe na uchungu nao. Na katika kitabu cha 1 Petro sura ya 3 mstari wa 7 unasema kwamba wake ni warithi wa neema ya uzima pamoja na waume zao. Sala za wanaume hazitakubaliwa ikiwa hawawaelewi na kuwaheshimu wake zao.

Huu ulikuwa ulinganifu kati ya nafasi ya wanawake kwenye dini ya kiislamu na nafasi ya wanawake katika Ukristo. Je! Unadhani ni dini ipi inapaswa kuitwa dini kamilifu?

Sasa hebu tuone ajabu ya jinsi familia inavyochukuliwa katika  Sharia ya Uislamu

## Sharia inawataka watoto kutotii walezi wao

Sura Al Tawba (9) katika mstari wa 23 inatuambia kwamba watoto wa Kiislamu hawapaswi kukubali uangalizi wa baba zao au ndugu kama walezi wao wanapenda maadili mengine zaidi ya maadili ya Uislamu

Unajua kwamba watoto wa familia walio kuwa hawahitaji ulezi, ila watoto wadogo. Hapa katika aya hii Qur'ani inawaagiza watoto wadogo kutowatiii walezi wao ikiwa si Waislamu wema. Je, utafurahi ikiwa mtu anawashawishi watoto wako kupuuza malezi yako kama baba au mlezi? Hiyo ndivyo Qur'ani inavyofanya.

Kama unavyojua, kuna upendo unaounganisha hata ya wanyama na vichanga vyao, kama ilivyo kati ya wazazi na watoto wao. Hata mtu asiye mcha Mungu anawapenda watoto wake. Hii ni kwa sababu Mungu ametuumba sisi kupendana. Upendo huu unatoka kwa Mungu. Mungu wa kweli hawezi kuwafundisha watoto kupuuza wazazi wao.

Unaona jinsi Sharia inapingana na upendo wa asili unaotoka kwa Mungu. Ikiwa sasa Sharia huwatendea ukatili huu wanafamilia wa kiislamu, unadhani itafanya nini kwa wasio waislamu? Hebu tuone mafundisho ya Sharia ya Uislamu kuhusu wasio Waislamu.

**Sharia inachukulia wasio Waislamu kama si wanadamu.**

Qura’ni inasema wasiyo Waislamu ni najisi. Hii ndiyo sababu wasio Waislamu wanaofanya kazi huko Saudi Arabia wanapaswa kukaa umbali wa kilomita 24 kutoka Makka. Tena hii ndiyo sababu kwa nini waislamu wengine hawana jinsi ila kunawa mikono yao baada ya kusalimiana na wasio Waislamu. Au, ikiwa wameletewa chakula na maji na wasio Waislamu, huosha sahani na glasi zao kwa staili ya Kiislamu. Nilifundishwa tangu utotoni, ya kuwa ikiwa tu ukigusana na mtu asiye Mwislamu tulitakiwa kujiosha kwa staili ya Kiislamu ili kujitakasa.

Qur'ani pia inawaita wasio Waislamu wabaya kuliko wanyama, mbwa, nguruwe, nyani na punda. Kuwaita wengine kama wanyama ni kumwasi Mungu, binadamu na hata Ibrahimu ambaye anaitwa baba wa Wayahudi na Waarabu: Muhammad na Wayahudi ni wazawa wa Ibrahimu. Mungu, ambaye alimpenda Ibrahimu, anawezaje sasa kusema mbele ya uso wake kwamba watoto wake ni wanyama? Je, mjukuu, Muhammad, angewezaje kumwambia babu yake Ibrahimu kwamba wajukuu wake kutoka kwa Isaka walikuwa wanyama, na wajukuu kutoka Ishmaeli tu ndiyo walikuwa wanadamu? Je, hili si jambo la dharau kwa babu Ibrahimu ambaye anawapenda wajukuu

wake wote? Kwa kuwaita wayahudi wanyama ni kama unamwambia babu yao alizaa wanyama.

*Sharia huwaita wasiokuwa Waislamu wanyama ili kuhalalisha mauaji yao*

Sura Al Anfal (8) katika mstari wa 39 inasema: Wachinjeni wale wasio Waislamu mpaka isiwepo fitina na mateso na dini yote iwe kwa ajili ya mwenyezi Mungu. Hiki ndicho kichocheo cha ugaidi dhidi ya wasio Waislamu kinachofanyika katika nchi nyingine za Kiislamu. Qur'ani inawaita wasio Waislamu makafiri na inasema kwamba wanaweza kuchukiwa, kuchekwa, kudanganywa, kupangiwa njama dhidi yao, kufanywa watumwa, kuteswa na kuuawa ikiwa hawafuati Uislamu.

Aina hii ya mitazamo na vitendo hukataliwa kabisa katika Injili ya Kristo. Mungu mwenye upendo, huruma na fadhili hawezi kuwaagiza wafuasi wake kuwaangamiza wengine kwa sababu ya imani zao. Ndugu zangu, hakuna mstari hata mmoja katika Injili nzima ya Yesu Kristo unaohamasisha chuki au mauaji. Huwezi kupata mstari kama huo kamwe. Kwa nini? Kwanza, kwa sababu Mungu hufurahia maisha ya viumbe wake sana. Pili, kwa kuwa hatukuwaumba watu, kwa hiyo hatuna mamlaka juu ya maisha yao.

Haiwezekani kujenga amani katika familia au katika jamii na chuki na uhasama wa Sharia, lakini

inawezekana kwa upendo na wema wa Kristo. Hivyo upendo wa Kristo ni mfano bora kwa mahusiano ya kibinadamu, na si Sharia ya Uislamu.

**Wakati wa kutafakari 13**

1. Je, tunaweza kuwa na urafiki wa kudumu katika familia zetu au na watu wengine kwa njia ya ukali, ubaguzi au uadui?
2. Je, itawaathirije watoto wetu tukifuata Sharia na kuwa wakali kwa wenzi wetu?
3. Je, mtu anaweza kuwa mfuasi wa kweli wa Mungu au wa nabii kwa nguvu na vurugu?
4. Je! Mungu anahitaji nguvu kuwashawishi watu, kama yeye ndiye chanzo cha hekima yote si anauwezo wa kuwashawishi watu kwa kutumia busara?
5. Je! Mungu anahitaji kutumia nguvu kuwafanya watu wafuasi wake licha ya kuwapa uhuru wa kuchagua?
6. Kwa nini upendo wa Kristo unazidi kanuni za Sharia?
7. Je, unahisi kuwajibika na kuwashirikisha wengine upendo wa Kristo?

## Binadamu wanahitaji Marafiki na sio Maadui

Je, unakubaliana na mimi? Ikiwa ndiyo, basi tunahitaji kujua jinsi na kwa njia zipi tunaweza kujenga marafiki wa kudumu.

Kama ambavyo haifai kwetu kuwa na maadui, si vizuri pia kwa wengine kama tutakuwa adui zao. Ni dhahiri kwamba hatuwezi kujenga urafiki wa kweli kwa kutumia hasira, chuki, uadui, udanganyifu, uongo au njia nyingine zozote zisizofaa. Njia zisizofaa ni njia za vita dhidi ya haki za wengine. Tukipuuza haki za wengine, hatutaweza kujenga urafiki nao. Urafiki unahitaji kuheshimiana, wema, kujitoa, msamaha, uvumilivu na kujidhibiti.

Yote haya yanatuambia kwamba tunahitaji kukaa mbali na mtu yeyote au imani ambayo inatufundisha chuki, hasira, unyanyasaji au tabia yoyote isiyofaa kwa wenye fikra tofauti na zetu. Tunahitaji kukaa mbali nao kwa sababu sio tu wanaharibu urafiki katika jamii zetu lakini pia katika familia zetu.

**Kuchukia wengine ni zaidi ya chuki.**

Kupanda mbegu ya chuki katika moyo wako, ni kuipanda katika familia yako pia. Nikupe mfano. Nabii wa Uislamu aliwahimiza Waislamu kuwachukia

wapagani na wafuasi wa dini nyingine. Chuki hio ilikuwa motisha wa kuwalazimisha wote wasio Waislamu katika Peninsula ya Arabia kuwa Waislamu na pia kuwaua wale ambao hawakujiunga na Uislamu. Saudi Arabia yote iliwekwa chini ya imani ya kiislamu na hapakuwepo na wasio Waislamu waliobaki wakiwachukia. Je! Chuki hio ilipotea? Hapana chuki iliyopandwa ndani ya mioyo ya Waislamu dhidi ya wasiokuwa Waislamu katika harakati za mwanzo za Uislamu, ilizaa matunda ya chuki kati ya watoto wa Kiislamu wenyewe, ikagawanya familia ya Muhammad, ikaleta na uadui miongoni mwa vizazi vya baadaye vya Kiislamu. Chuki hio ilisababisha mgawanyiko wa Sunni na Shia vikundi ambavyo vimekuwa vikimwaga damu ya kila mmoja kwa miaka 1400 tangu ujio wa Uislamu.

Je, si jambo la ajabu? Unafikiri kwa kupanda mbegu ya chuki ndani ya moyo wako dhidi ya wengine utawaumiza wengine tu, lakini haiko hivyo. Utajiumiza mwenyewe na familia yako pia. Chuki huwafanya watu kuwa wapinzani na pia humlisha sumu mchukiaji. Ndiyo maana Yesu Kristo anasema katika Injili yake kwamba hatupaswi kuwachukia hata adui zetu, bali tuwapende na kuwaombea.

Kwa bahati mbaya, Uislamu hufungua mlango mpana wa chuki na vurugu katika kila ngazi ya uhusiano kwa

Waislamu, na hivyo hii huwa tishio kwa upendo wa kweli na heshima.

## Kupiga mke ni vibaya kwa kila mmoja katika familia

Mwislamu anapofuata amri ya Qur'ani na kumpiga mama wa watoto wake, watoto wa mama huyo hawatajifunza upendo na heshima kutokana na ukatili wa baba yao dhidi ya mama yao bali watapata uchungu na hasira. Hasira na uchungu huo utaathiri tabia za watoto na kuwafanya wasiwe na uhusiano mzuri wao wenyewe na hata na wengine.

Ikiwa Qur'ani ingefundisha familia upendo wa kweli, upendo huo wa kweli kati ya mume na mke usingemfanya mmoja kuwa bora kuliko mwingine, bali ungewafanya mwili mmoja na kwa umoja huo wangeweza kupendana kama miili yao wenyewe licha ya tofauti zao. Mikono, miguu, macho, vyote viungo vya mwili mmoja japo vina tofautiana. Vyote vinabeba thamani sawa kwenye mwili, kupendana na kusaidiana kufanya kazi kwa umoja ili kuunda mwili mmoja wenye afya. Watu wa familia moja pia lazima wawe viungo vya mwili mmoja. Ikiwa mume anampiga mkewe familia yake haiwezi kuwa familia nzuri na yenye upendo. Kwa hiyo, huwezi kuwa na familia inayojali na yenye upendo na mafanikio isipokuwa ukikubali na kutekeleza misingi bora ya kifamilia. Hii ina maana

kwamba unahitaji kwanza kuwa mtu mwema, mwenye heshima zaidi, mwenye fadhili na kumsamehe mwenzi wako ambaye ana jukumu muhimu katika kuendesha familia pamoja nawe.

Ukweli ni kwamba Yesu Kristo pekee ndiye anayeweza kukupa misingi bora ya kifamilia na kuleta umoja huo. Ndoa kwa mtazamo wa Injili ya Yesu Kristo ni mfano wa umoja kati ya mume na mke ambao huonyesha ubora wao wa kweli. Kwa Yesu Kristo, ndoa sio kumfanya mume kumtawala mke wake, bali ni mume kuwa mtu mwenye hofu ya mungu ambaye ana huruma na upendo zaidi kwa mke wake kama atakavyo fanya kwa mwili wake mwenyewe.

Tuliona katika sura zilizopita jinsi wasomi maarufu wa Kiislamu wanavyo washusha hadhi wanawake katika familia na kuwafananisha na wanyama. Ikiwa Qur'ani haikuwapa ruhusa ya kuwapiga wake zao, wasingeweza kuwaita wake zao wanyama, na kuhalalisha tabia zao mbaya.

Kwenye familia unahitaji marafiki na si maadui. Kwa kuwa mbabe kwa mke wako au kumpiga, huwezi kutengeneza urafiki. Ni kwa sababu hii, unahitaji kuachana na Qura’ni na kuifuata Injili ya Yesu Kristo.

**Mitala ni sababu ya utengano na uadui.**

Qur'ani pia inakuwa chanzo ya utengano na chuki katika familia kwa kuhalalisha mitala. Unapofuata utaratibu wa Qura'ni na kuwa na mke zaidi ya mmoja, hii husababisha kukosa maelewano, chuki na wivu kati ya wanafamilia wako.

Kama Mwislamu unaweza kusema, "kweli, mitala hujenga ugomvi, pale tu ambapo mume asipotenda haki sawa kwa wake zake wote; ikiwa mume anatenda haki sawa kwa wote, hakutakuwa na shida yoyote." Je, ni kweli? Waislamu wanaamini kwamba Muhammad alikuwa na uwezo kamili wa kutenda haki katika familia yake. Ikiwa ndivyo, kwa nini hapakuwa na maelewano kati yake na wake zake?

Nikupe mfano kutoka kwenye Qur'ani: Sura Al-Tahrim (66) inaongelea juu ya mvurugano uliyokuwepo kati ya Muhammad na wake zake. Unaona kwamba hata mtu mwenye haki zaidi katika Uislamu hakuweza kuwa na maisha ya furaha na ya upendo na wake zake.

Kutoka mwanzo wa uumbaji, Mungu alijua kwamba mitala haitajenga upendo na urafiki. Vinginevyo, angeweza kuwaumba kina Eva wengi kwa ajili ya Adam. Lakini alimuumbia Adamu mke mmoja na Hawa kamuumbia mume mmoja. Mimi mwenyewe nimetoka kwenye familia yenye wake wengi, na pia

nimeshuhudia familia nyingine nyingi za Waislamu ambazo zina matatizo zaidi kwa sababu ya wake wengi. Mitala hujenga ugomvi na uadui. Hii sio tu hujenga matatizo kati ya wanandoa, lakini pia ndani ya mahusiano ya familia.

Tunapaswa kujihusisha na Injili ya Yesu Kristo ambayo huleta umoja, upendo na urafiki katika familia pale mume na mke mmoja wanapoungana na kupendana kwa moyo wote.

**Kuwafundisha watoto kutokuwaheshimu walezi wao ni sumu kwa urafiki**

Qur'ani pia inajenga uadui kwa kuwahimiza watoto kutokuwaheshim baba zao na kupuuza wazazi wao. Haya sio maadili mazuri. Watoto wanapaswa kuwaheshimu wazazi wao.

Qura'ni katika Sura Al Tawba (9) mstari wa 23 inasema kwamba hupaswi kumheshimu baba yako ikiwa sio mwaminifu kwenye Uislamu. Utaratibu huu wa Qura'ni hautajenga familia yenye afya. Baba yako anastahili heshima yako. Amefanya kazi kwa bidii, na kukupa chakula mchana na usiku ili uweze kukua na wewe uwe baba au mama wa baadaye. Je! Unaweza kutarajia huruma ya watoto wako ikiwa wewe unamkataa baba yako mwenyewe kwa sababu hajajisalimisha kwa imani yako au anafikra tofauti na imani yako? Kwa upande

mwingine, unawezaje kutarajia urafiki na wengine wakati una chuki na baba yako, ambaye yuko karibu yako kuliko wengine?

Nikuulize swali lingine. Je, baba yako hakuumbwa na Mungu na uhuru wa kuchagua imani yoyote anayoipenda? Huna haki ya kumdharau baba yako. Mheshimu bila kujali anachokiamini. Ubaba na ulezi ni vitu vya muhimu sana kwa Mungu wa Biblia. Mungu ametumia mfano wa baba na mama katika Biblia nakutuambia kwamba anatupenda kama mama au baba. Mungu wa kweli hawezi kukuagiza umdharau baba yako na uwe adui yake.

Kwenye familia unahitaji marafiki na si maadui. Kwa sababu hiyo, unahitaji kuepukana na mafundisho haya ya Qur'ani na kuheshimu uhuru wa wanafamilia wako kwa imani yoyote watakayo ichagua. Ukweli ni kwamba, utakuwa kinyume na Mungu, ikiwa huthamini uhuru wa wengine wa kuchagua ambao wamepewa na Mungu kama unawalazimisha imani yako.

### Kuwaua wengine kwa sababu ya imani zao kunafunga mlango wa urafiki

Pia, unapofuata amri ya Qur'ani na kuwaua jamaa na majirani zako wasio waislamu, inamaanisha kwamba unafunga mlango wa urafiki na unaufungua mlango wa

chuki, kulipiza kisasi na uadui. Chuki hii haina mwisho. Ukatili kati yako na wengine hautakaa uishe, isipokuwa pale tu wewe na familia yako mtakapo ondoka na kuuacha Uislamu, nakufuata imani yenye upendo na kuwaheshimu majirani zako, kama wewe mwenyewe. Vinginevyo, tabia yako ya kiadui itaathiri vibaya ujirani wako itafunga mlango wa urafiki wa kweli na kujaliana

**Kujiona kuwa bora kuliko wengine ni kikwazo kwa urafiki**

Qur'ani pia hufundisha kwamba wewe ni bora kuliko wengine. Mafundisho kama haya kamwe hayawezi kuruhusu uwepo wa urafiki wa dhati katika maisha yako. Qur'ani inasema katika Sura Al-Imran (3) mstari wa 110 kwamba Waislamu ni bora zaidi kuliko wale wasio Waislamu.

Unawezaje kuwa bora kuliko Myahudi au Mkristo au wengine, ikiwa wewe pia ni mwenye dhambi kama wao? Je! Mwenye dhambi anawezaje kuwa bora zaidi kuliko watenda dhambi wengine? Wenye dhambi wote ni sawa machoni pa Mungu. Kwa upande mwingine, urafiki wa kweli unahitaji unyenyekevu, wema na usawa vitu ambavyo Qur'ani inavipuuza. Ni kwa sababu hii utapingana na upendo katika urafiki ikiwa unafuata Uislamu.

Napenda kumaliza majadiliano yangu kwa kukupa sababu moja zaidi ambayo inaonyesha kwamba Uislamu unafunga mlango wa upendo halikadhalika wa urafiki.

## Muziki na moyo wa upendo

Uislamu unaamuru kuwa hupaswi kunufaika na muziki bali unatakiwa kuupinga. Muziki unatoka kwa Mungu. Muziki ni mlaini na mororo na huandaa mioyo milaini. Uwiano kati ya sauti na sauti za vyombo vya muziki mbali mbali unaleta hisia katika namna nzuri na ya upendo. Muziki kwa ujumla huimarisha urafiki. Muziki ni chakula kwa moyo wenye huzuni. Lakini Uislamu unapingana na njia hizi nzuri. Muziki umehalalishwa katika Biblia ili watu waweze kusherehekea wokovu na mahusiano yao na Mungu.[8]

Mambo yote uliyoyasikia katika ujumbe huu kuhusu Uislamu ni ya mwenendo wa udikteta. Tabia hizo zina lenga kuimarisha udikteta ambao husababisha mlango wa amani, upendo na urafiki kufungwa. Katika uislamu

---

[8] Mwimbieni Mungu, nguvu zetu, nyimbo za furaha, Mshangilieni Mungu wa Yakobo. Pazeni zaburi, pigeni matari, Kinubi chenye sauti nzuri, na kinanda. Pigeni panda mwandamo wa mwezi, Wakati wa mbalamwezi, sikukuu yetu. Kwa maana ni sheria kwa Israeli, Ni hukumu ya Mungu wa Yakobo. (Zaburi 81: 1-4, MKJV)

itakuwa vigumu kwako, kuishi kwa amani na maelewano. Unamhitaji Yesu na Injili Yake.

**Wakati wa Kutafakari 14**

1. kwa nini haiwezekani kuwapata marafiki wa kweli kwa kuwa na hasira, chuki, uhasama, udanganyifu, uongo na njia nyingine zisizo za haki?
2. Kwa nini tunahitaji kuepukana na chuki kwa watu wengine?
3. Ingawa Uislamu unaitwa dini ya amani na wengi, je! hili linaweza kuthibitika kwa hoja?
4. Je, si vizuri kujenga maisha yetu kwenye upendo na wema badala ya chuki na ukatili?
5. Kwa nini tunahitaji kumfuata Yesu Kristo?

## Injili ya Yesu Kristo Ina Maelekezo kamili kwa ajili ya mahusiano

Maagizo haya yameelekezwa kwenye akili, mioyo na dhamiri. Kwa pamoja yana kuthibitishia ubora wake ukilinganisha na misingi mingine. Hili ndilo lengo langu katika mjadala huu; kuwasilisha maagizo ya Yesu Kristo akilini, moyoni, na kwenye dhamiri yako ili kwamba ujue ni jinsi gani yalivyo ya kipekee, na manufaa na uwezo wakubadilisha maisha.

Mahusiano ni sehemu muhimu sana ya maisha ya wanadamu. Ikiwa imani yako haijengi umoja na maelewano kati yenu, itakuwa ni hasara kubwa kuishi kwenye imani hiyo. Imani inatujengea utambulisho na mitazamo katika mahusiano. Kwa hiyo, tunahitaji kuchagua ni imani ipi ya kufuata na ipi ya kuacha. Kwa hivyo ni muhimu kwetu kulinganisha imani yetu na za wengine na kuona kama ina ubora au inahitaji kubadilishwa na iliyo bora zaidi.

### Upendo na wema: Vipaumbele vya Injili katika mahusiano

Niliwaeleza kuwa mafundisho ya Injili ni kamilifu. Hii ni kwa sababu Injili inaamini kuwa upendo na upole ni vigezo muhimu katika kujenga mahusiano mazuri.

Hakuna imani nyingine inayotambua upendo na upole kama misingi ya mahusiano kama vile afanyavyo Yesu Kristo.

Imani zote zinazoamini katika nadharia ya mabadiliko haziwezi kuelezea misingi ya imani tofauti iliyopo kati ya upole na ukatili. Kwa nini? Kwa sababu, kwao kila kitu kinatokea kwa bahati mbaya. Kwa hiyo watu hawana nafasi ya kuchagua upendo na upole kama vigezo vya msingi katika mahusiano yao. Imani hizi zinazipa nguvu za asili uhuru wa kuchagua na kuwafanya watu wasiwe na nguvu. Utafiti, tathmini na maamuzi bunifu haviwezekani. Ukweli ni kwamba havitokei kwa bahati mbaya, ila vina tokea kwa maneno tunayosema na mitazamo tunayo ionyesha.

Katika imani kama za kisasa, kutoamini dini, Uhindu, Ubuddha na nyingine, kila mtu anachukuliwa kuwa sawa na Mungu. Upendo na upole vina kuwa vyombo vya ubinafsi na kutumika kwa manufaa binafsi.

Hebu fikiria katika familia, pale upendo na upole wa mume unapokosekana kwa mke wake na mke kwa mume wake au watoto kwa wazazi wao, kwa sababu kila mmoja amefundishwa kuwa Mungu na kufuata njia yake mwenyewe. Familia au jamii yenye maadili ya kibinafsi kama hayo huleta machafuko. Kamwe ubinafsi wa mume au mke au mtoto au kiongozi hauwezi kuleta amani katika familia au katika jamii. Ni

misingi ya mfano mzuri ambayo kiwango chake kinapita misingi mingine yote inayo weza kuleta amani.

Katika Uislamu upendo na upole viko chini ya mamlaka ya kiongozi wa Kiislamu. Kwa hiyo upendo na upole havitawali katika Uislamu, bali uamuzi na nguvu za mamlaka hutawala. Kwa hiyo, hakuna mtu katika Uislamu, hata Muhammad, anayeweza kuwa mfano wa upendo na upole kwa vile madaraka na nguvu vinafanya upendo na upole viwe na masharti.

## Yesu: mfano kamili wa upendo na fadhili

Yesu pekee anaweza kuwa mfano wa upendo na fadhili kwako, katika mahusiano yako na familia yako na wengine. Kwa nini? Napenda kwanza kuuliza maswali kadhaa na kisha kukupa sababu za hili.

Wewe unadhani anayepaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa upendo na upole anapaswa kuwa na tabia gani? Tafsiri sahihi ya mfano wa kuigwa ni upi?

Mfano huu wa kuigwa lazima awe mtu ambaye huuonesha kwa matendo upendo na upole uliyo tukuka kwa wote, marafiki na wapinzani. Kwamarafiki, kwa sababu urafiki wa kweli ni upendo na upole; kwa wapinzani, kwa sababu wanaweza kuchukua nafasi kutulia kidogo, ili waelewe kwamba upinzani sio kubomoa ila ni kuleta njia bora zaidi ya amani ya

kurejesha mahusiano ya amani. Hakuna dini wala falsafa inayoleta mfano wa kuigwa kama huo kwa ulimwengu, ila Injili ya Yesu Kristo. Mfano wa kuigwa ni Yesu Kristo Mwenyewe.

Injili ya Yesu Kristo inasema kuwa Mungu ni upendo. Mungu asinge kuwa upendo, basi ujumbe na mjumbe wake pia wasingeweza kuwa na upendo. Hivyo basi, hatua ya kwanza ya kuwa na mahusiano yenye upendo na wengine ni kumpata Mungu wa kweli ambaye ni chanzo cha upendo na tujenge maisha yetu juu ya msingi wake. Maisha yetu yanahitaji kuwa na uhusiano wa kina na chanzo cha upendo. Kwa kufanya hivyo hatutaweza kamwe kupungukiwa na upendo na fadhili katika mahusiano yetu na kamwe hatutapata visingizio vya chuki.

**Mjumbe wa kweli na imani yake lazima ijengwe kwenye misingi ya upendo na wema.**

Yesu Kristo anasema katika Injili (Mathayo 22: 37-40) kwamba Torati yote na manabii hutegemea mambo mawili: Kwanza, mpende Bwana Mungu kwa moyo wako wote, nafsi yako yote na akili zako zote. Pili, mpende jirani yako kama nafsi yako mwenyewe. Anamaanisha kwamba, nabii wa kweli na Torati ya kweli lazima viwe na misingi ya upendo na wema. Ikiwa sivyo, basi nabii na dini yake, na Torati hiyo havijatoka kwa Mungu mwenye upendo. Kwa hiyo,

kama una nia thabiti ya kujenga urafiki wenye amani na kudumu na wengine, hautaweza kufanikiwa ikiwa unamfuata nabii yeyote au mifano mingine isipokuwa tu pale utakapomfuata Yesu Kristo mfano wa kuigwa kwa upendo na wema.

Ikiwa unamfuata nabii mwenye hasira na mkatili au kiongozi wa namna hiyo, mtazamo wake utaathiri mahusiano yako na familia yako na wengine. Lakini ikiwa unamfuata Yesu, upendo wake usiyo na masharti na fadhili zake vitakuwa misingi ya mahusiano yako na wengine. Kuna tofauti kubwa kati ya maneno ya Qura'ni na Injili kuhusu mahusiano. Qura'ni inakosa upendo na wema ambavyo ni muhimu katika kujenga urafiki wa kudumu. Kristo alikuja ulimwenguni ili kutufundisha upendo na kusafisha mioyo yetu kutokana na chuki, laana, ukatili, na vita, lakini miaka kumi ya mwishoni ya maisha ya Muhammad ilikuwa imejaa vitu hivyo vyote. Je! urafiki wa kudumu unawezekana pakiwepo na chuki, laana, uadui na vita? Hakika haiwezekani. Fikiria, kama Mungu angekuchukia na kukulaani kwa dhambi zako, na kuwa mkatili kwako kila wakati. Je! ungekuwa na tumaini lolote la kumrudia ili uwe rafiki Yake tena? Hapana. Watu huwa rafiki wa Mungu kwa sababu ya upendo na huruma yake na si kwa sababu ya ukatili Wake. Ibrahimu alikuwa rafiki wa Mungu kwa sababu Mungu alikuwa ana urafiki na mwema asiyeogofya. Hii pia ni

kweli katika mahusiano yetu. Watu huwa marafiki nasi ikiwa tu wema, mwenye kuonyesha upendo na kuwajali. Hakuna mtu anayeweza kuwa rafiki yetu wa kweli ikiwa tunamlaani au kumchukia. Ndiyo sababu Injili katika 1 Yohana sura ya 4 mstari wa 11 na 12 inasema: Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana. ...tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu.(MJKV)

Injili inakuambia umruhusu Mungu mwenye upendo kuishi ndani yako ili upendo wako uwe kamilifu na kisha unaweze kuwabadilisha hata adui zako kwa njia ya upendo huo mkamilifu. Kwa sababu kitu chochote kilicho kamili kinavutia, na ni vivyo hivyo kwa upendo kamili. Upendo mkamilifu unakuwezesha kuwa na familia yenye upendo, na wewe na familia yako mtaangaza upendo katika jamii yenu. Upendo wako pia unaweza kuwashangaza wapinzani wako, na labda wataweza kufuata nyayo zako na kuwa huru kutokana na uadui. Ni kwa sababu hii unahitaji kumfuata Yesu Kristo na kufanya Injili Yake taji la kichwa chako katika mahusiano yako na familia na wengine.

**Wakati wa kutafakari 15**

1. Ingekuwaje shida kama upendo na wema vingetokana na Ukisasa, Uislamu na mitazamo

mingine ya mabadiliko ya ulimwenguni badala ya kutokana na mafundisho ya Yesu?

2. Unafikiri mfano mzuri wa kuigwa wa upendo na wema unapaswa kuwa na sifa gani?
3. Je, utakuwa na mahusiano ya aina gani na watu kama ukimfuata kiongozi au nabii mwenye hasira na mkatili?
4. Kwa nini tunahitaji kumtambua Mungu wa kweli ikiwa tunataka kuwa na amani, upendo na wema na wengine?
5. Ni aina gani ya mabadiliko ambayo upendo na fadhili vinaweza kufanya katika familia, jamii na duniani?
6. Je, ni vizuri kumheshimu Yesu kwa upendo na wema wake kamili?

## Qur'ani inamtaka Mtume wa Uislamu Kuweka imani yake katika Biblia

Je, unaweza kuamini hili? Hiki ndicho nitakacho zungumzia na kukufanya ushangae.

Kuna propaganda nyingi kutoka kwa waislamu wenye itikadi kali kwamba Torati na Injili vilibadilishwa. Je, hii ni kweli? Katika sura ya awali niligusia jinsi gani aya za Qur'ani zilibadilishwa. Je! Torati na Injili pia vilibadilishwa?

Waislamu, ambao wanasema kwamba Torati na Injili vilibadilishwa hawajaweza kujenga hoja ya kuthibitisha kwamba mabadiliko hayo yalifanyika wakati gani, kabla au baada ya Muhammad. Je! Unajua kwa nini hawajapata hoja ya msingi ya madai yao? Kwa sababu bila kujali nini watasema, bado kitakuwa kinapingana na maneno ya Qura'ni.

### Torati na Injili visingeweza kubadilishwa kabla ya Muhammad

Kwa sababu Sura Yunus (10) aya 94 inamwambia Muhammad: Ikiwa unayo mashaka katika Qur'ani waulize Wakristo na Wayahudi ambao wamesoma Maandiko kabla yako. Sura Al-e Imran (3) mstari wa 3 na Sura Al Maeda (5) mistari ya 46 hadi 48 pia

inasema kwamba Injili na Torati ni mwanga na mwongozo kwa watu.

Tunaona kwamba kwa mujibu wa Qur'ani, Muhammad alikua na mashaka na ukweli wa Qur'ani yake lakini, mungu wake alimwagiza ajifunze ukweli kutoka kwa Wakristo na Wayahudi waliokuwa wakiifuata Torati na injili. Hii inaonyesha kwamba Torati na Injili havikubadilishwa kabla ya Muhammad, vinginevyo mungu wake asinge viita mwanga na mwongozo wa watu. Na pia Mungu asinge mwelekeza Muhammad kujifunza ukweli kutoka kwa Wayahudi na Wakristo ikiwa walifuata maandiko yaliyobadilishwa.

### Wala mabadiliko hayakutokea wakati wa Muhammad

Kwa sababu Sura Al Baghara (2) katika mstari wa 91 na 97 na Sura An Nisa (4) katika aya ya 47 inamwambia Muhammad: Qur'ani ni uthibitisho wa Maandiko yaliyo mikononi mwa Wakristo na Wayahudi. Kisha Sura Al Maeda (5) katika aya ya 68 inasema: Enyi watu wa Kitabu! Hamna lenu jambo mpaka muishike torati na Injili, na yote mlio telemshiwa kutoka kwa Mola wenu....

Qura'ni sio tu inathibitisha ukweli wa Torati na Injili bali pia inawasisitiza Wayahudi na Wakristo kuweka msingi wa imani yao katika torati na injili hiyo. Qur'ani

isinge vithibitisha ikiwa vilibadilishwa na Wayahudi au Wakristo.

## Mabadiliko ya Torati na Injili yasingeweza kutokea baada ya kifo cha Muhammad

Kwa sababu, kama Qur'ani inavyothibitisha, kwamba torati ya kweli na Injili vilikuwepo katika Peninsula yote ya Arabia na maeneo mengine mengi ya karibu yaliyokuwa chini ya jeshi la Kiislamu. Basi viongozi wa Kiislamu na walimu kutoka karne ya kwanza ya Uislamu wangetunza nakala ya Torati na Injili ya kweli ambayo ingeweza kutumika kama ushahidi wa mabadiliko yoyote. Lakini hakuna rekodi katika vitabu vya kale vya Kiislamu kuthibitisha madai haya. Hii inaonyesha kwamba madai ya kubadilishwa kwa torati na injili hayana msingi.

## Qur'ani inamwagiza Muhammad kutegemea Maandiko ya Kikristo na ya Kiyahudi

Nashangaa sana kwa nini viongozi wa Kiislamu hawatilii maanani mambo haya mawili ya muhimu katika Qura'ni. Kwanza, Sura Yunus (10) mstari wa 94 na 95 inamwagiza Muhammad kutegemea Torati na Injili. Pili sura Al Maeda (5) katika aya ya 43 inasema kwamba Wayahudi wanapaswa kuifuata Torati yao wenyewe na hawana haja ya kuifuata Qura'ni au uamuzi wa Muhammad.

Je, hamjashangazwa kwamba mungu wa Qur'ani anamwambia Muhammad kuamini Injili na Torati, lakini pia anawahimiza Wayahudi na Wakristo kwamba hawana haja ya kuifuata Qura’ni? Kwa maana nyingine, Muhammad na waislamu wana nafasi ya kuwa na mashaka au kuikataa Qura’ni lakini sio Torati kulingana na Qura’ni. Ikiwa Muhammad, kama kiongozi mkuu wa Uislamu, anaagizwa kutegemea Torati na Injili, basi inakuwa dhahiri kwamba Waislamu, viongozi wa Kiislamu, walimu na waandishi wa kiislamu pia wanahitaji kutegemea Maandiko ya Kikristo na Kiyahudi, badala ya kueneza mashtaka ya uongo kuhusu maandiko hayo.

Aya hizi za Qur'ani zinatoa mwanga jinsi gani Muhammad anathamini maandiko matakatifu yaliyoko mikononi mwa Wakristo na Wayahudi. Hakuthibitisha tu mamlaka ya vitabu hivi vitakatifu, bali pia aliwahimiza Waislamu kukiri imani yao kwa kuvifuata. Kwa hiyo, Qur'ani yenyewe inafuta mashaka yote yaliyo juu ya Torati na Injili.

Ikiwa Wakristo na Wayahudi walibadilisha maandiko yao na kupoteza maana halisi, basi Muhammad asingechagua kutegemea maandiko na desturi zao. Lakini tunagundua kutokana na vitabu vya Kiislamu kwamba Muhammad alihudhuria kanisani huko Makka kwa miaka mingi na alikuwa akiwasiliana na

makuhani. Mke wake Khadijah daima alienda kanisani huko Makka. Hii ilikuwa kwa sababu Muhammad aliwaamini Wakristo. Ikiwa haya ni maisha ya kweli ya Muhammad na kama aliheshimu Biblia yake sana, hadithi hii ya mabadiliko ilitoka wapi?

## Je! Wazo la shutuma lilitoka wapi?

Dhana hii ya shutuma ilianza baada ya Muhammad kutoka Makka na kwenda Medina na kukimbilia katika kabila la Medina lililojulikana kama Khazraj,watu hawa waliwachukia Wayahudi na Wakristo. Kusudi aweze kuishi vyema na kukubalika, Muhammad alibadilisha mwenendo wake ili uendane na kabila hilo. Chuki inajenga matatizo makubwa katika mahusiano ya watu. Kama ukianza kumchukia mtu au kikundi cha watu, chuki hiyo inakufanya utengeneze shutuma nyingi za uongo dhidi yao, hata kuwaita wanyama waovu na kuwatakia kifo.

Hiki ndicho kilichotokea kwa Muhammad huko Medina. Wakati alipokuwa Makka aliwaona Wayahudi na Wakristo kama mifano mizuri ya kuigwa, na kuita maandiko yao mwanga kwa watu. Lakini baada ya kukimbilia Medina, aliwaita kuwa wanyama wabaya zaidi, alipuuza umuhimu wa maandiko yao na pia akawaamuru kuacha dini zao na kujiunga na Uislamu. Mambo aliyowafanyia Wayahudi na Wakristo baadaye yalikuwa kinyume kabisa na maelekezo ya Qur'ani iliyo

yatoa wakati wa kipindi cha mwanzo mwa huduma ya Muhammad huko Makka. Sababu yake ilikuwa kwamba mungu wake alikuwa amebadili mawazo yake juu ya Wayahudi, Wakristo na Maandiko yao ili kumpendeza Muhammad.

**Je! Mungu wa kweli husema kinyume na maneno na maagizo Yake ili kupindisha ukweli?**

Hapana kabisa. Hii ni sababu moja wapo iliyonisababisha kupoteza imani katika Qura'ni.

Uwezo na utawala wa Muhammad uliongezeka huko Medina mwaka baada ya mwaka, na hivyo hivyo Qur'ani ilikuwa ikisogea mbali na mafundisho yake ya awali. Mafundisho yalikuwa yana wachanganya zaidi watu, hata wengine walikasirika na kuondoka katika Uislamu kwa sababu ya udhalimu na ukatili kwa watu ambao haukuwepo mwanzoni. Muhammad wa Medina hakuwa kama Muhammad wa Makka tena. Makka, alikuwa mtu mwenye amani na hakuwalazimisha wapagani kumfuata. Wayahudi na Wakristo walikuwa kwenye njia sahihi ya kuifuata Biblia. Alikuwa hata akihudhuria kanisani na mke wake Khadijah. Lakini huko Medina alianza kuwachukia na kuthamini chuki dhidi ya Wayahudi na Wakristo, akitumia kisingizio kwamba mungu wake alibadili mawazo yake ili kumpendeza.

**Je! Wazo la shutuma lilieneaje?**

Huko Medina, Muhammad alikuwa chini ya shinikizo la kutafuta sababu na visingizio vyovyote vya kuwalaumu Wayahudi na Wakristo ili kuwafurahisha watu wa kabila lililomkaribisha. Aliwafundisha wafuasi wake kwamba jina lake lilitabiriwa katika Torati na Injili (Suras 7: 157 na 61: 6), ili wafuasi wake waweze kuwalaumu Wayahudi na Wakristo kwa kubadilisha Biblia kama wasipoweza kupata jina lake humo. Miaka baada ya kifo cha Muhammad, walimu wa Kiislamu waligundua kwamba jina la Muhammad halikuwepo katika Biblia. Kwa kuwa ilikuwa kinyume cha sheria kutilia shaka lolote juu ya maneno ya Muhammad na Qura'ni, chaguo rahisi na salama kwao ilikuwa kuwalaumu Wakristo na Wayahudi kwa kubadilisha Biblia na kuondoa jina la Muhammad. Kwa hiyo, habari za "kuondolewa kwa jina la Muhammad kutoka kwenye Biblia" zikaenea sana miongoni mwa Waislamu.

Kwa hiyo tunaweza kuona jinsi gani Muhammad alivyobadilisha mtazamo wake juu ya Wayahudi na Wakristo baada ya kuhamia Medina. Hii ilipelekea wafuasi wake kuikataa Biblia kwa shutuma zisizo na msingi na kuwafanya waislamu ulimwenguni kote kuwalaumu Wayahudi na Wakristo.

**Kiambazi cha shutuma**

Kwa sasa hofu ya kuzungumzia ukweli imezuia uwezekano wa walimu na viongozi wa kiislamu kukabiliana na tofauti zilizopo baina ya Qur'ani na Biblia katika namna ya kimantiki na ya kitheolojia.

Cha kushangaza, kwa viongozi na walimu wa kiislamu, uhalali wa Biblia haujapimwa kulingana na msingi wa ujumbe wake bali kwa kuangalia kama kuna jina la Muhammad au la. Tofauti halisi kati ya vitabu hivi viwili si uwepo au kutokuwepo kwa jina la Muhammad; ila ni wokovu ambao Biblia inawapa wafuasi wake katika maisha yao ya hapa duniani kitu ambacho Qur'ani haifanyi.

Basi tuseme jina la Muhammad lilikuwa katika Biblia. Je, hii ingeleta tofauti gani? Hakuna. Ujumbe mkuu wa Biblia ni kwamba unahitaji kuweka imani yako katika Yesu Kristo, ambaye yuko hai mbinguni na anaweza kukuongoza kwenda mbinguni. Hata kama jina la Muhammad lingekuwa limeandikwa katika Biblia, bado lingekuagiza uweke imani yako kwa Yesu. Kwa nini? Kwa sababu, Yesu ndiye njia pekee, ukweli na uzima wakukuongoza kwenda mbinguni.

Ujumbe wa Biblia kuanzia kwa Adamu hadi kwa Yesu umefupishwa kwa ukweli kwamba wokovu kwa watu ni jambo la muhimu sana kwa Mungu. Kwa sababu hiyo,

Mungu alijifunua mwenyewe katika Yesu Kristo ili kuwaokoa watu kutoka kwenye vifungo vya dhambi na Shetani. Hicho ndicho Mungu anacho zingatia katika Biblia si kukosekana au uwepo wa jina la nabii, lakini wokovu wa watu, ambao ni muhimu zaidi kuliko jina la mtu yeyote.

Biblia nzima ya Yesu Kristo kama Kitabu iliandikwa na manabii 40 kwa kipindi cha zaidi ya miaka 1600. Ikiwa na zaidi ya unabii 300, wote ukitazamia siku ambayo Yesu Kristo angekuja na kuokoa ulimwengu. Vurugu za kisiasa wala mabadiliko ya kiuchumi na kijamii hayakuweza kuathiri mtirirko wa jumbe za hawa manabii 40 wa Biblia kwa kipindi hicho kirefu. Unabii wote huu ulitimia kwa ujio wa Yesu Kristo. Lakini mivurugano ni mingi katika Qur'ani, hata kama iliandikwa na mtu mmoja tu, Muhammad, katika muda mfupi wa miaka 23 wa huduma yake. Licha ya muda mfupi huu, mistari mingi ya Qur'ani kutoka miaka 10 iliyopita ya maisha ya Muhammad ni kinyume na mistari ya awali ya Makka. Je! Hushangazwi na mtiririko wa ujumbe wa manabii wengi katika Biblia kwa kipindi cha mwaka 1600?

## Unawezaje kuondoa kiambazi cha mashtaka usoni mwako?

Shauku yangu ilinipelekea kusoma na kupima maneno ya Biblia ya Yesu Kristo mimi mwenyewe ambayo

viongozi wa Kiislamu wanayakataa. Nilijisemesha, Mungu amenipa macho ya kuona na kusoma, ubongo wakulinganisha, moyo na dhamiri vya kutathmini na kuamua. Hii ilinifungulia mlango nikaweza kugundua kwamba Biblia ya Kristo inaweka mikono ya mwanadamu mikononi mwa Mungu. Qur'ani kamwe haifanyi hivyo. Ni kwa sababu hii, nilimpa Yesu moyo wangu.

Nawe pia unahitaji kufanya vivyo hivyo, na uchukue juhudi binafsi, ili utambue kama Qur'ani au Biblia ya Yesu Kristo ipi ni ya ukweli, na uchague kimoja ambacho kinakupa uhakika wa wokovu. Si Qur'ani wala Muhammad anauwezo wa kukupa uhakika wa wokovu. Sura Lughman (31) mstari wa 34 na Sura Al Ahghaf (46) mstari wa 9 inasema kuwa hakuna mtu anayejua nini kitatokea kwake baada ya kifo. Lakini Biblia inasema wale wanaomfuata Kristo tayari wameokolewa na wataenda mikononi mwa Mungu baada ya kufa. Kwa hiyo, itumainie Biblia ya Yesu Kristo na uokoke.

**Wakati wa Kutafakari 16**

1. Je! Muhammad angeweka imani yake katika Biblia ikiwa alifikiri kuwa ilibadilishwa?
2. Je, kuna sababu yoyote ya msingi inayoonyeshwa kuthibitisha madai ya wasomi wa Kiislamu juu kile wanachoita mabadiliko yaliyofanyika katika Biblia?
3. Sababu moja wapo ya shutuma za wasomi wa Kiislamu ni ukosefu wa jina la Muhammad katika Biblia. Je, italeta utofauti wowote katika ujumbe mkuu wa Biblia ikiwa jina lake lingewekwa katika Biblia?
4. Tunapaswa kufanya nini ili kuwafanya Waislamu wajali zaidi wokovu wao wenyewe (kwa kuwa ni jambo la msingi zaidi kwa Mungu) kuliko kujali uwepo au kutokuwepo kwa jina la nabii katika Biblia?
5. Ni kitabu gani tunapaswa kufuata - Biblia ambayo inatoa uhakikisho wa wokovu au Qur'ani isiyo na wokovu kabisa?

# Tuhuma za waislamu dhidi ya Imani ya kikristo hazina msingi

Waislamu hulaumu Wakristo kwa mambo ambayo hawajawahi kuyaamini. Mfano mmoja ni tafsiri potofu ya maneno "Mwana wa Mungu". Wafuasi wa Yesu wanaamini kwa namna ya kiroho kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na wao pia wanaamini ni watoto[99] wa Mungu.

## Kumwita Yesu "Mwana wa Mungu" ni kufuru katika Uislamu

Qura'ni katika Sura An-Nisa (4) mstari wa 171 inasema kwamba Mungu hawezi kamwe kuwa na mwana. Na katika sura ya Mariamu mistari ya 35, 89 na 91 inasema kuwa ni kitu kibaya, na janga kubwa sana kutaja kwamba Mungu ana mwana. Ukilinganisha kauli hizi za Qur'ani ambazo ni kinyume na maana halisi ya maneno "Mwana wa Mungu" kama ilivyo katika Injili ya Yesu Kristo, unagundua kwamba maoni

---

[9]Injili inasema, "Heri wapatanishi kwa maana wataitwa wana wa Mungu." (Mathayo 5: 9) Yesu anaitwa Mwana wa Mungu kwa sababu si tu mpatanishi bali pia ni mfalme wa amani. Wafuasi wake pia wanaitwa wana wa Mungu kwa sababu wamejengwa katika imani na Yesu ili wawe mabalozi wake wa amani.

ya waandishi wa kiislamu hayakuwa sahihi kwa kusema eti ni "kufuru za Wakristo dhidi ya Mungu". Wanasema kwamba Wakristo wanaamini kwamba Yesu alikuja ulimwenguni kama matokeo ya uhusiano wa kimwili kati ya Mungu na Maria.

Hakuna sehemu yoyote katika Biblia ya Kikristo inayosema kuwa Yesu alizaliwa kutokana na uhusiano wa kimwili kati ya Mungu na Maria. Badala yake, inasema; kwa ujio wa Roho wa Mungu juu ya Bikira Maria, Roho alifanyika mwili na kujidhihirisha kikamilifu katika Yesu Kristo. Uhusiano wa Mungu na Maria katika Injili ni uhusiano wa kiroho. Mungu haitaji mke na hawezi kuwa na uhusiano wa kidunia na mwanamke kwa sababu yeye ni Mungu.

## Kupuuza ukweli wa maneno "Mwana wa Mungu"

Je, hili si jambo la kushangaza? wasomi wakiislamu na Muhammad walifungia macho ukweli halisi wa maneno haya katika Injili, lakini waliwadhihaki Wakristo na kuwaruhusu waislamu kuwaua kwa sababu ya kushindwa kuelewa tafsiri yao potofu ya maneno ya injili. Ndiyo sababu kila mwislamu anahitaji kuazima Injili kutoka kwa Mkristo, kuisoma binafsi na kuelewa kwamba shutuma za Kiislamu kwa imani ya kikristo sio za kweli. Waislamu wanahitaji kujua nini maana ya kuitwa mwana wa Mungu ili

waweze kukomesha chuki, kutokuelewana, na ukatili dhidi ya imani ya kikristo na Kiyahudi iliyo endelea kwa miaka 1400.

Injili inasema kuhusu kutungwa kwa mimba ya Yesu kwa Maria katika kitabu cha Luka sura ya 1 mstari wa 35: “Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu.”(MKJV) Unaona kwamba Injili inasema wazi kwamba Roho wa Mungu alimshukia Maria na akapata mimba ya mtoto Mtakatifu Yesu. Huo ulikuwa uhusiano wa kiroho si uhusiano wa kimwili.

Kuhusu wafuasi wa Yesu Kristo, injili katika kitabu cha Yohana sura ya 1 mstari wa 12 na 13 inasema kwamba Yesu aliwapa uwezo wote waliomwamini kuitwa wana wa Mungu. Waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu KIROHO kwa sababu ya imani yao katika Yesu Kristo. Injili tena katika kitabu cha 1 Petro sura ya 1 mstari wa 23 inawaambia wafuasi wa Yesu Kristo: “Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. “(MKJV)

Kwa hiyo, Yesu anaitwa Mwana wa Mungu kwa sababu yu hai, ni Roho wa milele na ni Neno la Mungu;

tunaitwa wana wa Mungu kwa sababu Yesu anaishi ndani yetu kama Roho wa milele na Neno la Mungu, na ametupa uzima wa milele na uhakika. Kwa hiyo, tafsiri za vitabu vya Kiislamu na maoni juu ya imani ya Wakristo kuhusu Mwana wa Mungu si ya kweli kabisa. Wasomi wa Kiislamu wanapaswa kusoma Injili na kuacha kuwalaumu Wakristo bila msingi.

## Qur'ani inasema kuwa Mwenyezi Mungu anaweza kuwa na mwana

Sasa nataka kukuonyesha mambo machache ya kuvutia kutoka kwenye Qura'ni. Sura Maryam (19) katika mstari wa 89 na 91 inasema kwamba kumhusisha Mungu na mwana ni jambo baya sana. Lakini Sura Az-Zumar (39) katika mstari wa 4 inasema kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana akitaka. Kama kumhusisha Mungu mwana ni jambo baya kwa nini sasa Qur'ani yenyewe ina fungua mlango wa watu kusema Mungu anaweza kuwa na mwana?

Je wasomi wa Kiislamu hawawezi kuona tatizo hili katika Qur'ani? Wao huwaita Wakristo wanakufuru kwa kuamini kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana. Je, sio kufuru kwa Sura Az Zumar kusema kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana akitaka? Kwa upande mmoja Qur'ani katika Sura An-Nisa (4) aya 171 inasema kwamba Mungu hawezi kuwa na mwana, lakini kwa upande mwingine Sura Az-Zumar

(39) katika mstari wa 4 inasema kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana akitaka. Umeipata hiyo? Sura Az-Zumar inasema kwamba haiwezekani kwa Mungu kuwa na mwana.

Je, si unafiki huu? Kwa upande mmoja, Qur'ani inawaambia Wakristo kwamba Mungu hawezi kuwa na mwana, lakini kwa upande mwingine inawaambia Waislamu, kwamba ndiyo, kama Mungu akipenda anaweza kuwa na mwana. Hii si haki kwa Qur'ani yenyewe kuthibitisha kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana, lakini hapo hapo inalenga kuwanyima Wayahudi na Wakristo imani hii. zaidi sana, inawaelekeza waislamu kuwaua wakristo na wayahudi kwa kuwa na imani kama hiyo. Hii sio haki kabisa.

Sura Al Tawba (9) katika mistari 29 na 30 inasema: Fanyeni vita dhidi ya wale waliyo pewa Maandiko....... Wayahudi wanasema, 'Ezra au Ozair ni mwana wa Mungu'; na Wakristo wanasema, 'Masihi ni mwana wa Mungu.' ....

**Kuna uwezekano wa kuondokana na tuhuma zisizo na mashiko.**

Natumaini umeona kwa nini Qur'ani haina sababu na haina haki halali ya kuwashutumu Wayahudi na Wakristo na kupigana nao kwa kuamini kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana. Kwanza, kwa sababu

Wakristo wanaamini hilo kwa namna ya kiroho, pili, Quran yenyewe inasema katika Sura Az-Zumar kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana. Kwa hiyo wasomi wa Kiislamu wanapaswa kujionea aibu kwa kuwalaumu Wakristo na Wayahudi kwa kueneza shutuma za uongo dhidi yao kila mahali. Wanahitaji kuwaomba msamaha Wayahudi na Wakristo. Tafsiri zote za vitabu vya Kiislamu na maoni juu ya imani ya Wakristo kuhusu Mwana wa Mungu si sahihi kabisa. Waandishi wa Kiislamu hawataweza kupata mtazamo wa kweli wa Ukristo isipokuwa wakiisoma Injili. Wanapawsa kuacha vikwazo vya kimila vya Uislamu nyuma na kusoma Injili na tafsiri za maneno ya Injili ili waweze kuelewa mahusiano ya Wakristo kwa Umwana wa Yesu Kristo.

Nami nilikuwa hivi nilipokuwa bado Mwislamu. Daima kulikuwa na shinikizo la kitamaduni kwa watu kama mimi kufuata mila, bila kujali kama zilikuwa sahihi au mbaya. Lakini ninafurahi sana kwamba katika hatua mojawapo ya maisha yangu mawazo yangu na moyo wangu vilitamani kuona maisha nje ya Uislam. Na ni wakati huo Yesu alijifunua kwangu nakubadilisha mtazamo wangu wa dunia.

**Tofauti na imani ya Kikristo, Uislamu hutafsiri Utatu kama miungu mitatu**

Nataka kukushirikisha mojawapo ya mashtaka ya Uislamu yasiyo na msingi dhidi ya Wakristo kuhusu Utatu.

Qur'ani (Nisaa 4: 171; Al Maeda 5: 116) na tafsiri za Kiislamu husema kwamba Wakristo wanaamini katika miungu mitatu. Hii sio kweli kabisa. Ni kufuru katika Biblia ya Yesu Kristo kwa kumwamini Mungu zaidi ya mmoja. Injili inasema mara nyingi kwamba "Mungu ni Mmoja" (Marko 12:32, Warumi 3:30, 1 Wakorintho 8: 4, Wagalatia 3:20, 1 Timotheo 2: 5).

Hakuna uthibitisho wa miungu mitatu katika Injili kabisa. Uislamu umepotosha ukweli ili upate kisingizio cha kuwahukumu Wakristo. Wakristo kamwe hawatafsiri Utatu katika Injili kumaanisha miungu mitatu. Tafsiri na fafanuzi zote huonyesha ni imani katika Mungu mmoja wa kweli

Nini maana ya utatu katika imani ya kikristo? Ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Kama Mungu mwenye upendo na msamaha, Wakristo wanamwita Baba wa Kiroho. Kama mwanzilishi wa Ufalme Wake wa Kiroho ndani ya mioyo yetu hapa duniani, anaitwa Mwana. Na kama Mungu mlinzi, mwenye kutupa uhakika na mwongoza hapa duniani, anaitwa Roho Mtakatifu. Kwa

maana hiyo Utatu ni Mungu huyo huyo anayejifunua kwetu kwa njia tatu tofauti.

Sisi kama binadamu pia tuna aina tofauti ya vyeo katika maisha yetu hapa duniani. Mimi naitwa mwana, mume na baba. Ingawa mimi ni mtu mmoja, ninajionyesha kwa njia tatu au kama watu watatu ili kuonyesha upendo na wajibu wangu katika familia yangu. Hii haina maana kwamba mimi ni watu watatu wanao tofautiana. Mimi ni mtu mmoja lakini ninajionyesha kama watu watatu. Hii ni vivyo hivyo kwa Mungu.

Mungu mwenyewe ahitaji majina haya; yote ni kwa manufaa ya binadamu. Binadamu anahitaji upendo safi ambao upo kwa Mungu pekee. Kwa kuwa katika maisha yetu ya kila siku, hakuna upendo unaozidi upendo wa wazazi kwa watoto wao, Mungu anajiita Baba, akionyesha kwamba anatupenda kwa moyo kama mzazi lakini zaidi kuliko wazazi wetu.

## Angalia jinsi gani Mungu anavyoelezea upendo na matendo yake katika Biblia

Katika kitabu cha nabii Isaya, sura ya 66 mstari wa 13 Anasema: "Mfano wa mtu ambaye mama yake amfariji, ndivyo nitakavyowafariji ninyi;.....(NKJV) Tena katika kitabu cha Isaya sura ya 49 mstari wa 15 Mungu anasema: "Je! mama aweza kumsahau mwanawe

anayenyonya, hata asimwonee huruma mtoto wa tumbo lake? Naam, wanaweza kusahau, lakini sitakusahau." Yesu anasema katika kitabu cha Mathayo sura ya 7 mstari wa 11 katika Injili:" Ikiwa nyinyi, mliyo waovu mwajua kuwapa, watoto wenu vipawa vizuri, hakika Baba yenu wa Mbinguni atafanya zaidi: atawapa mema wale wamwombao? "(MKJV)

Hivyo upendo wa Mungu ni upendo wa mzazi kwetu. Anatugusa kwa upendo wa karibu kama baba ili kutufundisha nini maana halisi ya upendo wa kweli, haki, utakatifu, utauwa, amani na furaha. Ni kwa sababu hizi, anaitwa Baba.

**Mungu pia anaitwa Mwana**

Roho wa Mungu alimshukia Maria na Roho akazaliwa kwa mwili kama Yesu. Hii inamaanisha Mungu alijifunua mwenyewe katika Yesu. Mungu anauwezo wa kujifunua kwa njia yoyote anayotaka. Alijionyesha kama moto kwa Musa na kama mtu ndani ya Yesu kwa ajili yetu.

Kwa nini Mungu anataka kujidhihirisha mwenyewe? Kwa nini hajifichi kama mungu wa Uislamu? Kwa sababu ana mpango wa kimbingu wa kutekeleza duniani. Mpango wake unaweza kufanikishwa duniani na Mungu tu kwa vile hakuna mtu mwingine anayejua mpango huo isipokuwa Mungu.

Pia, Mungu amewaumba binadamu na kusudi. Ili kutoa kusudi la maisha, uwepo wa daima wa Mungu na usimamizi wake ni muhimu. Yeye ndiye mbunifu wa kuimarisha Ufalme wake katika mioyo yetu. Mbunifu anafanya mambo mawili: Kwanza, anaandika kila kitu kwenye karatasi, pili, anaenda sehemu husika kwa ajili ya kujenga. Mungu pia anafanya hivyo. Aliandaa Biblia kama Neno lake lililoandikwa la kuonyesha ni jinsi gani ya kuuanzisha ufalme wake wa kiroho ndani ya mioyo yetu. Kisha akajifunua mwenyewe katika Yesu na akaingia katika maisha yetu ili kuimarisha ufalme Wake katika mioyo yetu pia.

Je, maneno ya Mungu yanaweza kuwa na maana gani kwetu ikiwa hatuna mtu wa Mungu pamoja nasi? Ndiyo sababu Injili inasema katika kitabu cha Yohana sura ya 1 mstari wa 14: "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli." Kwa hiyo Mungu alijifunua mwenyewe katika Yesu na akamwita mtu huyo katika ufunuo huu "Mwana" ili kujenga ufalme wake wa kiroho hapa duniani.

### Mungu pia anaitwa Roho

Katika injili Mungu aliyepo kila mahali, mwenye kufundisha, na kufariji, mwenye kutoa ulinzi, uhakika na mwongozo, anaitwa Roho Mtakatifu. Kwa Mungu

kuwa Mungu pekee wa upendo na Mwokozi haitoshi kwa wanadamu. Pia tunahitaji uwepo wake wa kudumu kutukumbusha na kutulinda, kama mama au baba kutushikilia mikono hadi mwisho wa safari yetu hapa ulimwenguni. Uwepo huu wa daima wa Mungu pamoja nasi duniani huitwa Roho Mtakatifu katika Injili. Hivyo Utatu humaanish miungu mitatu, lakini udhihirisho wa Mungu Mmoja kwa njia tatu. Kwa hiyo, mashtaka ya wasomi wa Kiislamu kwa wakristo hayana msingi

Nitamaliza majadiliano yangu na mashtaka mengine ya kushangaza na ya ajabu kutoka kwenye Qura'ni. Katika Sura Al Tawba (9) mstari wa 31 inasema: "Wayahudi na Wakristo huwachukulia walimu wao na watawa wao kama mabwana mbadala wa Mungu, ...."

Hakuna mafundisho kama hayo katika Biblia nzima wala katika historia ya Wayahudi wala Wakristo. Ni mashtaka yasiyo na msingi kabisa. Injili na Wakristo wanaamini katika Mungu mmoja tu. Mashtaka ya Kiislamu kuhusu imani ya Wakristo hayana mashiko.

**Wakati wa kutafakari 17**

1. Injili (Luka sura ya 1 mstari wa 35) na Qura'ni (Sura Maryam mistari ya 17 hadi 21) vyote vinasema kwamba Mungu alimtuma Roho Wake kwa Bikira Maria na akamzaa Mwana Mtakatifu. Basi kwa nini wasomi wa Kiislamu hupuuza

uhusiano huu wa dhahiri wa kiroho kati ya Mungu na Maria, na kudanganya kwamba Yesu alikuwa ni matokeo ya uhusiano wa kimwili kati ya Mungu na Maria?

2. Kuna ukweli gani katika maandiko ya wasomi wa kiislamu waliyokataa kumwita Yesu "Mwana wa Mungu" wakati hata Qur'ani yenyewe inathibitisha kwamba Mungu anaweza kuwa na mwana kama akipenda?
3. Ni kufuru kumwamini Mungu zaidi ya mmoja katika Biblia. Wakristo hawajawahi kutafsiri Utatu kama miungu mitatu, kwa nini basi wasomi wa kiislamu na Muhammad wanasema kwamba Wakristo wanaamini katika miungu mitatu?
4. Ni nini kinachoweza kusaidia Waislamu kuwa huru na habari zisizo sahihi na mashtaka ya uongo?
5. Kama Mwislamu, Danieli pia aliwashutumu Wakristo kuhusu Utatu na Umwana wa Yesu Kristo. Maoni yake yalibadilikaje?

## Mchezo wa Kisiasa katika Uislamu unapingana na imani yake yenyewe

Kwa msingi wa kidini, Uislamu ni dini pekee ya kisiasa duniani. Huwezi kuitenga siasa na uongo na udanganyifu. Sio tu siasa za Kiislamu zimeshindwa kuepuka uongo na udanganyifu, bali zimekwenda mbali zaidi na kuhalalisha tabia hizi kwenye nyakati fulani.

### Siasa za kudanganya

Suras Al-e Imran (3) aya ya 54 na Al Anfal (8) mstari wa 30 zinasema: Mwenyezi Mungu ni mdanganyifu kuliko wote. Kama Mwenyezi Mungu ni mdanganyifu kuliko wote, hii ina maana atatumia udanganyifu wake katika kila kitu, hata katika siasa pia. Kama Mwenyezi Mungu anatumia udanganyifu katika siasa, hamfikirii kwamba watumishi wake waaminifu pia watafuata nyayo zake? Hakuna shaka nao pia watafuata siasa zake.

Uhalalishwaji wa udanganyifu katika Uislamu imewagharimu sana waislamu tangu kuanzishwa kwa Uislamu mpaka sasa. Udanganyifu ulifungua mlango wa michezo ya uongo na ya kisiasa, na hata ndani ya jamii ya Kiislamu.

Qur'ani pia inasema kwamba Mwenyezi Mungu alihalalisha uongo. Sura An Nahl (16) aya ya 106 inafundisha kwamba kuna hali ambazo zinaweza "kumlazimisha" Mwislamu kusema uongo. Sura Al Baghara (2) aya ya 225 inawaruhusu Waislamu kukana imani yao kwa Mwenyezi Mungu ikiwabidi mpaka hali itakaporudi kuwa kawaida. Sura Al-Imran (3) aya ya 28 inawaambia Waislamu kuwa marafiki na wasiokuwa Waislamu mpaka watakapo pata nguvu ya kuwatawala au kufanya kitu dhidi yao.

Unaona kwamba mungu wa Uislamu huwaruhusu wafuasi wake kusema uongo na kuishi bila uaminifu kati yoa na wengine.

Matokeo yake, uongo uliathiri mahusiano ya Kiislamu na mfumo wao wa sheria. Mwandishi maarufu wa Hadithi Bukhari anaandika katika Hadith yake namba 857 ya Kitabu cha 49 katika toleo la 3 kwamba Muhammad nabii wa Uislamu alisema: Mtu anayeleta amani kwa watu kwa kutengeneza maneno mazuri au kwa kusema mambo mazuri, ingawa si ya kweli, hasemi uongo.

Unadhani nini kitatokea pale mungu na nabii wa taifa wanapotoa kibali cha kusema uongo! Kwa sababu hii kusema uongo pale inapokubidi au Taghiyya haijaruhusu uaminifu kujengeka kati ya mataifa ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa Biblia, ni ukweli pekee, na sio uongo, unaweza kujenga mahusiano ya dhati na ya amani. Uongo na udanganyifu vilihalalishwa na Mwenyezi Mungu, Muhammad, na wasomi wa kiislamu na vikawa sehemu ya imani na siasa za Kiislamu. Kisha nini kilitokea? Udanganyifu na uongo ulifanya michezo ya kisiasa isiepukike katika siasa za Kiislamu na kusababisha imani za Kiislamu kukosa msimamo.

**Kwa sababu ya michezo ya kisiasa, Muhammad mwenyewe alibadili kanuni za Uislamu.**

Kuona kwamba nabii wa Uislamu alibadilisha kanuni za Uislamu mara kwa mara bila kusita, wafuasi wake pia wakamwiga hadi kufikia hatua ya kupuuza amri na mila za Muhammad baada ya kifo chake. Waislamu walilazimishwa kufuata mabadiliko haya ya kiimani.

Biblia inakataa aina yoyote ya udanganyifu na uongo. Katika kitabu cha Mithali za Sulemani sura ya 14 aya ya 5 na 25 Biblia inasema: "Shahidi mwaminifu hatasema uongo; Bali shahidi wa uongo, pumzi zake ni uongo.... Shahidi wa kweli huponya nafsi za watu; Bali atoaye uongo hudanganya." (NIV) Injili pia inasema katika 2 Wakorintho sura ya 4 aya ya 2:".lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za

Mungu." (NIV) Biblia inakataa wazi udanganyifu na uongo. Wakati, Qur'ani inavifanya kuwa sehemu muhimu ya imani ya Kiislamu, na kusababisha michezo ya kisiasa na machafuko.

**Mfano wa kwanza wa michezo ya kisiasa katika Uislamu ni kubadili mwelekeo wakati waislamu wanaswali.**

Kwa miaka kumi na tano mwelekeo wa swala wa Muhammad, au Ghiblah ulikuwa Yerusalemu yeye na wafuasi wake waliswali mara tano kwa siku kuelekea mji huo. Hii ilikuwa wakati alipokuwa bado ana matumaini ya kuwaleta Wayahudi kwenye Uislamu na kumkubali yeye kama nabii wao. Lakini walimkataa kwa sababu manabii walitakiwa kutoka kwenye uzao wa Isaka. Kwa sababu hii, Muhammad aliwachukia Wayahudi na hakutaka tena kuswali akielekea mji wa Kiyahudi wa Yerusalemu. Alibadili mwelekeo wake wa swala kutoka kwa Mungu Mmoja aliye patakatifu huko Yerusalemu na kugeukia Kaba ambapo mamia ya sanamu yalikuwa bado yanaabudiwa na wapagani. Sura Al Baghara (2) katika mistari 142 na 145 inatuambia kwamba Mwenyezi Mungu alithibitisha mabadiliko ya Ghiblah kumfurahisha Muhammad. Matokeo yake, sehemu muhumu ya imani ya Uislamu ilikufa kwa sababu ya michezo ya kisiasa.

Mabadiliko ya Ghiblah katika Uislamu hayana maana nyingine zaidi ya kuonyesha dalili ya ukosefu wa msimamo wa mafundisho ya Kiislamu. Mungu wa kweli hawezi kumwagiza nabii wake kugeuza uso wake na kuachana na patakatifu pa Mungu na badala yake kuelekea katika hekalu la sanamu.

Tatizo la pili ni kile Sura Al Baghara (2) inachosema kwamba Mwenyezi Mungu alithibitisha mabadiliko ya Ghiblah ili kumfurahisha Muhammad. Ingawa katika imani ya kweli, ni nabii na watu ambao wanapaswa kumpendeza Mungu asiye na dhambi, sio Mungu kufurahia nia za mtu mwenye dhambi. Ujumbe huu katika Qura'ni hauna mashiko.

Muhammad alichokifanya ilikuwa mchezo wa kisiasa. Kwa kuwa alipoteza tumaini la kuwafanya Wayahudi kuwa Waislamu, aliamua kuwekeza katika wapagani na kuwavuta katika Uislamu. Ni kwa sababu hii, aliacha Yerusalemu na kuchagua Ka'ba kama Ghiblah kwa ajili yake mwenyewe na Waislamu wote.

## Mfano wa pili wa michezo ya kisiasa katika Uislamu ni kupenya kwa amani, na kisha kutawala kwa nguvu

Katika miaka 13 ya kwanza ya kuhubiri kwake, Muhammad alisema: "Na kusiwepo na kulazimishwa katika dini", ambayo sasa ni aya ya 256 ya Sura Al

Baghara (2) ya Qura’ni. Wakati huo, alikuwa na wafuasi 150 tu. Katika miaka 10 ya mwishoni ya maisha yake wakati alipokuwa ana wafuasi wengi zaidi, Muhammad alijiweka katika nafasi kubwa ya madaraka kama kiongozi wa kisiasa na kiongozi wa kidini bila shaka, na hivyo alilazimisha makundi yote ya watu katika Peninsula ya Arabia kuwa wafuasi wake. Kisha lugha ya Qura’ni ikabadilika kutoka "dini haipaswi kulazimishwa" na kuwa "hakuna dini nyingine yoyote itakayokubalika isipokuwa Uislamu" ambacho kimeelezwa katika Sura Al-e Imran (3) aya ya 85.

Mchezo huu wa kisiasa katika Uislamu ulikuwa mfano wa kuigwa na viongozi wengi wa Kiislamu baada ya Muhammad, ambao umekuwa kama sumu ya kuua uaminifu na urafiki. Tunavyoendelea mbele, utaona madhara yake katika kila kipengele cha maisha.

**Mfano wa tatu wa michezo ya kisiasa katika Uislamu ni matumizi ya mabavu kupata madaraka.**

Mabadiliko ya mara kwa mara yaliyoletwa na Muhammad kama mbinu ya kuwafikia wengine yalionekana kama ishara kwa wafuasi wake kwamba kiongozi wa Kiislamu ana mamlaka ya kufanya kila kitu anachotaka. Viongozi wa Kiislamu waliochukua madaraka baada ya Muhammad, Abu Bakar, Omar,

Othman na Ali walirithi migogoro ya kisiasa kutoka kwa Muhammad na walijua kwamba wanaweza kubadilisha kila kitu katika Uislamu kuwa wanavyo taka wao.

Mkwewe Ali alidai kuwa ndiye kiongozi pekee wa halali, lakini baba-wakwe zake na shemeji yake walipendelea uongozi kulingana na ukubwa. Mvutano kati yao ulisababisha kuundwa kwa vikundi vya Sunni na Shia, ambavyo vimeleta mauaji mengi.

## Mfano wa nne wa michezo ya kisiasa katika Uislamu ni mabadiliko ya eneo la Ka'ba

Je! Unajua kwamba michezo ya kisiasa na mvutano katika Uislamu vilisababisha mabadiliko ya Ka”ba huko Becca au makka kutoka Petra nchini Jordani hadi kwa sasa Makka nchini Saudi Arabia? Hii ilitokea mwaka wa 64 baada ya Hijra au mwaka 683 baada ya Kristo. Ka'ba ya Petra ilikuwa eneo la hija kwa Muhammad, Abu Bakar, Omar, Othman na Ali. Wote walizaliwa na kulelewa Petra. Walikuwa hawajawahi kwenda Hija Makka ya sasa. Waquraishi (Ghorayshis) na wahashemu wote waliishi Petra. Si ajabu kwamba hata ufalme wa sasa katika Jordan unajiita wa kihashemu. Muhammad alikuwa Mhashemu. Ni wakati akiwa Petra ndipo alipojitangaza kuwa nabii. Ka'ba ya Petra iliharibiwa wakati wa Yazid ibn Muaviyah na Ka’ba mpya ilijengwa huko Saudi Arabia.

Watu wa Jordan wanashikilia vikali madai ya kwamba wao ni wahashemu pekee. Ufalme wa Jordan umeweka bendera kubwa katika mpaka wa Jordan na Saudi Arabia. Neno pekee kwenye bendera hii ni Wahashemu, ambalo lina maana sisi ni wayordani na wahashemu pekee na sio ninyi wa Saudi Arabia.

Napenda kwanza kukupa mrejesho kutoka kwenye Qura'ni na kisha kutoka kwenye vitabu vya Kihistoria ni kwa nini Makka ya sasa haiwezi kuwa Makka ya awali ya Muhammad. Kisha nitakuambia kwa nini Ka'ba ilifungwa katika Jordan na kujengwa huko Saudi Arabia.

*Makka ya sasa haifanani na Makka iliyotajwa katika Qura'ni*

Aya za Qura'ni kuhusu Ka'ba zinafanana na maelezo ya Petra badala ya Makka ya sasa. Sura Al-e Imran (3) katika mstari wa 96 na 97 inasema kuwa Ibrahimu alijenga mahali patakatifu huko Becca. Sura Al Fath (48) mstari wa 24 inazungumzia kuhusu jeshi la Uislamu ambalo lilishinda na kuitawala Ka'ba iliyokuwa kwenye bonde la Makka. Ni Ka'ba ya Petra ilikuwa katika bonde lakini hakuna bonde lolote karibia na Kaba ya sasa au katika maeneo ya karibu yake.

*Pia, Makka ya sasa haiendani na ushahidi wa kihistoria*

Unajua kwamba wapagani wa kabla ya Uislamu walifanya sherehe ya Hija pia. Maandiko ya awali kuhusu Ka'ba yanasema kwamba ilijengwa katika bonde. Wanahistoria na wataalamu wa mambo ya kale wanataja miji mingi huko Saudi Arabia na makabila mbalimbali ya kipagani kabla na wakati wa Muhammad, lakini hakuna mji katika kusini mwa Saudi Arabia unaoitwa jina la Makka. Je! Jiji la kidini muhimu sana na kubwa ambalo lilikuwa ni njia kuu ya biashara, linawezaje kujificha machoni mwa wanahistoria na wataalam wa mambo ya kale? Hawakuandika kuhusu mji huo, kwa sababu haukuwepo Saudi Arabia. Ulikuwepo nchiini Jordan. Ushahidi wote wa kihistoria unaonyesha kwamba Hija kuu za kabla ya Uislamu kwa ajili ya sherehe ya Hajj zilikuwa zinafanyika huko Petra, ambapo kulikuwa na jiwe leusi au Hajar-ol Asvad na Ka'ba au Beytol-Haram

Jiwe leusi hilo lilikuwa sababu moja wapo ya kuwavutia wahujaji kwenda Petra. Miaka 400 kabla ya Muhammad, mwanafalsafa wa Kigiriki Maximus wa Tiro alisema kuwa jiwe leusi lilikuwa Petra. Encyclopedia ya Kigiriki Suda (Souda) pia inaelezea ukweli kwamba jiwe leusi ilikuwa Petra.

Tabari, mwanahistoria maarufu wa Kiislam, anasema kwenye ukurasa wa 192-1984 katika kitabu chake cha historia kwamba Ibrahimu na Ishmaeli walijenga Ka'ba katika bonde. Katika ukurasa wa 712 hadi 713, Tabari anasema tena juu ya utoto wa Muhammad, akicheza na wavulana katika bonde kwenye mji mtakatifu. Na kulikuwa na kijito kidogo karibia na Ka'ba.

Kuna marejeo ya mashamba, miti ya matunda na mizabibu karibu na Kaba katika maandishi ya kale, lakini ni vigumu kuashiria ardhi yoyote yenye rutuba kwenye ardhi kavu ya Makka ya sasa. Karibu na Ka'ba ya sasa hakuna bonde wala mto wala mashamba wala miti ya matunda.

Historia inatupa taarifa zaidi kwamba mji mtakatifu ulizungukwa na kuta na milima. Mlango wa mji kulikuwa kati ya nyufa mbili au Thaniyas katika miamba ya milima. Muhammad aliingia katika mji kupitia nyufa hizi.

Jiji la Makka la sasa halina ishara yoyote ya kuta za kale, milima au miamba inayoizunguka na hakuna pa kuingilia kwa kupita kwenye njia ya nyufa za miamba. Lakini maelezo haya yote yanafanana na Petra ya sasa katika Jordan.

Milima miwili ya Safa na Marwah ni muhimu katika Hajj ya Kiislamu. Katika maandishi ya kale ya

kihistoria kuna milima miwili mikubwa huko Petra ambayo ilikuwa na sanamu na mahekalu kwa juu. Watu waliipanda milima kwa ngazi nyingi kwenda kuabudu sanamu. Katika Makka ya sasa kuna vilima viwili vidogo vilivyotengenezwa na watu ambavyo vinaitwa Safa na Marwa na viko ndani ya msikiti.

Mlima Hira ulikuwa na pango ambapo Muhammad alikaa muda mrefu akifunga na kuswali kama mpagani kabla ya kujiita nabii wa Kiislamu. Katika machapisho ya Kiislamu, Mlima Hira uliangaliana na mji na ulikuwa sehemu ya juu ya Makka. Lakini Mlima Hira wa leo uko mbali na Ka'ba na hauangaliani na mji.

Petra ni kaskazini mwa Madina na Makka ya sasa iko kusini. Lakini vitabu vya kihistoria vinatuambia kwamba majeshi ya Qurayshi daima yalishambulia Medina kutokea upande wa kaskazini. Pia, wakati wa Vita vya andaki', Medina ililindwa na andaki lilokuwa kati ya milima miwili upande wa kaskazini mwa jiji. Na majeshi ya Kiislamu yaliyokuwa yakiondoka Madina kwenda kuishambulia Makka daima walielekea kaskazini kutoka Medina kuelekea Petra badala ya kusini kuelekea Makka ya sasa. Kwa maana nyingine, jiji halisi takatifu au Makka lilikuwa kaskazini mwa Medina na sio kusini.

*Misikiti ya mwanzo pia ilielekezwa Petra*

Misikiti yote inapaswa kuangalia Ka'ba kulingana na mila ya Kiislamu. Misikiti iliyojengwa tangu wakati wa Muhammad hadi mwaka 107 Baada ya Hijra au mwaka wa 725 Baada ya Kristo yote inaangalia Petra. Katika miaka mia iliyofuata misikiti mpya ilianza kujengwa ikiangalia sehemu tofauti kwa sababu ya mvutano uliyokuwepo kati ya vikundi vya Kiislamu juu ya Ka'ba mbili. Katika mwaka wa 133 baada ya Hijra au mwaka 750 Baada ya Kristo serikali ya Abbasid nchini Iraq iliiteka Syria na ikafanya Baghdad kuwa makao makuu ya utawala wa Kiislamu. Tokea hapo misikiti ya Mashariki ya kati ilianza kuswali ikielekea Ka'ba mpya huko Saudi Arabia.

*Je! Mabadiliko haya ya kutoka Petra hadi Makka yalitokeaje?*

Miaka mitatu baada ya kifo cha Muhammad ambayo ni mwaka wa 64 baada ya Hijra au mwaka wa 683 Baada ya Kristo, Abdullah ibn az-Zubayr, gavana wa Petra alimwaasi khalifa Yazid wa nasaba ya Umayyad huko Dameski ya Siria na akajitangaza kuwa khalifa. Tabari anatuambia kwamba Abdullah aliibomoa Ka'ba na kuisawazisha, akachukua lile jiwe leusi na kuhamia eneo la mbali huko kuliko na Makka ya sasa. Alifanya hivyo ili kujiweka mbali na kulipiziwa kisasi na Waumayyad, na pia ili kujenga Kaaba mpya na

kuliweka jiwe leusi huko kwa ajili ya kuwavutia watu kwenda hija kwenye Ka'ba mpya. Alijua kwamba mioyo ya Waislamu ilipaswa kuwa popote pale jiwe leusi lilipokuwa.

Watawala watatu wa Umayyad walifariki wakati huu, mmoja baada ya mwingine, na kusababisha matatizo ya ndani ya serikali ya Umayyad na wakakosa nguvu ya kupigana Abdullah ili kulirejesha lile jiwe leusi Petra. Udhaifu wa serikali ya Umayyad ulisababisha Abdullah kufanikiwa katika jitihada zake za kuanzisha Ka'ba mpya, pamoja na kituo cha Hija na mwelekeo wa swala kwa Waislamu.

Katika mwaka wa 68 baada ya Hijra au mwaka wa 687 baada ya Kristo, kulikuwa na hija za kwenda maeneo tofauti. Wengine walikwenda Petra wakitumaini kwamba jiwe leusi litarejeshwa. Wengine walikwenda Makka ya sasa, kwa sababu jiwe leusi lilikuwa pale. Katika mwaka wa 71 baada ya Hijra au mwaka wa 689 Baada ya Kristo, mji wa Kufa nchini Iraq uliasi dhidi ya waumayyad na kujiunga na Abdullah katika kukuza Ka'ba mpya. Katika mwaka wa 94 baada ya Hijra au mwaka wa 713 Baada ya Kristo tetemeko la ardhi liliharibu sehemu kubwa ya Petra na kwahiyo mji ulitelekezwa. Wengi walitafsiri hilo kama adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa jiji la Petra na ni ishara ya kukubalika kwa Ka’ba mpya. Kisha mwaka wa 128

baada ya Hijra au mwaka wa 745 Baada ya Kristo tetemeko la ardhi lingine liliharibu majengo katika Syria na Jordan. Kwa hiyo matumaini yote ya kulirudisha jiwe leusi Petra yalipotea. Katika mwaka wa 133 baada ya Hijra au mwaka wa 750 Baada ya Kristo Abbasid wa Iraq wapindua waumayyad nchini Syria na Waislamu wengi katika Mashariki ya kati walianza kuomba wakielekea Ka'ba mpya huko Saudi Arabia.

*Bado kulikuwa na wapinzani wa Ka'ba mpya na Makka.*

Waqarmatia waliyoasi dhidi ya waabbasid na kuichukua Bahrain, walipinga vikali hija yoyote ya kwenda Ka'ba mpya na waliwaua waislamu wengi waliokuwa safarini kwenda huko. Mwaka wa 930 Baada ya Kristo, walivamia Makka ya sasa wakaliondoa jiwe leusi na kubaki nalo kwa miaka 21 bila kulirududisha kwa Waabbasid. Uondoaji wa jiwe leusi uliharibu kabisa tamaduni na taratibu zote za hija. Hatimaye, Waabbasid nchini Iraq waliwalipa kiasi kikubwa cha fedha Waqarmatia ili kulirudisha lile jiwe leusi. Jiwe leusi halikuwa tena kipande kimoja bali lilikuwa limevunjwa katika vipande kadhaa na Waqarmatia.

Je! Unaona jinsi gani michezo ya kisiasa na mivutano ilivyobadilisha hata makao matakatifu na muhimu

katika Uislamu kutoka Petra hadi Makka ya sasa? Je, unatambua kwamba Uislamu hauna vigezo muhimu vinavyo julikana, kila kiongozi anafanya chochote anachopenda? Je, siasa hizi zisizokuwa na msimamo zina manufaa yoyote kwenu? Hakuna.

Ninataka kukuambia mchezo mmoja zaidi wa kisiasa kwenye Uislamu na kisha nimalize.

## Mfano wa tano wa michezo ya kisiasa ya Kiislamu ni kuwa aridhi ya Israeli ni ya wa Wapalestina na sio Wayahudi

Sura Al Maeda (5) katika mstari wa 21 na 22 inasema kwamba Mwenyezi Mungu aliwapa Israeli Wayahudi na ni yao milele na si ya Wapalestina wala makundi mengine. Sura Al Isra (17) aya ya 104 inasema kwamba wana wa Israeli kaeni katika Nchi Takatifu na wakati wa ahadi utakapofika, Mungu atawakusanya Wayahudi wote waliotawanyikiia nchi mbalimbali kuwaleta israel.

Kinyume na mafundisho ya Qura'ni, ulifundishwa kuwa Wayahudi wanamiliki Israeli. Baadhi ya serikali na viongozi wa Kiislamu wamekuwa wakituma mamilioni ya dola kila mwaka kwa Wapalestina, Hezbollah na makundi mengine ili kuwafukuza Wayahudi kutoka Israeli, nchi ambayo Qura'ni inasema Mungu amewapa Wayahudi milele.

Je, si jambo la kusikitisha kwamba pesa nyingi hupotea katika kutekeleza uongo, wakati zingeweza kutumika kuwasaidia mamilioni ya watu maskini katika nchi za Kiislamu? Je, sio kitu cha kusikitisha kwamba vijana wengi wanashawishiwa kushiriki katika ugaidi dhidi ya Wayahudi kwa sababu tu ya uongo na michezo ya kisiasa? Viongozi wa Kiislamu wamekuwa wakiwaweka Waislamu gizani na uongo na michezo yao ya kisiasa. Hii imeyagharimu mataifa ya Kiislamu kuwa kiasi kikubwa. Unaweza tu kushinda udanganyifu, uongo na michezo ya kisiasa kwa kuwa kuelimishwa. Ni kwa kupitia Yesu Kristo tu tunaweza kushinda michezo hii ya kisiasa.

### Wakati wa Kutafakari 18

1. Ni kwa njia gani imani ambayo Mwenyezi Mungu ni mdanganyifu kuliko wote inathiri dini na maisha ya wafuasi wake?
2. Uongo na udanganyifu ni sahihi katika Uislamu katika nyakati fulani; hii inaitwa Taqiyya au Uongo au udanganyifu wa pale inapokubidi. Je, hii haimaanishi kwamba watu hufundishwa na Mwenyezi Mungu pia na dini yao kusema uongo na kudanganya?
3. Uongo na udanganyifu katika Uislamu ulifungua mlango wa michezo ya kisiasa. Toa mfano wa jinsi gani mchezo huu wa kisiasa uliziba njia ya

uwezekano wa kujenga mahusiano ya kweli na ya amani kati ya Waislamu?

4. Toa mifano wa namna gani uhalalishwaji uongo na udanganyifu uliishia kufanya mafundisho ya Kiislamu kuwa hatarini kubadilishwa mara kwa mara.
5. Je! Watu wanahitaji kujenga misingi ya maisha yao katika imani ambayo inakataa udanganyifu wote na uongo na kuwafundisha maadili mema tu? Kwa nini?
6. Nini kitatokea ikiwa Waislamu hawata tambua misingi bora?
7. Je, tuna wajibu wa kujenga ufahamu juu ya maadili bora kati ya Waislam?

## Faraja ya kujikwamua kutoka kwenye udanganyifu, Uongo na Michezo ya Kisiasa.

Ina uma sana mtu anapokudanganya au kukuficha ukweli. Kama vile ambavyo uongo na udanganyifu wa wengine unaweza kukuumiza, vivyo ndivyo uongo na udanganyifu wako pia unaweza kuwaumiza wengine. Inaumiza kwa kila mtu. Suluhisho ni wewe kujinasua wewe kwanza kabla ya kutarajia wengine kujinasua.

Itakuwa faraja kubwa kwako na familia yako kuwa huru dhidi ya uongo, udanganyifu na michezo ya kisiasa na kujenga maisha yako katika misingi ya ukweli na uaminifu. Itafanya kila mtu ajihisi yuko salama. Kwahiyo unahitaji kuifuata imani ambayo sio tu hairuhusu uongo, na udanganyifu bali ina ng'oa mizizi yake iliyo ndani ya moyo wako kwa kukuelewesha na kukuweka huru.

Katika majadiliano yangu ya awali nilizungumza namna unafiki uongo, udanganyifu na michezo ya kiasa ilivyoanzia kwenye Uislamu na kugharimu mataifa ya kiislamu pakubwa tangu mwanzo wa Uislamu.

### Namna ya kujilinda dhidi ya mchezo wa kisiasa

Unawezaje kujilinda dhidi ya mambo yasiyo na maadili ambayo ni sehemu ya siasa za Kiislamu? Huwezi, kwa

sababu Uislamu umeyaruhusu kupenya katika kila nyanja ya maisha. Qur'ani inasema kwamba Mwenyezi Mungu ni mdanganyifu kuliko wote. Hii ina wapa waislamu nafasi ya kuhalalisha udanganyifu na uongo wakiamini kuwa ni sawa kwa vile Mwenyezi Mungu pia huvitumia.

Umewahi kufikiri kuwa uongo, udanganyanyifu na ujanjaujanja au mchezo wowote usiofaa ni vikwazo kwa amani na utulivu popote au katika familia yako? Haijalishi unamdanganya nani, kuna unaweza kusababisha mtu huyo akujibu na kutumia visingizio na sababu kama zako. Wote wawili hamtaminiana. Kimsingi, pasipo kuaminiana hakuna amani wala utulivu. Ndiyo maana amani, utulivu na upendo wa kweli vinakosekani katika familia nyingi, kwa sababu udanganyifu na uongo vimeharibu uaminifu. Wanafamilia hujifunza kusema uongo na jinsi ya kuishi na udanganyifu. Wanaume na wanawake, wazazi na watoto wote wamejifunza jinsi gani na wapi pa kusema uongo. Je! hili si jambo la kuhuzunisha?

Sijawahi kusahau maneno ya profesa wa sheria wa chuo kikuu nilichohitumu shahada yangu ya kwanza huko nchini kwangu. Kwa umakini alisema , "Nashangaa kwa nini kuhonga hakuja halalishwa, kwa sababu kila mtu anafanya hivyo." Akasema pia, "Kwa nini tusioinyeshe maadili yetu ya kila siku kwa wengine

na kuwaambia wazi kwamba hakuna siku ipitayo maishani mwetu bila ya sisi kusema uongo na kudanganya "

Hii ni hali halisi katika nchi zote za Kiislamu. Maisha yao yameathiriwa na kanuni na maadili yasiyofaa ya Kiislamu na watu wengi hawaoni shida kutumia uongo na udanganyifu katika mahusiano yao. Kama inavyosemwa: "Tunaitana ndugu kwanza na kisha tunadanganyana."

**Ujasiri wa kushinda misingi ya giza na kuwa huru**

Kwa dhati naupenda ujasiri wa wanaume na wanawake ambao wanaona mambo yasiyofaa katika jamii na tamaduni zao, na kuwa na ujasiri wa yaonyesha wazi na kutafuta msaada wa kuvunja minyororo hii. Watu kama hao wana uwezo mkubwa wa kuachana na Uislamu na kutafuta njia bora zaidi.

Je! isingekuwa bora zaidi kuwa huru kutokana na maisha mabaya na kutembea katika nuru kama mwanga wa taa juu ya kilima ambapo kila mtu anaweza kufaidika nayo? Kila mtu - wewe, familia yako na wengine. Ni faraja na amani isiyopimika kuwa mfano wa nuru kwa familia yako badala ya kuwa mfano wa giza unaoendeleza uongo na udanganyifu. Utakuwa na wakati wa furaha sana pale maisha yako

yatakapobadilika na ukaweza kusema, "Sasa niko huru. Sasa ndiyo yangu ni ndiyo ya kweli, pia hapana yangu ni hapana ya kweli. Sihitaji kusema maneno ya kupotosha tena. Kwa sababu sasa nuru ni mfano wangu wa kuigwa, na sio giza." Hiki ndicho imani ya kweli inachofanya. Siyo tu haikufundisha udanganyifu na uongo, bali ina ng'oa mizizi yake iliyo moyoni mwako na kukufanya kuwa mkamilifu, na mwana wa mungu. Ndiyo, mwana wa Mungu. Utaweza kutembea na Mungu wa kweli, kuangaza kama wakala wake miongoni mwa watu na kuwa nuru kwao.

## Uislamu ni kikwazo cha kuepukana na uongo, udanganyifu na michezo ya kisiasa.

Nina uhakika wa 100% kwamba Uislamu ni kizuizi kwako kuweza kutembea na Mungu. Ndiyo sababu niliondoka katika Uislamu na nikawa mfuasi wa Yesu Kristo. Nilitaka kuwa na amani katika familia na mahusiano yangu na wengine, lakini Uislamu ulikuwa kizuizi kwasababu ya Taqiyah au uongo unaokubalika. Kuna wakati katika maisha yangu niligundua kuwa sikutaka kuuishi Uislamu tena. Sikujaribu kumwambia mke wangu, au wanafamilia, au marafiki au mtu yoyote mwingine, kwa sababu ya kuogopa adhabu ya Kiislamu. Uislamu unakuchukulia kama mfungwa. Uislamu hauamini katika uhuru na haukuruhusu kuondoka. Unayo machaguo mawili tu, ukiri ukweli na

ufe au useme uongo na uishi. Kwa kuwa kusema uongo na kuishi ni maarufu sana, wewe pia unakuwa kama viongozi na watu wengine, unasema uongo na kuishi. Lakini bahati iligonga mlango wangu nilipogundua kuwa nilihitaji kutafuta njia ya kujiondoa katika Uislamu uliyoniondolea amani na faraja. Nilikuwa na kiu ya amani na faraja ndani mwangu. Kiu hiyo ndiyo iliyo nisaidia kushinda mashinikizo ya Kiislamu ndani ya moyo wangu na kupata amani na faraja.

## Unaweza kuwa huru ukitaka

Unajua, ukiupata ulimwengu wote lakini ukakosa amani na utulivu moyoni, unahisi kuwa huna kitu. Ndipo utakapo amua kufanya kitu cha kuleta amani katika maisha yako. Tuna dhana katika lugha ya kiIrani ambayo inasema: "Una weza kama unataka." Kwa maneno mengine, ukitaka kitu, chukua hatua za kukusadia kukifanikisha, unaweza ukakipata. Nilichukua hatua kuelekea kwenye amani na faraja, na vilinijia. Ukiachana na maisha yako mauovu na kuchukua hatua kuelekea kwenye amani, Yesu Mfalme wa amani huchukua hatua mia moja kukufuata. Hiki ndicho kilichotokea kwangu. Nilihitaji kumruhusu Yesu Kristo na Injili Yake kuwa mwanga wa maisha yangu. Injili inasema katika kitabu cha 1 Yohana sura ya 2 mstari wa 21 kwamba hakuna uongo katika kweli. (NIV) Niliposoma jambo hilo, nilitambua kuwa

Uislamu hauwezi kuwa dini ya kweli kwa sababu inahalalisha uongo na udanganyifu. Wale sio wakweli na ni maadui wa mahusiano ya amani

Nabii Sulemani anasema katika kitabu chake Mithali sura ya 12 mstari wa 22: Midomo ya uongo ni chukizo kwa Bwana; Bali watendao uaminifu ndio furaha yake.(NIV) Mungu wa kweli huchukia, uongo na michezo ya kisiasa. Kwa nini? Kwa sababu vinaharibu amani na faraja kati yako na Mungu, na kati yako na wengine.

**Je! Unatamani Mungu kufurahishwa na kupendezwa nawe?**

Sio tu nilitaka kuwa na amani moyoni mwangu, katika familia na mahusiano yangu na wengine, lakini nilitaka pia kuwa na amani na Mungu wangu. Kisha angeweza kufurahishwa na kupendezwa nami kama Nabii Sulemani alivyosema.

Hakuna kimojawapo cha haya kingeweza kutokea kwangu ikiwa ningebaki kuwa Mwislamu. Lakini yote yamekuwa sehemu ya maisha yangu baada ya kumpa Yesu moyo wangu. Nuru ya Yesu Kristo ilivua na kuving'oa vitu vibaya vilivyo ndani mwangu, na kuniongoza kwenye chanzo cha upendo kamili, utakatifu, amani na faraja.

Mabadiliko ya maisha yangu yalimshangaza mke wangu, na kumtia moyo kuisoma Injili ya Yesu Kristo. Matokeo yake, alimpa Yesu moyo wake pia. Aligundua kuwa mahusiano ya amani katika ndoa ya wezekana kwa msaada wa Yesu na si Uislamu. Kwa kusoma injili alipata kuelewa vitu vingi. Kwa mfano, aligundua kuwa Yesu alisema mtu anapaswa kuwa na mke, au mume mmoja tu, mke na mume wanapaswa kupendana kama wanavyojipenda wenyewe. Alisema hivi, "hili ni jambo zuri sana, mke mmoja na mume mmoja!" Aliipenda. Alielewa kila kitu. Aligundua kuwa mume na mke, serikali na watu hawawezi kamwe kuwa na amani ikiwa wanaifuata imani ambayo inaruhusu uongo na udanganyifu. Aliuacha Uislamu na akamfuata Yesu Kristo.

Bila shaka unatamani kuwa na amani na faraja moyoni mwako. Ikiwa ndivyo, basi unahitaji kuchukua hatua ya kuitimiza tamaa hiyo ili kupata faraja maishani mwako, na kuondokana na usumbufu wowote maishani mwako.

Kwa hili, unahitaji kumfuata Yesu Kristo. Hakuna mtu mwingine anaweza kukupa amani na faraja ya kweli.

**Wakati wa Kufakari 19**

1. Je! huoni kuwa uongo na udanganyifu ni uvamizi wa haki na uhuru wa wengine?
2. Ikiwa tunawadanganya wengine, je haitaathiri maisha yetu na ya familia zetu? Kwa njia gani?
3. Kuna ugumu gani kwako kujilinda wewe na familia yako dhidi ya uongo, udanganyifu na michezo ya kisiasa wakati dini yako inavikaribisha? Ni njia ipi bora ya kuwa huru kama ni hivyo?
4. Injili ya Yesu Kristo inasema kuwa hakuna uongo katika ukweli. Je! Hii ina maana gani kwako kiroho na kimantiki?
5. Tunawezaje kumheshimu Yesu kwa mafundisho yake ya kuaminika?

## Hakuna wokovu nje ya Yesu

Injili ya Yesu Kristo katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 4 mstari wa 10 hadi 12 inasema wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. Kwa maneno mengine, hakuna mtu wala malaika wala dini au mila yoyote ya kidini, au tamaduni ulimwenguni kote ya kukuokoa kutoka kwenye dhambi na Shetani na kukupa uzima wa milele, bali Yesu Kristo.

**Yesu anawezaje kukuokoa?**

Ni nani awezaye kukuokoa isipokuwa Mungu au yeye aliye na nguvu za kumshinda Shetani? Anaweza kuweka huru kutoka kwenye utumwa wa Shetani na kuendelea kukuhakikishia usalama dhidi ya adha na mateso ya Shetani. Je, Yesu anawezaje kukuokoa kama yeye si Mungu? Injili inasema kwamba Yesu ni Mungu na Mwokozi wa wanadamu hakuna mwingine yoyote isipokuwa Yesu Kristo aliyekuja kuishi ulimwenguni kama Neno na Roho wa Mungu na kama udhihirisho wa Mungu Mwenyewe.

Ndiye huyu ambaye jina lake ni Imanueli maana yake Mungu pamoja nasi. Jina lake pia ni Yesu, maana yake Mkombozi na Mwokozi. Yeye pia huitwa Masihi na maana yake ni mpakwa mafuta na mwenye uweza wa

wokovu. Je, kuna sababu za kiroho, na za msingi juu ya madai ya Injili ambayo hushawishi, mioyo na dhamiri za watu kumfuata Yesu? Je! Injili inathibitisha kwamba Yesu ni Mungu Mwenyewe na anaweza kuwaonyesha watu njia ya wokovu na kwenda mbinguni?

**Unabii kuhusu Yesu na utimilifu wake**

Kabla ya kuonyesha sababu za Injili niruhusu kwanza nikusomee baadhi ya unabii uliosemwa juu ya Yesu karne nyingi kabla ya ujio wake. Kuna unabii zaidi ya 300, amabo manabii kabla Yesu aliwatabiri juu yake. Injili inatupa muhtasari wa imani ya manabii hao kuhusu Yesu Kristo katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 10 mstari wa 43. Inasema: "Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi." (CEV)

Unabii huu ni wa ajabu na kushangaza. ulitabiriwa tangu miaka ya 1200 hadi 400 kabla ya Yesu na wote ulitimizwa na Yesu baada ya kuzaliwa kwake hadi alipo paa kwenda mbinguni. Nitagusia juu ya unabii kadhaa kati yao.

Karibia miaka mia saba kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo nabii Isaya alitabiri juu yake na kusema: Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye

atamwita jina lake Imanueli.. (Isaya 7:14, MKJV) Imanueli inamaanisha Mungu pamoja nasi.

Isaya alitabiri tena (Isaya 9: 6-7): Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; Kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo. .(MKJV)

Angalia ambacho nabii Daudi anasema katika Zaburi ya 45 mstari wa 6 kuhusu Yesu: "Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele, Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili. "(CEV)

Kwa hiyo karne  nyingi kabla ya Yesu manabii wa Biblia waliona Mungu alipenda kujidhihirisha  kama mwanadamu ili kuweza kuwafikia wanadamu na kuanzisha mahusiano ya karibu nao. Waliamini kwamba Mungu angeonyesha utimilifu wake kupitia mwili wa Yesu Kristo ili kuvunja ufalme wa Shetani na kuanzisha ufalme wa mbinguni mioyoni mwa watu tangu sasa hadi mwisho. Jinsi matukio ya mbele yalivyo kuwa yakipita akilini mwao katika maono walikaza macho yao kutazamia nyakati za utukufu

ambapo Mungu mwenyewe angejithihirisha kupitia Yesu Kristo duniani ili kuleta upendo, furaha na amani dhidi ya vita na chuki. Walimwona Yesu Kristo, Umungu Wake uliyo kamilika na kama Mfalme wa Amani, akipindua ufalme wa giza na kuuangaza ulimwengu. Waliona pia kuwa mamlaka yake ya kiroho yalikuwa imara kiasi kwamba hakuna mtu mbinguni wala duniani angeweza kuyapindua. Ndiyo maana nabii Isaya alisema, "Ufalme wake na amani havina mwisho." Kwa sababu hiyo, alisema kuwa Mtoto aliyezaliwa na Bikira ataitwa Mungu muweza wa yote

Watu walisikia unabii huu na daima walikuwa wanasubiri Mungu aje na kukaa kati yao na kuwakomboa kutoka kwenye taabu zao zote. Yesu alizaliwa kisha wakaona sifa zote za Mungu ndani yake. Walimwona akituliza dhoruba baharini. Walimwona akiwafufua wafu, akiwafanya vipofu kuona, akiwaponya wale waliopooza na kila aina ya ugonjwa. Hata yeye alidai kuwa yeyote aliyemwona alikuwa amemwona Baba wa mbinguni.

## Utimilifu wote wa Mungu ulikaa ndani ya Yesu

Injili inasema katika kitabu cha Waebrania sura ya 1 mstari wa 3: Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;

(CEV) Sura hiyo hiyo ya kitabu cha Waebrania mstari wa 8 inathibitisha kile Nabii Daudi alichosema juu ya Yesu: "Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili. " (CEV)

Injili inasema pia katika Wakolosai sura ya 1 mstari wa 19 kwamba ukamilifu wa Mungu wote ulikaa ndani ya Yesu Kristo. Kwa maneno mengine, Yesu ni Mungu, Mwenye nguvu za kufanya kila kitu na hakuna asichoweza kufanya. Mtume wa Yesu Kristo Paulo katika barua yake kwa Wafilipi sura ya 4 mstari wa 13 anasema : "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. " (ESV)

## Mungu alijifunua mwenyewe katika Yesu kwa ajili ya wokovu wa watu

Hivyo hadithi nzima ya Biblia tangu mwanzo hadi mwisho ni msingi wa imani kwamba Mungu ndiye mwokozi pekee na anajifunua mwenyewe katika Yesu kuwaokoa watu, kuwasaidia wamshinde Shetani na kuwaongoza mbinguni.

Ikiwa unaamini uwepo wa Mungu, basi unahitaji pia kuamini kuwa Mungu ni Mwenye nguvu na anaweza kuwaokoa watu kutoka kwenye vifungo vya shetani na kila aina ya minyororo ya kiroho na ya kimwili. Pia unahitaji kuamini kuwa kama uumbaji ulivyohitaji Mungu kujidhihirisha mwenyewe na kuwaumba

Adamu na Eva, ndivyo wokovu pia unavyohitaji udhihirisho binafsi wa Mungu na uwepo wake ili kuwaokoa watu na kuendelea kuwahudumia. Kwa hiyo unahitaji kumruhusu Mungu achukue nafasi na kuujaza moyo mwako ili kusiwepo na nafasi ya shetani kukusumbua. Mungu hapendi kumpa shetani nafasi na wala shetani kumpa Mungu nafasi. Hawapendani na kamwe hawataki kuishi pamoja moyoni.

Kwa hiyo, lazima Mungu au shetani aishi ndani ya moyo wako. Ikiwa Shetani anaishi moyoni mwako, itamaanisha kuwa huna Mungu, wala haujaokolewa na wala huna uhakika wa wokovu. Lakini ukimpa Mungu nafasi ya kuishi moyoni mwako, basi utakuwa mtoto wa Mungu, utakwenda mbinguni na utakuwa na uhakika wa wokovu milele. Ndiyo sababu ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo unakuwa wa muhimu sana katika maisha yetu. Hakuna anayeweza kutuokoa kutoka kwenye mikono ya shetani isipokuwa Mungu akijidhihirisha kwetu binafsi ili kuimarisha mpango wake wa wokovu wetu, na kuushinda ufalme wa shetani ndani ya mioyoni yetu.

### Je! Mungu anaupinduaje ufalme wa shetani mioyoni mwetu na ni kwa jinsi gani anatekeleza mpango Wake katika maisha yetu?

Napenda kwanza kukwambia jinsi utawala wa shetani unavyo stawi ili iwe rahisi kuelewa kuanguka kwake.

Kwa kila nafsi ambayo shetani anaipata na kuitawala huwa chanzo chaa mwendelezo wa ufalme wake. Vivyo hivyo, kila mtu anayeondoka kutoka kwenye ufalme wake (shetani) nakuungana na Mungu huwa chanzo cha kuporomoka kwa ufalme wa shetani. Kwa maneno mengine, utaendeleza ufalme wa shetani ikiwa haujaokoka na hauna uhakika wa wokovu. Lakini utauangamiza ufalme wa shetani, ukimruhusu Yesu kukuokoa, kukupa uhakika na utambulisho wa mbinguni.

Haiwezekani kumshinda Shetani bila Yesu. Kwa kuwa Shetani ndiye mwalimu wa udanganyifu na uongo, anajifunua kwa njia nzuri za uongo na kwa njia nyingne yoyote iwezekanayo, hata kama nabii wa uongo, ili kukunasa. Kuna uwezekano zaidi wa kudanganywa ikiwa huna mwongozo mzuri maishani mwako. Ndiyo sababu nilikuambia kuwa ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo ni wa muhimu sana kwetu.

Hakuna mtu anayeweza kuwa mfano bora wa kuigwa maishani mwetu isipokuwa Mungu katika Yesu. Miongoni mwa wanadamu, kila mtu amempa nafasi shetani na kutenda dhambi. Hata Muhammad, nabii wa Uislamu, alisema katika Sura (7) Al Aaraf mstari wa 188 kwamba shetani alimgusa na kumfanya atende dhambi. Kila mtu amejihusisha na uvunjifu wa sheria, alipuuza haki za wengine na kwa hiari au bila kujua,

alifanya kazi ya shetani. Watu wenye dhambi hawawezi kuwa mifano mizuri. Mungu pekee asiye na dhambi na aliyejidhihirisha kama Yesu asiye na dhambi ndiye anafaa kuwa mfano mzuri kwetu. Alijionyesha kwetu kupitia Yesu ili kwamba tupate kuelewa sifa za mfano mzuri ambaye anaweza kutufanya washindi katika kila eneo la maisha iwe kifalsafa, kiimani, kijamii, kisiasa au kimaadili.

Yesu alionyesha mfano bora kwa kupitia maisha yake ya duniani na kuthibitisha kupitia matendo yake yaliyoandikwa katika Injili. Anatufundisha kifalsafa kwamba Mungu, tofauti na dini nyingine, hajificha bali daima anapatikana na yuko tayari kukaa ndani ya mioyo yetu na kutulinda dhidi ya shetani ambaye mpango wake ni kutufisha. Pia anatufundisha kiimani kuwa Mungu ni mtakatifu, mwenye haki, upendo, mpole, na mpenda amani na kamwe hana ushirika na shetani. Ingawa tayari tumeona katika mistari ya mwanzo ya Sura Al Jinn (72) katika Qur'ani kwamba mungu wa Uislamu hutumia mapepo kueneza dini yake, Uislamu.

Maisha na mafundisho ya Yesu hapa duniani vimeonyesha wazi kwamba mtu yeyote au mungu ambaye anashirikiana na shetani na mapepo si wakweli na hawezi kuwaokoa watu. Ndiyo sababu watu wanahitaji kumtafuta mwokozi wa kweli. Yesu pia

anatufundisha kijamii, kimaadili na kisiasa kuwa mfano bora hutuongoza kwenye upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, uaminifu, upole, na mahusiano ya kujidhibiti. Yeyote anaye fanya kinyume na maadili haya hawezi kuwaongoza watu kwenye wokovu au kwa unganisha na Mungu. Kwa hivyo, sasa unaelewa katika kila nyanja kwa nini hakuna jina lolote mbinguni au duniani isipokuwa Jina la Yesu Kristo ambalo tunapaswa kuokolewa nalo. Ndiyo sababu Injili inatuambia: Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. (Luka 19:10)

Waliyopotea ni wale ambao hawajaokoka, wasiyo na uhakika wa wokovu na mara nyingi hawana ulizi dhidi ya mashambulizi na mitego ya shetani. Wakati pekee ambao shetani hawezi kutugusa na kutudanganya ni wakati tunapokuwa wa ufalme wa mbinguni tukilindwa chini ya uongozi na Roho wa Yesu Kristo. Watu wengi ulimwenguni wanafuata dini kwa sababu tu wazazi au jamaa zao wanaifuata dini hiyo. Hawajui kuwa dini yao haiwezi kuwafunulia Mungu ili Mungu awaweke chini ya mbawa zake dhidi ya dhambi na Shetani. Lakini tamaa ya Mungu kwetu ni kuifuata imani ambayo tunajua ni ya kweli, tuwe na sababu za ukweli wake, inaweza kutuokoa na kutuongoza katika njia ya haki kwenda mbinguni.

Nina furaha na bahati kwamba macho yangu yalifunguliwa na nilitambua kuwa uhusiano wangu binafsi na Mungu ulikuwa muhimu zaidi kwa Mungu kuliko kila kitu kingine. Kwa hiyo, nilijielekeza kwenye shauku ya kimungu kwa ajili ya wokovu wangu, nikatafuta mfano bora na kumwona Yesu. Nimeona sababu nzuri kuwa Yesu ndiye njia bora, chanzo cha ukweli na uzima. Yeye pekee ndiye wa kuwaokoa watu. Na nilimpa maisha yangu. Unaweza kufanya hivyo na kumwamini pia. Anaweza kukuokoa pia.

**Wakati wa Kufakari 20**

1. Watu wanaamini kwamba Mungu yuko kila mahali. Ikiwa ndivyo, huoni kuwa anaweza kujidhihirisha kwako popote ulipo?
2. Ikiwa Mungu ni Mungu anayejionyesha, ni nini kinatuzuia kuamini ushuhuda wa wale waliomwona Mungu?
3. Mungu alimuumba mwanadamu kwa mikono na pumzi yake binafsi, hufikiri kuwa katika wokovu (upya wa kiroho) uwepo binafsi wa Mungu ni wa muhimu pia?
4. Je, si vizuri kukumbatiwa na kuokolewa na Mungu mwenyewe?
5. Musa alisema kuwa Mungu alijifunua kwake kama moto. Pia alizungumza na Mungu uso kwa uso. Injili inasema kwamba Mungu alijithihirisha katika

Yesu kuuokoa ulimwengu. Unafikiria nini, je! Mungu hawezi kujidhihirisha Mwenyewe kwa njia yoyote anayotaka?

6. Kuna umuhimu gani kwa Mungu kujihusisha binafsi (kwa kuwa mfano wa mwanadamu) kuwaokoa watu?
7. Dini nyingine zote zinaacha watu waokoke kwa jitihada zao, lakini Injili inasema kuwa Mungu pekee ndiye anaweza kuokoa. Ni wokovu gani wa kuaminiwa zaidi - wa mwanadamu au wa Mungu?
8. Kama unataka kuokolewa na Mungu, basi unahitaji kumfuata Yesu Kristo kwa sababu ni katika imani kwa Yesu Kristo tu Mungu ni mwokozi.

# Yesu ni Njia, kweli na Uzima

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. (Yohana 14: 6, MKJV)

Watu wote wanaomwamini Mungu wanapenda kuwa na uhakika wa kuwa na Mungu milele. Yesu anatoa uhakika huu wenye faraja kwa watu kitu ambachoo hakuna mtu aliyeweza kufanya kabla. Anasema kuwa Yeye ndiye Njia na anaweza kuwapeleka watu mbinguni milele.

## Yesu ndiye njia ya kwenda mbinguni

Yesu hazungumzi kama nabii ambaye husema kama ukifanya hiki au kile utaweza kwenda mbinguni. Anasema kuwa yeye ndiye Njia ya mbinguni. Mtu yeyote anayemwamini ataingia mbinguni. Kwa hiyo Yesu si kama manabii ambao walionyesha njia kwa wafuasi wao lakini hawakuweza kufanya zaidi ya hapo. Yeye badala yake alionyesha kupaa kwake mbinguni. Wanafunzi wake na mamia ya wengine walimwona akipaa mbinguni  na kumwamini yeye  aliyesema kuwa atawapeleka wafuasi Wake mbinguni alipo. Kwa hiyo, Yesu ndiye Njia. Wewe na mimi tunahitaji kumwamini ikiwa tunataka kwenda kwa Mungu mbinguni na kuokolewa milele.

Unajua mtu yeyote anayetaka kutupa habari njema lazima awe mfano wa habari hio njema? Nabii wa Uislamu alisema kwamba unaweza kwenda mbinguni, lakini mwenyewe hakuwa na uhakika ya kwenda mbinguni wala hakuweza kuonyesha kupaa kwake mbinguni kama Yesu alivyofanya.

Baada ya Muhammad kufa, wafuasi wake walichelewesha mazishi. Kwa kuamini kwamba hakustahili kuzikwa chini kwenye udongo, walitarajia apae kwenda mbinguni kama Yesu. Haikutokea, na matokeo yake, mmoja wa wafuasi wake aliwashawishi wengine kuwa Muhammad alikuwa kama wao na alipaswakufa kama wao. Kwa maneno mengine, hakuwa kama Yesu aliyeweza kufufuka kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni.

Hakuna aliye kama Yesu. Yeye alishinda kifo na sasa ameketi kwenye kiti cha enzi na anaweza kutupeleka wewe na mimi mbinguni tukiamua kumfuata.

**Yesu alisema kuwa Yeye ndiye ukweli.**

Hatuwezi kuelewa madai haya ya Yesu isipokuwa tukielewa ukweli ni nini. Ukweli ni kuwasilisha jambo kama lilivyo. Kamwe hauwezi kuvumilia taswira faki ya mambo. Kwa mfano, ukweli unamwonyesha Mungu, kama mtu asiye na uongo au udanganyifu kwa sababu asili yake ni mwenye haki na mtakatifu.

Yesu na Injili kamwe hawasemi Mungu mwongo au mdanganyifu, lakini Muhammad katika Qura'ni yake anasema Mungu ndiye mdanganyifu kuliko wote na anaruhusu udanganyifu katika mazingira fulani. Nikupa nukuu kutoka kwenye Qur'ani katika mazungumzo ya awali yanayoonyesha kuwa uongo na udanganyifu unakubalika kama maadili kwa ajili ya kuendeleza Uislamu. Katika Uislamu unaweza kutoa ushuhuda wa uongo ili kuangamiza maisha ya mpinzani au asiye Mwislamu.

Hivi havikubaliki kabisa katika Injili ya Yesu Kristo. Huruhusiwi kusema uongo au kutoa ushahidi wa uongo dhidi ya mtu yeyote, ikiwemo na adui yako, kwa sababu ukweli kamwe haukuzi uongo. Injili katika kitabu cha Yakobo sura ya 3 mstari wa 10 hadi 12 inasema: Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, haifai mambo hayo kuwa hivyo. Je! Chemchemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu? Ndugu zangu, Je! Mtini waweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa tini? Kadhalika chemchemi haiwezi kutoa maji ya chumvi na maji matamu. (MKJV) Kwa namna hiyo, kama ukweli ni chemchemi mioyoni mwetu, ndimi zetu lazima zizungumze ukweli. Lakini kama tukisema uongo au kudanganya ina maana kuwa uovu ni chemchemi ya mioyo yetu, na si ukweli.

Kimwa cha Mungu kimenena kutoka moyoni mwake. Moyo wake ni mahali pa ukweli thabit. Hakuna kiini chochote cha uongo au udanganyifu katika moyo wa Mungu; na kwa sababu hii Yeye hawezi kusema uongo wala kumdanganya wala kumwambia yeyote kusema uongo au kudanganya. Kwa hiyo, nabii au dini yoyote ambayo inahusisha uongo na udanganyifu na Mungu, bila kujali ni kwa sababu gani, haiwezi kuwa ya Mungu na ya kweli.

Maisha ya Yesu Kristo duniani yalikuwa ufunuo kamili wa ukweli wa Mungu bila ya uongo au udanganyifu wowote. Injili yake pia inakataa aina yoyote ya uongo na udanganyifu, hata ule unaokubidi. Kwa hiyo, Yesu yuko sahihi kudai na kusema kuwa Yeye ndiye ukweli. Hahusishi uongo na udanganyifu wowote na Mungu, kamwe hahimiza mtu yeyote kusema uongo au kudanganya, na hakuna uongo wala udanganyifu katika maneno na matendo Yake. Yeye ndiye chanzo cha ukweli, na ukweli wa maisha yake ya duniani ndiyo sababu ya sisi kumwamini sasa na hata milele.

**Yesu alisema kuwa Yeye ndiye Uzima.**

Injili inasema katika kitabu cha Yohana sura ya 1 mstari wa 4 kwamba katika Yesu kuna uzima, na uzima huo ni nuru ya watu. Masha yake ni uzima ambao unawapa watu maisha ya milele, huonyesha watu njia nakuwapeleka mbinguni. Yesu anasema katika Injili

kwenye kitabu cha Yohana sura ya 5 mstari wa 25: Amin, amin, nawaambia, Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai. (MKJV) Yesu aliwafufua wafu na kugusa moyo wa wale walio hai na kuwapa uzima wa milele. Alithibitisha madai yake miongoni mwa watu kuwa yeye ndiye mtoa uzima.

Kazi ya Kristo sio kuwaongoza tu watu kama nabii, bali pia kusafisha na kuhuwisha mioyo yao kutokana na dhambi, na kuwapa uzima wa milele kwanza, na kisha kuwaongoza katika ukweli, utakatifu, haki, amani na upendo. Moyo hauwezi kuongozwa ikiwa haujatakaswa na kufanywa upya kwanza. Hakuna mtu anayeweza kusafisha, kuuimarisha na kuongoza moyo kwenye ukweli isipokuwa Yeye aliye uzima na chanzo cha uzima. Yesu ndiye mtu huyo. Kama uzima na chanzo cha uzima, Yeye ndiye mtoa uzima. Kwa hiyo, Yesu ndiye njia ya mbinguni. Yeye pekee ndiye Njia ya kumfunua Mungu na kumfanya aweze kupatikana katika maisha yetu ya kila siku.

*Katika Njia ya Yesu Kristo hakuna pazia kati ya Mungu na watu*

Katika yeye watu wanaweza kuwa na Mungu, kuzungumza na kusikia sauti yake moja kwa moja na kuungana na Yeye. Lakini Qura'ni katika Sura Ash Shura (42) mstari wa 51 inasema kuwa kuna pazia kati

ya Muhammad na mungu wake, na mungu wa Uislamu kamwe hazungumzi na yeyote moja kwa moja. Hapa unahitaji kuiruhusu dhamiri yako kufanya uamuzi sahihi kati ya njia za Muhammad au za Yesu. Muhammad alifundisha kuwa katika njia yake kwa Mungu, daima kutakuwa na pazia kati yake na Mungu, lakini kizuizi hicho hakipo katika njia ya Yesu. Kwa hiyo, Yesu ndiye Njia ya kwenda Mbinguni.

Pili, Yesu tayari yuko mbinguni lakini sio vivyo kwa Muhammad kulingana na Qura'ni. Ni dhahiri kwamba aliye mbinguni anaweza kuwa Mwongozo sahihi na Njia ya kwenda mbinguni.

Tatu, ni wanaume na wanawake tu wa mbinguni wanaoweza kufika na kuwa na Mungu. Ikiwa unamfuata Yesu, na wewe unakuwa wa mbinguni pia kama yeye na utakuwa na Mungu milele. Kwa hiyo, Yesu Kristo ndiyo tumaini la kumfanya Mungu ajulikane kwa Waislamu na kwa wote.

Yesu ni tumaini la kuwaunganisha Waislamu na Mungu. Yesu ndiye tumaini pekee kwa Waislamu kumshinda shetani na kuwa huru siku ya hukumu. Yesu ndiye tumaini la kuwafanya Waislamu watu wambinguni. Weka imani yako kwa Yesu na upokee furaha ya milele ya wokovu.

Asante sana kwa uvumilivu wako tangu mwanzo wa mazungumzo yangu hadi mwisho. Natumaini na kuomba kwamba yalikuwa na yatakuwa na manufaa. Mungu akubariki.

**Muda wa Kutafakari 21**

1. Ni nini kinamchofanya Yesu awetofauti na nabii?
2. Yesu alisema Yeye ndiye Njia ya mbinguni. Je! Kuna ushahidi wowote juu ya hili?
3. Yesu niwambinguni, na hata sasa yuko Mbinguni, anajua njia ya mbinguni na anaweza kutuongoza kwenda mbinguni. Je, kuna chochote cha kukuzuia kumwamini sasa?
4. Yesu pia alisema kuwa Yeye ndiye ukweli. Je! Maisha yake ya duniani yanathibitisha madai Yake?
5. Ikiwa Yesu ni kweli, je, si vizuri kwako kumkubali kuwa mfano wako wa kweli?
6. Roho wauzima wa Mungu ulimjia Bikira Maria na akazaliwa mtoto mtakatifu mleta uzima. Ndiyo sababu Yesu alisema kuwa yeye ni uzima wa milele na ni chanzo na mtoa uzima. Ikiwa hujaweka imani yako kwake, tafadhali ufanye hivyo na upokee uzima wa milele.

## Bibliography

Muhammad Jarir Tabari, Tabari's History, "*The History of Prophets and Kings*"

Qurans: Nobel Koran, Pickthall, Yusuf Ali and Dr. Mohsin.

Scripture quotations are from The Holy Bible, King James Version (KJV) (public domain).

Scripture taken from the Holy Bible, Modern King James Version ®, Copyright © 1962 – 1998. By Jay P. Green, Sr. Used by permission of the copyright holder.

Scripture quotations marked are from ESV (The Holy Bible, English Standard Version ®), Copyright © 2001 by Crossway, a publishing ministry of Good News Publishers. Used by permission. All rights reserved.

Scripture quotations are from The Holy Bible, NEW INTERNATIONAL VESION ®, Copyright © 1973, 1978, 1984 by International Bible Society. Used by permission of Zondervan Publishing House. All rights reserved.

Scripture quotations are from the (CEV) Contemporary English Version Copyright ® 1991, 1992, 1995 by American Bible Society, used by permission.

The Mecca Question by Jeremy Smyth, Copyright © Jeremy Smyth, 2011.

https://en.wikipedia.org/wiki/First_they_came_...

https://en.wikipedia.org/wiki/Giraffe#Neck;

http://www.africam.com/wildlife/giraffe_drinking

Waislamu wanafundishwa tangu utotoni kwamba Uislamu ni dini ya mwisho na kamilifu. Viongozi na wasomi wa Kiislamu hufundisha hili bila kuwaruhusu waumini wao kupima Ushahidi wa dai hili kwa kulinganisha na imani zingine. Kwa kweli wamenyimwa uhuru waliopewa na Mungu na haki ya kuchagua imani na misingi bora, ambayo ni ya lazima katika kuendelea kimaisha.

***Ufahamu na Uhuru*** huwasaidia Waislamu kujinasua kutokana na uongo wa Kiislamu kwa kujifunza kutoka kwa mitazamo ya dini na tamaduni zingine. Kitabu hiki kimeanza kwa kuwataka Waislamu kuelewa kwamba hawataweza kuwa na mfumo bora wa imani na kuishi katika utamaduni bunifu bila kupata kwanza ufahamu binafsi. Kitabu kinaendelea kuelezea mafundisho ya msingi ya Uislamu, kulinganisha na kutofautisha vipengele muhimu vya imani ya Kiislamu na yale ya Imani ya Kikristo, ili Waislamu wawe na mtazamo wa kweli wa kutathmini madai ya Uislamu kuwa imani kamilifu.

**Dk. Daniel Shayesteh**, mwalimu wa zamani wa itikadi kali za Kiislamu na mwanasiasa, sasa ni mchambuzi na mwinjilisti wa Yesu Kristo. Kwa miongo miwili ya kusafiri duniani na idadi isiyohesabika ya mazungumzo na Waislamu na wengine wa imani tofauti, Danieli ana kipaji na uwezo wa kugusa akili na mioyo ya watu na kushirikisha upendo wa Kristo kwa nguvu ya kipekee.

Exodus From Darkness Inc@2016.
Haki zote zimehifadhiwa.
www.exodusfromdarkness.org

ISBN: 978-9987-859-98-6
9 789987 859986